

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Tatu – Tarehe 5 Septemba, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

DUA

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu!

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali mbali (Na. 4) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4), Bill, 2019*].

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria

Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4), Bill, 2019*].

MHE. JOYCE J. MUKYA (K.n.y MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA KATIBA NA SHERIA):

Maoni ya Msemadi Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4), Bill, 2019*].

MWENYEKITI: Asante, Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

Na. 30

Uchaguzi wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa – 2019

MHE. JOHN J. MNYIKA aliuliza:-

Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliwahi kupewa jukumu la nyongeza la kusimamia kura ya maoni ya mabadiliko ya Katiba kwa Sheria iliyotungwa na Bunge kwa kutumia Ibara ya 74(6)(e) ya Katiba ya Nchi:-

(a) Je, ni kwa nini Ibara ya 74(6)(e) isitumike ili Uchaguzi wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa wa Mwaka 2019 usimamiwe na Tume ya Taifa ya Uchaguzi badala ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI)?

(b) Je, ni kwa nini Serikali hajatekeleza makubaliano na Vyama ya mwaka 2014 ya kuwezesha Uchaguzi wa Vitongoji na Mitaa kutumia Daftari la Wapiga Kura liliolloreshwa badala ya Orodha ya Wakazi?

(c) Je, ni hatua gani Serikali imechukua kuhakikisha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2019 unakuwa huru na wa hak?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa John John Mnyika Mbunge wa Kibamba lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi yaliyoainishwa katika Ibara ya 74(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kusimamia uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiliani na kutekeleza majukumu mengine yoyote kwa mujibu wa sheria iliyoitungwa na Bunge. Jukumu la kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa si mionganini mwa majukumu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa mujibu wa Katiba isipokuwa ni jukumu la Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288. Hivyo, masharti ya Ibara ya 74(6)(e) ya Katiba hutumika tu pale ambapo kuna Sheria iliyoitungwa na Bunge inayoipatia Tume ya Taifa ya Uchaguzi majukumu mengine.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyo tangulia kueleza, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tume ya Taifa ya Uchaguzi haina Mamlaka ya kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Kutokana na msimamo huo wa Kikatiba uchaguzi wa Serikali za Mitaa hauwezi kutumia daftari la kudumu la wapiga kura kwa kuwa daftari hilo lipo chini ya usimamizi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa mujibu wa masharti ya Kifungu cha 12 cha Sheria ya Uchaguzi, Sura ya 343. Kwa msingi huo, makubaliano yoyote yaliyowahi kufanyika kuhusu matumizi ya daftari la kudumu la wapiga kura katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa yanapaswa kuzingatia masharti ya Kikatiba na sheria za nchi.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unakuwa huru na haki Serikali imeandaa Kanuni na Miongozo ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za Mwaka 2019 ambazo zimezingatia maoni yaliyotolewa na wadau mbalimbali wa uchaguzi vikiwemo vyama vyama siasa vyenye usajili wa kudumu Tanzania pamoja na asasi za kiraia.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Serikali imekwepa kujibu msingi wa swali kwa sababu msingi wa swali langu ni kwamba Ibara ya 74(6)(e) ya Katiba imesema Bunge linaweza kutunga sheria ya kuipa tume jukumu la kusimamia suala lingine lolote na Ibara hiyo ya Katiba pamoja na kuwa kwenye majukumu ya Tume kulikuwa hakuna jukumu la kusimamia kura ya maoni ya mabadilliko ya Katiba, sheria ikatungwa na Bunge ya kura ya maoni...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika uliza swali.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Sasa ndio najenga msingi wa swali kwa sababu amejibu tofauti kabisa. ni kwa nini Serikali imeogopa kuleta Bungeni Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambayo ingeondoa mamlaka kwa Waziri wa TAMISEMI ingeweka daftari la kudumu kutumika na ingepeleka majukumu yote kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili uchaguzi usimamiwe na Tume ya Uchaguzi badala ya kusimamiwa na Serikali yenye kwa maana ya Waziri wa TAMISEMI ambaye ni *interested part* ndio alazimike kutunga kanuni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwenye sehemu ya mwisho ya majibu amesema kwamba kanuni zimeandaliwa kushirikisha wadau, bahati nzuri nilikuwepo kwenye kikao kilichofanyika mwezi Aprili cha kujadili kanuni. Tumekaa kikao kama vyama, anasema vyama vimeshirikishwa; tumekaa kikao Aprili, Aprili hiyo hiyo tarehe 25 mwezi wa nne, Waziri akatoa Kanuni kwa siri zilizochapishwa, zimekuja kutolewa hadharani mwezi Agosti na Kanuni zile hazijazingatia maoni ya vyama, wadau na

tayari Kanuni hizo zimeanza kutumika vibaya, tunaona Wakuu wa Mikoa ambao ni viongozi wa kisiasa, Wakuu wa Wilaya, Maafisa Tarafa sasa ndio wanapewa jukumu la kusimamia uchaguzi wakati ni makada wa Chama cha Mapinduzi, kutakuwa na uchaguzi wa uhuru na haki katika mazingira kama hayo? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, majibu ya Serikali ni sahihi kulingana na swali ambalo ameliuliza. Nikirejea swali la Mheshimiwa Mbunge anasema je, ni kwa nini Ibara ya 74(6)(e) isitumike ili kusimamia uchaguzi wa Vitongoji na Vijiji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hoja anayosema swali la kwanza kwamba kwa nini Serikali isilette mabadiliko ya Katiba, Serikali inaweza ikaleta Muswada wa kubadilisha Katiba lakini pia Mheshimiwa Mbunge ana nafasi hiyo na hajafanya hivyo. Kwa hiyo, angeleta mabadiliko hayo tungeyajadili lakini kwa sasa tunazungumza uchaguzi wa Serikali za Mitaa *as by now* kwa mujibu wa taratibu, kanuni na sheria zilizopo utasimamiwa na Waziri mwenye dhamana, hakuna mabadiliko ya Katiba ambayo yamekwishafanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili; Mheshimiwa Mbunge ananiuliza kwamba kanuni hizi hazikuzingatia miongozo, sio kweli na yeye mwenyewe bahati nzuri amethibitisha kwamba alihudhuria, sasa mkiitwa kwenye kikao kujadili na kutoa maoni siyo lazima Serikali ichukue kila kitu mnachokisema, maoni yakitolewa wataalam wanakaa, wanaangalia katiba, sheria, miongozo mbalimbali na *practice* ya kawaida halafu tunaamua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni hizo sasa hivi wala hazikumpa dhamana yoyote Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya kwamba wakasimamie uchaguzi, muongozo huu hapa. Mheshimiwa Mnyika Naibu Katibu Mkuu wa chama

chake cha CHADEMA alikuwepo siku hiyo Mheshimiwa Waziri anatangaza kanuni, amepewa kanuni za uchaguzi, mwongozo wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Mwongozo wa Mpiga kura. Na kanuni inasema pia asasi za kiraia na mtu ye yote yule anaweza akapewa hii akasoma na akaomba miongozo mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Mnyika asiwe ana hofu, Mheshimiwa Mnyika uchaguzi huu utakuwa ni huru na haki na kanuni imemeleza vizuri nani anapaswa kusimamia uchaguzi huu. Tujipange, tukutane kazini, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbewe.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana tukaona mambo haya ya uchaguzi ni mepesi lakini amani ya Taifa hili itapotea ama itaathirika kama tukipuuza masuala ya uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *subsidiary legislation* zozote zinazotungwa katika nchi hii leo, lazima kwa njia moja au nyingine ziwe *ratified* na Bunge. Sheria ndogondogo tunazositunga kabla hazijaanza kutumika kimsingi zinastahili kuletwa kuwa *ratified* na Bunge. Vikao vya wadau vinavyokaa ni maoni wala vikao vya wadau vinavyokaa kujadili *subsidiary legislation* ama *legislation* yote haviwezi kuwa mbadala wa Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Sheria Ndogo...

MBUNGE FULANI: Swalii, hatutaki hotuba.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Sheria Ndogo ya Bunge haijawahi kuona kabisa au kupitia na kuthibitisha ama kuzi-*accept* ama kutoa maoni kanuni hizi zilizotungwa na TAMISEMI. Ninachouliiza Mheshimiwa Waziri atueleze katika utamaduni huo ambako tayari kanuni zimeshaingizwa kazini, Kamati ya Sheria Ndogo

ya Bunge haikuzipitia kwa kisingizo kwamba wadau walizipitia ambaio sio Bunge. Je, jambo hili ni sahihi? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Asante Mheshimiwa Waziri majibu, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo kidogo kuhusu suala ambalo ameliibua Mheshimiwa Mbewe, amesema kwamba sheria ndogondogo zinapotungwa lazima kuletwaa Bungeni kabla ya kuanza kutumika, hiyo kwa mujibu wa utaratibu siyo sahihi na bahati nzuri Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo yupo hapa ataaeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Ndogo huwa zikishatayarishwa zinapelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uchambuzi yaani *vetting* na baada ya hapo Mwanasheria Mkuu wa Serikali humrudishia Waziri husika na Waziri yule anazi-gazette halafu baada ya hapo zinapelekwa kwenye kikao kinachofuata cha Bunge kwenye Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo kwa ajili ya kuchambuliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongeze kusema mtu anaweza kusema labda mchakato huo hautoi nafasi ya kuweza kuziangalia vizuri zile sheria ndogo, kimsingi sheria ndogo zote zinatungwa chini ya sheria mama na ipo misingi ya kisheria inayoelekeza namna gani sheria ndogo zitungwe na mojawapo ya misingi hiyo ni kwamba isipingane kimsingi na sheria mama. Na inapotokea kuna changamoto moja au mbili ile Kamati ya Bunge kuhusu sheria ndogo kutoa maoni na maelekezo yake na kama kuna changamoto yoyote inarekebishwa, kwa hiyo, hakuna tatizo kabisa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mlata!

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kupigania afya yangu, sasa hivi naendelea vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kumekuwa na upotoshwaji mkubwa sana kwa watu wasioitakia mema nchi hii, wamekuwa wakiweka dosari ambazo hazipo kwenye suala hili la uchaguzi. Je, Serikali imejipangaje kuwaelimisha zaidi Watanzania ukweli ambao wamekuwa wakifanya hivyo na uchaguzi umekuwa ni huru na ndio maana wapinzani ni wengi ndani ya Bunge, Madiwani, Wenyeviti na kadhalika. Mmejipangaje kuwaelimisha Watanzania hawa wanaopenda amani katika nchi yao? Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwanza nampongeza na kumpa pole sana kwa kupata shida ya afya na Mungu amemjalia na aendelee kuimarika Mbunge mwenzetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni swali muhimu sana, nasema ni muhimu kwa sababu ni kweli kwamba hata swali la msingi la leo utaona ni swali ambalo limejaa tu hofu bila sababu yoyote ile kwa sababu uchaguzi wa Serikali za Mitaa si kwamba unaanza kufanyika kwa mara ya kwanza Tanzania leo mwaka huu, ni uchaguzi ambao tumefanya awamu kadhaa huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na bahati nzuri nilliyesimama hapa pia nimekuwa Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa kuitia chama cha upinzani CHADEMA kama ingekuwa uchaguzi sio huru mwenyewe mwaka 2014 nisingekuwa Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa pale Kivule, nilishinda uchaguzi na nikawa Mwenyekiti wa Mtaa kuitia chao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili; uchaguzi wa nchi hii ni huru, nilikuwa Mbunge kuitia CHADEMA, nilishinda kwa kanuni hizihizi na Katiba hiihii iliyopo na leo nimesimama

mbele yako kama Mbunge kupitia Chama cha Mapinduzi. Hii yenyewe inaonesha kwamba uchaguzi wa Tanzania ni huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye Serikali za Mitaa, mchakato wa uchaguzi huu kanuni zimeandaliwa na wadau waliitwa wakatoa maoni yao, tukachakata na wataalam wakashauri kanuni hii hapa imeshatolewa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi ameshatoa nakala hizi kwa Wakuu wa Mikoa wote na vyama vya siasa wanazo hizi kanuni. Hakuna mtu ambaye amekuja mbele ya Watanzania akakosoa kifungu chochote kwenye kanuni kwamba kimekinzana na Katiba kina mapungufu, wamepokea na wameridhia, tunaendelea na mchakato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeenda mbali zaidi, tumetoa mwongozo kwa wapiga kura, hapa inaeleza nani ana sifa za kugombea, mchakato ndani ya chama namna mbalimbali za michakato na usimamizi na imetaja nani anapaswa kusimamia uchaguzi na imewakataa mpaka Watendaji wa Kata ukisoma vizuri. Kwa hiyo, nitashangaa sana watu ambao wanakuja hapa wana hofu ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tarafa, Watendaji na watumishi wa Serikali lakini kanuni imeeleza ni nani ambaye anapasa kusimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitabu cha tatu ambacho kimetolewa ni Mwongozo kwa Mpiga Kura na kanuni imeeleza kama mtu ye yeyote ama asasi za kiraia anataka kutoa elimu ya uraia, kuchunguza ndani na nje kanuni imetoe mwongozo kuna utaratibu wa kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme kwamba Serikali imejipanga vizuri sana kuendesha uchaguzi wa Serikali za Mitaa na utasimamiwa na Waziri mwenye dhamana na Watanzania wapo tayari sana kufanya uchaguzi huru na haki, wapate viongozi wao, wazingatие maelekezo ya Serikali ili tupate viongozi ambao watatuwakilisha. Wananchi wasiwe na hofu, uchaguzi utasimamiwa na vyombo viro na kama kuna mtu ye yeyote ambaye ana jambo lolote ambalo

anadhani kwamba linataka maelezo, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ipo wazi, tunawakaribisha tupate maoni tujadiliane kwa maana ya kuboresha,

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Na. 31

Kurekebisha Kasoro za Mfuko wa Kaya Maskini

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI (K.n.y. MHE. ENG.
RAMO M. MAKANI) aliuliza:-**

Utekelezaji wa Mpango wa Kaya Maskini katika Jimbo la Tunduru Kaskazini una changamoto nyingi sana zinazolalamikiwa na Wananchi:-

Je, Serikali itachukua hatua zipi za makusudi kurekebisha kasoro hizo ili wananchi wapate kunufaika vema zaidi na huduma za Mfuko huo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora, naomba kujibu swali la Eng. Ramo Matala Makani kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa Mheshimiwa Eng. Makani hakutaja waziwazi changamoto za utekelezaji wa mpango kwenye Jimbo lake, Serikali kupitia *TASAF*, changamoto kubwa ambayo Mpango unakumbana nao ni kilio kutoka kwa baadhi ya wananchi maskini ambao hawajafikiwa na huduma za Mpango huo kwenye Viji/ Mitaa/Shehia takribani 5,693 ambavyo havikufikiwa katika Awamu ya Kwanza ya Mpango huu wa kunusuru kaya maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Makani na Wabunge wengine kwamba utaratibu umeshaandaliwa wa kuweza kufika kwenye Vijiji/ Mitaa/Shehia hizo mara tu baada ya mpango kuanza utekelezaji. Katika awamu hii, TASAF imejipanga vizuri kuhakikisha kuwa yale malalamiko ya upendeleo, ubaguzi na kuachwa kwa watu maskini kuandikishwa kwenye Mpango huu hayajirudii na mifumo ya kielekroniki itatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge na viongozi wote kwamba muda utakapofika wahakikishe wanalisimamia vizuri zoezi la utambuzi wa walengwa ili wale wanaostahili basi waweze kuwa wameandikishwa kwenye mpango huu. Hatua kali zitachukuliwa kwa viongozi na watumishi katika ngazi zote ambao katika maeneo yao watabainika kuwepo watu au kaya zisizo na vigezo kwenye Awamu ya Pili ya Mpango huu wa Kunusuru Kaya Maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni malalamiko ya walengwa kuhusu makato ya fedha kipindi cha malipo. Suala hili walengwa wanaendelea kuelemishwa kwa nini makato yanatokea. Sababu ya kukatwa fedha zao ni kutokana na kutotimiza masharti ya kupokea ruzuku hasa kwa kaya zenye watoto walio shulenii halafu hawaendi shule na wale wanaotakiwa kuhudhuria kliniki ambao ni watoto wenye umri wa miaka mitano na hawafanyi hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo kaya itashindwa kutimiza masharti ya kutimiza watoto hao kutohudhuria shulenii au kutopeleka watoto kliniki fedha hizo zinakatwa kama adhabu. Nimuombe Mheshimiwa Makani na Wabunge wengine wote, mnapoenda kwenye ziara katika Majimbo yenu ndugu zangu tusaidiane kutoa elimu hii ili kuepusha malalamiko ambayo sio ya lazima. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jacqueline.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza maswali ya nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Eng. Makani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, nimpongeze Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Naibu wake kwa utendaji mzuri wa kazi. Pamoja na majibu hayo naomba maswali madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, ni lini Serikali itashughulikia changamoto katika kaya za vijiji kwenye Tarafa za Nakapanya, Matemanga, Nampungu na Mlingoti? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni lini Serikali itapitia upya utaratibu wake na kuhakikisha kwamba wanufaika wanakuwa ni wale wenye kaya maskini na siyo wale wenye uwezo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu maswali madogo mawili ya nyongeza wifi yangu Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama mwanamke naomba nimpongeze kwa sababu walengwa wengi ambao ni wanufaika wa kaya maskini ni wanawake kwa sababu wameonyesha uaminifu mkubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika swali kuhusu Tarafa za Napakanya, Matemanga, Nampungu na Mlingoti, naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi *TASAF* tumekuwa katika Awamu ya Tatu na mwezi ujao Oktoba tunategemea kuzindua rasmi sehemu ile ya pili

ambapo tumemaliza sehemu ya kwanza. Hizi Tarafa zote nne ambazo amezisema basi walengwa wote wale ambao hawajaflkiwa watafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swalii la pili, naomba niseme kwamba Serikali ya Awamu ya Tano kupitia Mpango huu wa Kunusuru Kaya Maskini tumejipanga kuboresha zaidi kuhakikisha kwamba walengwa wote ambao tulikuwa tunawawezesha na sasa hivi wameweza kusimama wenyewe, tutakuwa na mpango mkakati kuhakikisha kwamba wamefuzu tunaita *graduation* ili sasa waweze *ku-phaseout* ili tuweze kusaidia wale wengine ambao hawaijivezi kwa sababu wasiojiweza, maskini sana, wazee, walemavu wapo kila siku basi tuendelee kuwahudumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, tumeboresha mfumo kuhakikisha kwamba kuanzia sasa hivi tutakwenda kielektroniki ili kuondokana na suala zima la kaya hewa. Niwatake Wabunge wote na Watanzania wote kuhakikisha kwamba wanaendelea kuunga mkono juhudii hizi za Serikali ya Awamu ya Tano kuhakikisha kwamba walengwa wote wanaotokana na kaya maskini ndiyo hao wanaostahili kupewa misaada yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwamoto na Mheshimiwa Lubeleje.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Mpango huu wa Kunusuru Kaya Maskini (*TASAF*) umefanikiwa kwa kiwango kikubwa na umenufaisha nchi na sisi Wabunge tukiwa wamojawapo. Je, Serikali itakuwa sasa tayari kutoa takwimu ni Wilaya, Mkoa na Kijiji gani mpango huu umefanyika vizuri ili iwe mfano kwa Wilaya au Mikoa mingine ambayo imeshindwa kufanya vizuri?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja dogo la nyongeza la Mheshimiwa kaka yangu Mheshimiwa Mwamoto, kama ifauatvyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango mzima huu wa *TASAF*, takwimu zipo na muda wowote anapozihitaji tutampatia kwa sababu ni zoezi endelevu. Sisi kama *TASAF* tumejipanga kuonyesha kwamba sasa hivi tutakuwa tunaonyesha zaidi *multiply effect* ya walengwa wote na mpango mzima mpaka leo hii tumetumia shilingi ngapi ili kuonyesha kwamba *impact* yake inaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lubeleje.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Kamati yetu ya Utawala na Serikali za Mitaa tulipotembelea Mikoa ya Mwanza, Mara na Simiyu, tulikuta madaftari mengi wameorodheshwa watu ambao siyo walengwa, ni vijana ambao ni matajiri, wana mali na nyumba nzuri. Tulikwishatoa ushauri kwenye Wizara hii hawa vijana wote waondolewe. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, orodha ile mlihakiki na kuondoa majina hayo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu swali dogo la nyongeza Mzee wangu Mheshimiwa Lubeleje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli siku za nyuma kulikuwa na walengwa wengine ambao wana uwezo lakini walikuwa kwenye mpango. Serikali ya Awamu ya Tano hilo

tumelidhibiti na hao wote tuliwaondoa. Ndiyo maana pia katika jibu langu la nyongeza nimesema katika sehemu yetu hii ya pili tunakwenda kielektroniki kudhibiti wale wote ambao wanasema wanatokana na kaya maskini lakini kumbe ni kaya maskini hewa. Hilo tumelidhibiti na tumeboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na swali Na. 32 la Mheshimiwa Mwantum Dau.

Na. 32

Kuvinusuru Visiwa vyta Unguja na Pemba

MHE. MWANTUM DAU HAJI aliuliza:-

Kasi ya mmomonyoko wa ardhi na uhaba wa udongo katika Visiwa vyta Unguja na Pemba inatishia uhai wa Visiwa hivyo:-

Je, ni hatua zippi za makusudi zimechukuliwa katika kuvinusuru Visiwa hivyo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), naomba nichukue fursa hii sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mwantum Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Visiwa vyta Unguja na Pemba vina maeneo takribani 148 yaliyoathirika na mabadiliko ya tabianchi (Pemba 125 na Unguja 23). Athari hizi ni pamoja na mmomonyoko wa fukwe na kuingia kwa maji ya bahari katika mashamba na makazi ya watu. Ili kuvinusuru visiwa hivi dhidi ya athari ya mabadiliko ya tabianchi, Serikali

imechukua hatua mbalimbali kuitia miradi inayofadhiliwa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuitia Mradi wa kujenga uwezo wa jamii kuhimili athari ya mabadiliko ya tabianchi (*LDCF*) ambao umetekelizwa mwaka 2012 - 2018, shughuli zifuatazo zimefanyika: Ujenzi wa kuta mbili za mita 25 kila moja katika eneo la Kisiwa Panza - Pemba na ujenzi wa makinga bahari (*gloynes*) matano ya wastani wa urefu wa mita 100 kila moja katika eneo la urefu wa mita 538 Kilimani - Unguja; upandaji mikoko Pemba maeneo ya Kisiwa Panza hekta 200, Tumbe hekta 10, Ukele hekta 7 na Tovuni hekta 1; na upandaji mikoko Unguja maeneo ya Kisakasaka hekta 8 na Kilimani hekta 1.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kuitia Mradi wa Kupunguza Uhalibifu wa Ardhi na Kuongeza Uzalishaji wa Chakula katika Maeneo Kame nchini mwaka (2017 - 2022), shughuli zifuatazo zinategemewa kufanyika katika maeneo ya Micheweni, Kata ya Micheweni na Kiuyu Maziwang'ombe ambazo ni: Kujenga makinga maji katika mashamba (*dykes*) ili kuzuia maji ya bahari kuingia katika mashamba; kutoa elimu kuhusu kilimo kinachokabiliana na mabadiliko ya tabianchi kuitia mashamba darasa; upandaji wa miti ili kuhifadhi udongo na kutunza mazingira; na uanzishaji wa biashara ndogo ndogo ili kuwezesha jamii kuwa na shughuli mbadala za kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi; kudhibiti mmomonyoko wa udongo; na kukabiliana na uhaba wa udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwantum, jiandae Mheshimiwa Dkt. Sware.

MHE. MWANTUM DAU HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu ya kina kuhusu swali langu hili, nampongeza sana, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, yamekuwepo matukio ya ongezeko la kina cha bahari kiasi cha kuwepo kwa tishio la kimazingira katika baadhi ya maeneo. Je, Serikali inasema nini kuhusiana na suala hilo katika Visiwa vya Unguja na Pemba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tatizo hili ni la muda mrefu kweli, toka liliyyogundulika kuhusu mazingira katika Visiwa vyetu vya Pemba na Unguja. Mheshimiwa Naibu Waziri atakuja lini sasa Zanzibar kuangalia maeneo yaliyoathirika katika Visiwa vya Pemba na Unguja? Nataka unihakikishie utakuja lini Zanzibar mbele ya Bunge letu hilli.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mwantum Dau Haji kwani amekuwa mdau mzuri wa eneo hili la mazingira. Nimhakikishie tu kwamba katika miradi ambayo inaendelea na kama nilivyosema kwamba tunashirikiana vizuri na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar sasa tunaifanya tathmini. Katika tathmini ile ambayo tunaifanya kila baada ya miezi mitatu maana yake sasa nitakuja rasmi baada ya Bunge hilli, walau siku mbili hivi kwa ridhaa ya Mwenyekiti, ili tukishirikiana nawe na Wabunge wengine kwenye maeneo ya Pemba kuyaona hayo maeneo vizuri na kuhakikisha tunayapatia ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Sware.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Suala la mmomonyoko wa udongo ni kubwa na lipo dhahiri kabisa, ukiona mkusanyiko wa udongo na mchanga katika mapito ya njia za maji za mito. Kumekuwa pia na uchimbaji holela wa michanga hii, inazidi kuvunwa au pia vina nya maji vinakuwa vifupi na nyakati za mvua basi husababisha mafuriko. Wizara husika ina mkakati gani kuleta suluhisho katika suala hili ambalo ni muhimu sana na lina *effect* kubwa sana katika mazingira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Sware.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubaliane naye kumekuwa na changamoto kubwa sana ya mmomonyoko wa ardhi hasa kwenye maeneo ambayo kuna mapito ya maji. Eneo hili kwa kweli nikiri kabisa tumeendelea kulifanya kazi na limekuwa na changamoto kubwa. Mkakati uliopo ni kuhakikisha maeneo yote haya kwa kushirikiana na viongozi wa Halmashauri wanatupa taarifa zilizo rasmi ili kutengeneza miradi ya kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumekuwa tukitoa maelekezo kwenye Halmashauri husika ili kukabiliana na maeneo ambayo yanahitaji kupata ufumbuzi wa muda mfupi lakini yale ya muda mrefu Wizarani tunapata taarifa na tunachukua hatua stahiki.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar.

Na. 33

Uanzishwaji wa Benki ya Wanawake Zanzibar

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR aliuliza:-

Je, ni sababu gani zimekwamisha uanzishwaji wa Benki ya Wanawake kwa upande wa Zanzibar?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliari fu Bunge lako Tukufu kwamba kwa sasa hatuna Benki inayoitwa ya Benki Wanawake Tanzania, baada ya iliyokuwa Benki ya Wanawake Tanzania kuunganishwa na Benki ya *TPB*. Hivyo basi, huduma za iliyokuwa Benki ya Wanawake Tanzania zinaendelea kutolewa na Benki ya *TPB* ambapo Benki ya *TPB* imeanzisha dirisha maalum la akina mama katika matawi yake yote 76 yaliyopo nchini Tanzania, yakiwemo matawi ya Unguja na Pemba ili kukidhi mahitaji ya huduma za kibenki kwa akina mama kote nchini. Kwa muktadha huu, wanawake na wananchi wote wa Zanzibar wataendelea kuhudumiwa kupitia dirisha hilo maalum.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Faida.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kuunganisha Benki hii ya Wanawake pamoja na Benki ya Posta Tanzania. Kwa nini

naipongeza? Naipongeza kwa sababu Benki ya Wanawake Tanzania ilikuwa katika maeneo machache hususani Dar es Salaam na maeneo mengine, haikuwa katika mikoa yote, lakini Benki ya Posta iko kila eneo la Tanzania hii, naipongeza sana Serikali yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu lipo hapa, katika hiyo Benki ya Posta ya Tanzania kuna akaunti moja inaitwa Tabasamu kwa ajili ya wanawake. Nadhani watu wengi hawaiilewi, leo Mheshimiwa Naibu Waziri atueleweshe hapa. Je, hii akaunti ya Tabasamu imewasaidia kwa kiwango gani wanawake wa Tanzania katika kuwainua kiuchumi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la moja la nyongeza la Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Dada yangu Mheshimiwa Faida kwa kuwa yuko mstari wa mbele kufuatalilia maslahi mapana ya wanawake wa Tanzania. Niwapongeza sana wanawake wa Zanzibar kwa kutuletea kifaa hiki na kinafanya kazi sawasawa kwa ajili yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili kwa sababu hata swali lake aliloliuliza, kauliza *specific* ili wanawake waendelee kufahamishwa nini faida wanayopata baada ya Benki ya Wanawake Tanzania kuunganishwa na Benki ya *TPB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefungua akaunti ya Tabasamu ni sahihi kabisa, Dada yangu Mheshimiwa Faida na akaunti hii maalum imefunguliwa kwa ajili ya wanawake wa Tanzania pekee, waweze kuhudumiwa kama wanawake kama walivyokuwa wakihudumiwa na Benki yao ya Wanawake Tanzania. Kwa hiyo, huduma zote zile zinatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakinii nyongeza katika akaunti hii ya Tabasamu kama lilitivo jina lake, tunataka kipeleka Tabasamu kwa mwanamke wa Tanzania. Tunahitaji mwanamke wa Tanzania awezeshwe kupata mkopo wenye riba nafuu, awezeshwe yeye peke yake siyo lazima awe kwenye kikundi kama ambavyo mabenki mengine yanafanya, aweke akiba yake kidogo kidogo apate mkopo nafuu na aweze kufanya shughuli zake za ujasiriamali, afanye shughuli zake za kiuchumi na za kijamii kwa ajili ya maslahi yake yeye mwenyewe binafsi na maslahi mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe wito kwa wanawake wa Tanzania, tuitumie akaunti hii ya Tabasamu ndani ya Benki yetu ya Posta. Imeanza vizuri na sisi tuko tayari kuwahudumia wanawake wa Tanzania kwa sababu Serikali ya Chama cha Mapinduzi inawajali Watanzania na hasa wanawake. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Alfredina Apolinary Kahigi.

Na. 34

Hitaji la Kiwanda cha Kuchakata Ngozi

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI aliuliza:-

Katika Mkoa wa Kagera kuna Ranchi za Taifa zipatazo nne ambazo ni Kagoma, Mabare, Kitengula na Missenyi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kiwanda cha kuchakata ngozi katika Mkoa wa Kagera?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO - MHE. HUSSEIN M. BASHE
(K.n.y WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Alfredina Kahigi, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba uwepo wa Ranchi za Taifa Kagoma, Mabare, Kitengula na Missenyi pamoja na uwepo wa mifugo mingi katika Mkoa wa Kagera kunatoa fursa kubwa ya uwekezaji wa viwanda vyakuchakata mazao ya mifugo. Aidha, Kampuni ya Ranchi za Taifa (*NARCO*)imeandaa mpango mkakati wa kibashara wa miaka mitano kuanzia mwaka 2017 mpaka mwaka 2022 kwa lengo la kuendeleza na kueneza ufugaji bora hususan ufugaji wa ng'ombe bora wa nyama aina ya *boran* kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi kwa kutumia mbinu za kisasa. Mpango huu pia unalenga kusaidia *NARCO* kuingia ubia na kampuni ambazo zinaweza kujenga viwanda vyakuchakata mazao ya mifugo ikiwemo ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kuititia Chuo cha *DIT, campus* ya Mwanza, umeandaliiwa mpango kazi kwa kutoa mafunzo kwa vikundi vyavijana na akina mama hususan namna ya kusindika ngozi na uzalishaji wa bidhaa za ngozi, ambayo yakitumika ipasavyo yatasaidia kuongeza wigo wa kimasoko wa zao la ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia fursa za uwekezaji zilizopo kwenye Sekta ya Mifugo, katika Mkoa wa Kagera, Wizara inashirikiana na Wizara ya Viwanda pamoja na Kituo cha Uwekezaji (*TIC*), kuendelea kutangaza fursa hizo na kutafuta wawekezaji makini wenye nia ya kuwekeza kwenye viwanda vyakuchakata nyama, ngozi na mazao mengine ya mifugo ili kusaidia kutoa ajira kwa wananchi wa Kagera, kuongeza thamani ya mazao ya mifugo na kuongeza kipato cha wafugaji.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kahigi.

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nakupongeza kwa majibu yako mazuri na kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Kilimo. Mungu akutangulie. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali yangu mawili ya nyongeza, swali la kwanza; Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzuia wafugaji hao wasiweze kugonga ngozi mihuri ili wasikose soko la ngozi zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa wafugaji wanakamua maziwa mengi katika ranchi hizo na wafugaji wengine wa pemberi; Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwatafutia vifaa vyta kuweka maziwa yao? Maana vifaa wanavyovitumia siyo bora kwa kuweka maziwa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (k.n.y. WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kuweka alama na kuchoma chapa ng'ombe, ni kweli kwamba inapunguza ubora wa mazao ya ngozi. Kuwepo kwa fursa ya uwepo wa maziwa mengi kutoka kwa wafugaji, nayo ni fursa ambayo ni lazima Serikali ichukue hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mifugo imeunda Kikosi Kazi ambacho kinahusisha Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Mifugo na Wizara ya Fedha na kikosi kazi hiki kinaanza kuzunguka kuangalia uwezekano wa namna gani ya kuanzisha maeneo madogo madogo ya usindikaji wa mazao ya mifugo, hasa maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kuweka alama, Wizara iko katika mchakato wa kuangalia ni namna gani tunaweza kutumia *system ya tagging* kwenye masikio ili kuweza kuweka *numbering system* na kuwatofautisha wafugaji. Hii itaondoa tatizo la kuweka michoro katika ngozi na kuongeza thamani ya ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Mheshimiwa Hassan Elias Masala.

Na. 35

**Kuboresha Shule na Zahanati Zilizopo kwenye
Kambi za Jeshi**

MHE. HASSAN E. MASALA aliuliza:-

Kambi za Jeshi 41KJ, 452 *Medium* ni miongoni mwa kambi kongwe na zenyne mchango mkubwa katika Ulinzi wa Taifa letu. Kutokana na ukongwe huo, kambi hizo zimechakaa miundombinu yake mfano shule na zahanati zilizopo kwenye kambi hizo:-

- (a) Je, nini mpango wa Serikali juu ya kuboresha miundombinu ya Zahanati zilizopo kwenye kambi hizo?
- (b) Je, nini mpango wa Serikali wa kuboresha miundombinu ya shule hiyo iliyopo kwenye kambi hizo?
- (c) Je, nini mpango wa Serikali juu ya kuboresha miundombinu ya *Medium Workshop* hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y
WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Elias Masala, Mbunge wa Nachingwea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Jeshi 41KJ na 451KJ ni miongoni mwa kambi kongwe na zenyne mchango mkubwa katika ulizi wa Taifa letu. Kutokana na ukongwe wa kambi hizo, umepelekea kuchakaa kwa miundombinu ya zahanati, shule na *medium workshops* zilizopo huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshwaji wa miundombinu ya hospitali kuu ya kanda iliyopo chini ya kambi ya Jeshi la 41 KJ, umekamilika likiwemo jengo kuu la hospitali, wodi za wagonjwa, chumba cha kuhifadhi maiti pamoja na vitanda vya malazi na kujifungulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyopo ni upungufu wa wataalam pamoja na madawa, ambapo kwa hatua za awali Jeshi la Wananchi wa Tanzania tayari limeshawaandikisha madaktari 300 ambao wamepelekwa Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi Monduli na wanatarajiwu kutawanywa katika hospitali na vituo vya afya mbalimbali nchini, ikiwemo hospitali kuu ya kanda iliyopo 41KJ. Changamoto ya upungufu wa madawa itashughulikiwa kadri ya fedha zinatakavyopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, 451KJ, ina kituo kidogo cha afya ambacho hutoa huduma ya kwanza kwa Maafisa, Askari, pamoja na raia waliopo jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule inayozungumziwa hapa ni Shule ya Msingi ya Maji Maji iliyopo katika Kambi ya Jeshi 41KJ. Kwa nyakati tofauti Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu mbalimbali ya shule za msingi zikiwemo shule zilizopo katika maeneo ya Jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea kufanya mawasiliano na Wizara yenye dhamana ya kusimamia Shule za Msingi (TAMISEMI) ili ione uwezekano wa kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya Shule ya Msingi Maji Maji iliyopo katika Kambi ya Jeshi 41KJ Wilayani Nachingwea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za bajeti zimekuwa hazitosherezi katika kufufua karakara hiyo, hivyo Jeshi la Wananchi Tanzania limeweka mikakati ya kufufua miundombinu ya karakana ili iweze kuijiendesha kibashara kwa ajili ya kulihudumia Jeshi na Wananchi kwa ujumla. Aidha, mchakato wa kuipeleka karakana hiyo katika ngazi ya VETA unaendelea chini ya Makao Makuu ya Jeshi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masala.

MHE. HASSAN E. MASALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza ambalo nilikuwa naomba kujua, kwa sababu kituo hiki cha kanda ambacho kiko *41KJ* kinahudumia wananchi wanaotoka maeneo ya Kilimani Hewa, Nampemba, Mtepeche, Mkotokuyana pamoja na Mandai; pamoja na mkakati ambao Serikali imeusema, hebu aniambie ni mkakati gani ambao Wizara wanaweza wakaufanya kwa haraka ili kuhakikisha wataalam wanapatikana katika kituo hiki ili wananchi waendelee kupata huduma pamoja ukarabati ambao tayari umeshafanyika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili ambalo nilikuwa naomba kujua, ni suala hili la ukarabati wa kituo cha karakana ambacho kiko pale kikosi cha mizinga. Vijana wengi wa Nachingwea sasa hivi wanakosa sehemu ambako wanaweza kwenda kuendelea na masomo yao. Karakana hii kwa sasa inachukua idadi ndogo sana ya wanafunzi au wanachuo. Nini mkakati wa Wizara ili kuhakikisha jitihada hizi za kuihamisha hii karakara kuipeleka *VETA* unafanyika au kutoa fedha kwa ajili ya kununua vifaa na kuongeza wataalam ambao watakwenda kutoa huduma kwa vijana wa Wilaya ya Nachingwea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y.)
WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Masala kwa jitihada zake mbalimbali ambazo anachukua katika kuwasaidia

wananchi wa Jimboni kwake Nachingwea. Amekuwa akifanya hivyo hata kwa taasisi na vyombo vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, katika kujibu swali lake, kwanza kwenye eneo la wataalam kama ambavyo nimejibu katika swali langu la msingi, ni kwamba tayari hivi tunavyozungumza kuna madaktari takribani 300 ambaao wanaendelea na mafunzo katika chuo chetu cha Monduli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kwamba madaktari wale watakapokuwa wamekamilisha mafunzo yao, basi mionganoni mwao tutawapeleka katika hospitali ile iliyopo katika kikosi cha 41KJ, eneo la Nachingwea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la mkakati wa kuboresha Chuo cha *VETA*; ni kweli Chuko cha *VETA* hiki kinasaidia sana na kitaendelea kusaidia zaidi wananchi hususan kwa maeneo ya Nachingwea na maeneo mengine nchini kitakapokuwa kimeimariswa. Ndiyo maana dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba inakiimariswa chuo hiki ikiwa kimo katika mpango kazi wa Jeshi la Wananchi Tanzania. Mionganoni mwa mambo ambayo tunatarajia kufanya ni kuhakikisha kwamba chuo hiki kinaunganishwa na *VETA*.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tunavyozungumza, ni kwamba tunatoa huduma ile kwa kuazima Walimu kutoka *VETA* kuja kufundisha, lakini pale ambapo mikakati hii itakapokamiliaka, tutakuwa tuna Walimu wa kutosha ambaao watakuwa pale pale chuoni muda wote. Mbali ya hiyo, tutakuwa tunaweza kuongeza vifaa pamoja na kuimariswa majengo ya chuo hicho ili kiweze kutoa huduma kwa wananchi wengi zaidi wakiwemo wananchi wa Mheshimiwa wa Jimbo la Nachingwea kwa Mheshimiwa Hassan Masala.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Hussein.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la

nyongeza. Kwa kuwa Serikali imekuwa ikichukua vijana wengi kuwapeleka kwenye mafunzo ya JKT na baada ya mafunzo hayo, vijana wachache sana ambao wanapata ajira na vijana wengi wanakuwa wako mitaani. Kwa nini Serikali isije na mikakati ya hao vijana ambao wanamaliza mafunzo ya JKT kuwatafutia ajira mbalimbali kama vile kwenye migodi na maeneo mengine ili kuweza kupunguza vijana hao kuzurura mitaani na baadaye kuandaa bomu ambalo ni hatari? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y.)
WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza malengo ya kuwapeleka vijana JKT, haina maana kwamba vijana wote watakaopelekwa JKT wataajirisha na vikosi vyetu vya ulinzi na usalama, ni kwa sababu idadi ya nafasi za ajira zilizopo katika vyombo vyetu hivi ni chache kulinganisha na idadi ya vijana ambao wanaingia JKT. Hata hivyo, kwa kuwa mafunzo haya ya JKT yanaimarisha uzalendo na kujenga ujuzi mbalimbali, kwa hiyo, ni imani ya Serikali kwamba maandalizi ya vijana ambao wanakwenda JKT yatawasaidia kuweza kutumia fursa nyingine zilizopo nchini za kuweza kupata ajira ikiwemo katika taasisi binafsi, taasisi za Serikali, pamoja na kujajiri wenywewe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Saada.

MHE. SAADA MKUYA SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Pamoja na kazi nzuri ambazo zinafanywa na vikosi vyetu hivi vya Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kuna maeneo ambako kuna Kambi za Majeshi na kumekuwa kuna uwekezaji ambao unaendelea, hususan kumbi za *disco*, pamoja na mambo mengine ambayo yanafanana na hayo ambayo mara nyingine zinaleta athari za kiutamaduni na maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inasemaje kuhusiana na kambi hizo ambazo zinakuwa zinapigwa diskon kati

maeneo ya wananchi na hivyo kuathiri utamaduni pamoja na maadili ya maeneo yanayohusika? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y.)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya kumbi za starehe katika nchi yetu yapo kwa mujibu wa taratibu tulizojiwekea na siyo katika makambi ya Jeshi tu, ni maeneo mbalimbali. Hata kumbi ambazo zipo katika maeneo ya Kambi za Jeshi kwa ajili ya starehe zinatakiwa zifuate utaratibu ule ule ambao tumejiwekea wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sidhani kama ni sahihi kuonyesha kidole katika maeneo ya kambi ya Jeshi peke yake, imani yangu ni kwamba ukizingatia maadili na misingi ya Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania, nadhani itakuwa ni sehemu ya mwisho kuonyeshwa kidole katika ukiukwaji wa sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kama ana kesi mahususi ambayo anadhani inahitaji kufuatiliwa, namwomba Mheshimiwa Saada Mkuya atupatie taarifa ya eneo la kambi ambalo anazungumza ili tufuatilie na kuona hatua za kuchukua.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Mkundi.

Na. 36

Aina ya Mazao Yanayofaa Kulimwa Ukerewe

MHE. JOSEPH M. MKUNDI aliuliza:-

Kutokana na ufinyu wa ardhi na ongezeko la watu kwenye visiwa vya Ukerewe, pamoja na ardhi kutokuwa na rutuba, kumesababisha Kilimo kisicho na tija:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kufanya utafiti wa kisayansi ili kuwashauri wananchi wa Ukerewe aina ya mazao yanayopaswa kulimwa na jinsi ya kutumia eneo dogo la ardhi kwa ufanisi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN MOHAMED BASHE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (*TARI*) ni kufanya utafiti wa tabaka na afya ya udongo katika kanda zote saba za kilikolojia za kilimo nchini, ikiwemo kanda ya Mwanza. Utafiti huo wa kisayansi unalenga kubaini aina za virutubisho na tabia za udongo katika maeneo mbalimbali pamoja na kubaini mimea na mazao yanayostawi kwenye udongo husika ili kuweza kutoa elimu kwa wakulima kuhusu kiasi, aina na matumizi sahihi ya mbolea za viwandani na asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Ukerewe ambayo wananchi wengi hulima mihogo, mpunga, mtama, mahindi, viazi vitamu na machungwa, utafiti wa awali unaonyesha kwamba, udongo wake una mboji kiasi kidogo cha asilimia 1.3 ukilinganisha na kiwango cha asilimia 2.5 ambacho ndicho kiwango cha mboji katika udongo wenye rutuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile utafiti umeonyesha kwamba kiwango cha tindikali kwa maana ya *pH* ni 5.4 ukilinganisha na *pH* ya 6.6, kiwango ambacho kinafaa kwa mimea ya kufyonza virutubisho kutoka kwenye udongo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa kiasi hicho cha tindikali katika maeneo hayo kunaashiria kwamba kuna

upungufu wa virutibisho vya *nitrogen, phosphorus, potassium, sulphur, calcium* na *magnesium*. Aidha, kulingana na matokeo hayo, inashauriwa kutumia mbolea zenye virutubisho vya *nitrogen, potassium, phosphorus, sulphur, calcium* na *magnesium*, ambazo ni pamoja na Minjingu, mazao ya *ramila, samadi* na *CAN, UREA* na *DAP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sampuli za udogo zimechukuliwa katika kanda na mkoa mbalimbali nchini ukiwemo Mkoa wa Mwanza unaojumuisha Wilaya ya Ukerewe kwa lengo la kubaini viwango vya virutubisho vilivyopo katika sampuli hizo ambapo kwa sasa tathmini ya kina inaendelea kufanyika katika maabara ya *TARI, Selian*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kukamilika kwa tathmini hiyo kutasaidia kushauri wakulima kuweka viwango vya mbolea vinavyohitajika kulingana na virutubisho stahiki kwa mazao husika na aina ya mazao na yanayopaswa kulimwa katika maeneo husika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mkundi.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake, lakini napongeza vile vile hatua zilizofikiwa za kufanya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; pamoja na kwamba utafiti bado unaendelea, lakini tatizo la msingi tayari limepatikana kwamba kuna kiwango kidogo cha mboji, lakini pHvilevile ya udongo wa Ukerewe iko chini. Sasa swali langi, Wizara iko tayari kuijumuisha Ukerewe katika maeneo yanayopata ruzuku za pembejeo itakayoambatana na ushauri wa aina ya mazao yanayopaswa kulimwa kwenye maeneo yetu ya Ukerewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Ukerewe tuna fursa kubwa sana ya matunda, lakini tatizo kubwa, matunda yetu yamekuwa yanaharibika kwa kukosa soko. Tumejitahidi

kupata wawekezaji kwa ajili ya kujenga viwanda, lakini tumekuwa tunakwama ama kutokana na kiwango cha malighafi inayozalishwa au aina ya matunda tunayoyazalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iko tayari kuwasaidia wananchi wa Ukerewe ambao wanalima matunda ili aina ya matunda yanayotakiwa iweze kulimwa, lakini sambamba na hilo, kusaidia kuwepo kwa kiwanda cha kusindika matunda haya? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN MOHAMED BASHE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mkundi kwa kazi kubwa anayofanya Jimboni kwake. Kuhusu suala la kupewa ruzuku kama ni *special case*, suala la ruzuku kwenye mbolea, hatuwezi kutoa *commitment* kama Serikali kwamba tutawapa watu wa Wilaya ya Ukerewe peke yao. Suala la ruzuku ama mabadiliko ya sera juu ya suala la kutoa ruzuku katika Sekta ya Kilimo, litatazamwa kwa ujumla wake kwa kuwa sasa hivi Wizara inapitia upya Sera yetu ya Kilimo ya Mwaka 2013 ili kuona mahitaji na namna gani tunaweza kutatua changamoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hatua za awali, tunaendelea kusisitiza wananchi wa Wilaya ya Ukerewe, watumie mbolea za minjingu na mbolea nyingine ambazo zinaweza kuongeza uzalishaji katika eneo lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la matunda, siyo suala la Ukerewe peke yake, mazao yote ya *horticulture* sasa hivi kama Wizara tunafanya *baseline study* ya kuangalia ni namna gani tunaweza kufanya *zoning* ya kila eneo ili tuweze kutambua ni mazao gani ya *high value* yatokanayo na *horticulture* yanaweza kuzalishwa. Wizara sasa hivi iko katika hatua za awali kuangalia ni namna gani sekta ya

horticulture inaweza kupewa kipaumbele na namna gani mazao ya matunda na mboga mboga yanaweza kupewa kipaumbele kama zao la muhimu kwa ajili ya *export* katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuwaombe Waheshimiwa Wabunge watupe muda, kabla ya mwaka wa fedha ujao tuta-*unveil* Sera ya Wizara ambayo itafanya *diversification* katika sekta nzima ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Paresto, halafu Mheshimiwa Boni.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuulizwa swali dogo la nyongeza. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri amekiri hapa kwamba mnafanya mapitio ya Sera ya Mbolea kwa ujumla, lakini kumekuwa na changamoto ya usambazaji wa mbolea na kutokufika kwa wakati kwenye maeneo husika na uhitaji wa uhalisia wa eneo husika.

Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha usambazaji unafanyika kwa wakati na kwa mahitaji ya maeneo husika ili basi hizi ardhi zetu ambazo zimekosa rutuba ziweze kupata rutuba?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba kuna upungufu katika baadhi ya maeneo katika suala la uasmbazaji wa mbolea na Wizara sasa hivi inachukua hatua ya kufanya *reform* katika Taasisi yetu ya *TFC* ili tuweze kuondokana na hili tatizo pale ambapo tunafanya *bulk procurement* kuititia *TFC* ili matatizo ya namna hiyo yasiweze kujirudia. Lakini yapo maeneo ambayo kuna wazalishaji wa ndani kama Minjingu ambao tumeamua kama Serikali kuwapa *priority* ili maeneo ya karibu ambayo kiwanda hichi kinafanya kazi na mbolea yake

inaweza kutumika iweze kutumika kwa haraka, lakini sisi kama Wizara tunapitia mfumo mzima wa usambazaji wa pembejeo za mazao ili kuondoa mambo makubwa mawili:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ucheleweshaji, mbili wizi unaoendelea katika usambazaji wa pembejeo ambao siku ya mwisho anaenda kubeba mkulima. Kwa hiyo, tunaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba mchakato huu unaendelea na tunaaamini kwamba msimu huu wa kilimo mambo mengi yatabadilika katika usambazaji wa pembejeo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Boniphace Mwita jiandae Mheshimiwa Mwalongo.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuuliza swali dogo la nyongeza;

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimu wa mwaka jana wa Pamba 2018/2019 tuliwaambia wakulima wa Pamba tuchange shilingi 100 kwa kila mkulima, iwe umekopa au hukukopa kwa maelezo kwamba msimu 2019/2020 hatukatwa pembejeo. Naomba kupata maelezo ya Serikali mwaka huu pembejeo wakulima wanakatwa au hawakatwi? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE): Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwamba wakulima wanakatwa ama hawakatwi ni kwamba wakulima wanakatwa pembejeo za pamba msimu huu. Kilichotokea msimu uliopita fedha walizokatwa zililipa madeni ya pembejeo ambayo wakulima walipewa msimu uliotangulia, kwa hiyo msimu huu wakulima wa Pamba watakatwa pembejeo ambazo wamehudumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongezeee hapa na niseme na hili jambo liwe wazi, mfumo wa usambazaji pembejeo

katika msimu ujao wa Pamba utabadilika. Tathmini ya awali iliyonekana ni kwamba wakulima wa Pamba mwaka huu wanalipia pembejeo ambazo *either* hawakuzitumia ama wanabebeshwa mzigo, Wizara sasa hizi *task force* yetu iko kuititia mchakato mzima na tutachukua hatua kwa watu wote waliowaibia wakulima wa Pamba mwaka huu. Msimu ujao tunachokifanya mkulima wa Pamba Tanzania *Cotton Board* itatoa fomu ambayo itakuwa na *duplicate* ya fomu tatu, fomu moja ataachiwa mkulima aliyechukua pembejeo na itaonesha bei na thamani halisi, fomu nyingine itabaki kwenye *AMCOS*, fomu nyingine itabaki kwenye Ushirika ili msimu unapokuja wakati wa kuuza pamba gharama zake ziweze kuthibitishwa kabisa halali, kwa sababu sasa hivi kuna maeneo *AMCOS*na Ushirika unawaibia wakulima wa pamba ambao hawakuweza kubebeshwa gharama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni kwamba wataendelea kulipa na tutabadilisha mfumo wa utoaji. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mwalongo, jiandae Mheshimiwa Zubeda, Mheshimiwa Nsanzugwanko.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa la wakulima wa Njombe ni udongo kuwa na tindikali nyingi zaidi na wataalaam wanajua hilo. Je, Serikali inatusaidiaje wakulima wa Njombe Mjini kutuletea chokaa ya kilimo ili kupunguza tindikali kwenye udongo? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri nakupa maswali mengi naona uzoefu wako ni mzuri, kwa hiyo majibu mazuri yanapatikana, ahsante. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE): Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Wizara inafanya *mobile sampling* kwa nchi nzima kuangalia udongo na kuweza kuja na *study* ya wazi kujua kwamba wapi kuna tatizo gani na

tuweze kupata *solution*. Tumuombe Waheshimiwa Wabunge watuvumilie wakati tunamaliza *study* hii tunaamini kufika mwisho wa siku huu tutakuwa na *sample* ya nchini nzima na kujua eneo gani linafaa kulima nini na eneo gani linahitaji mbolea gani ili tuweze kuwapitia huduma sahihi wakulima wetu badala ya kulima kwa kubahatisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Anatropia.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya wakulima wa Kahawa Mkoani Kagera na hasa Wilaya ya Kyerwa kujitolea na kulima Kahawa wameendelea kupata bei ndogo ya mazao yao ikiwa kilo ni shilibngi 1,100 kinyume na kauli ya Mheshimiwa Rais.

Je, ni lini wananchi wa Kyerwa wataanza kulipwa shilingi 1,500 kama alivyoagiza Mheshimiwa Rais kwa kilo moja ya Kahawa?

MWENYEKITI: Hilo halipo katika swali la msingi kaa chini, Mheshimiwa Nsanzugwanko. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nianze kwa kumpongeza Naibu Waziri huyu kwa kuteuliwa. Nina swali dogo la nyongeza:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma haujafanyiwa *soil profiling* na Mkoa wa Kigoma una Chuo chake cha Kilimo cha Mbondo ni kwa nini sasa Serikali na hii tumeshaiomba huko nyuma, kwa nini sasa Chuo cha Mbondo kilichopo Kasulu kisifanywe ni Chuo Dada cha *TARI* kwa ajili ya *profiling* ya udongo katika Mkoa wa Kigoma, Mkoa ambaa unapata mvua nyingi kuliko Mikoa mingine yote katika nchi yetu? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE):

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niseme kitu kimoja tumetenga mwaka huu Shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kuwekeza katika Chuo hicho kilichoko Kigoma, na specifically Kigoma itakuwa ni moja ya eneo la kimkakati la Wizara ya Kilimo kwa sababu ya *Palm* na tuna mpango wa *UNIDO* na *FAO* ambao tutawekeza fedha nyingi kwa ajili ya uzalishaji wa *Palm Oil* ili iwe ni *solution* ya kuondokana na kuagiza mafuta katika nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ombi ulilosema kwamba iwe ni Chuo sehemu ya *TARI* itakuwa chini ya *TARI* na itapewa hadhi kama vyuo vingine *center* za utafiti ambazo ziko chini ya *TARI*. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. Tunaendelea Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe.

Na. 37

**Fidia kwa Wananchi Waliopitiwa na Barabara
ya *By Pass* - Babati**

MHE. ESTER A. MAHAWE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawalipa fidia wananchi wa Sinai, Hangoni, Kwere na Mruki waliopitiwa na barabara ya "By Pass" ya magari makubwa yatokayo Dodoma na kutokea stendi mpya ya Babati Mjini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI UJENZI (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)
aliibuu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa barabara ya mchepuo Babati *Bypass* katika barabara ya Dodoma Babati, Arusha na Singida Babati unatekelezwa kwa pamoja na mradi wa Mtera *Bypass* katika barabara ya Iringa Dodoma chini ya ufadili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika na uko katika hatua ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na maandalizi ya makablasha ya zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya majukumu ya Mhandisi Mshauri ni kutambua sehemu ambamo barabara ya mchepuo itapita yaani *alignment*. Mara baada ya maeneo itakamopita barabara ya mchepuo kujulikana na kukubaliwa na Serikali kazi itakayofuata ni ya usanifu wa kina ambapo mali zitakazokuwa katika maeneo inamopita barabara ya mchepuo zitatambuliwa na kufanyiwa tathimini kwa ajili ya fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua iliyofikiwa sasa ni kwamba kazi ya upembuzi yakinifu inaendelea lakini bado maeneo na mali zitakazoathiriwa na mradi itakamopita barabara hayajulikana, hivyo mali na kutathiminiwa na kufidiwa hazijajulikana Serikali italipa fidia kwa mujibu wa sheria.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mahawe.

MHE. ESTER A. MAHAWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake lakini nimfahamishe tu kwamba miaka mitatu iliyopita wananchi wa maeneo ya Mruki, Hangoni, Sinai pamoja na Kwere walizuiwa na Halmashauri kuendelea kuendeleza maeneo yao yaliyohisiwa kwamba ndiko barabara itakapopita wakiwa wamefanyiwa tathimini nakuhadiwa fidia. Je, kwa kauli ya Serikali sasa wananchi hawa wanaruhusiwa kuendelea na majukumu yao ya kuendeleza maeneo yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kwa kuwa majibu ya Serikali pia hayajatoa *time frame* yaaani lini sasa upembuzi huo wa kina utakamilika. Je, Serikali iko tayari kusema ni lini upembuzi utaanza na kukamilika ahsante? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI UJENZI (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze tu Mheshimiwa Mbunge Mahawe kwa sababu amekuwa akifuatilia sana juu ya maendeleo ya Babati na Manyara kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba Halmashauri kuwazuia wananchi au kuwaelekeza wananchi kwa vyovytote vile haikuwa sahihi sana kwa sababu ilitakiwa Mamlaka inayohusika na ujenzi wa barabara ifanye hivyo. Kwa hiyo, niwaombe mahali popote kutakapokuwa na miradi ya barabara tusubiri kupata kauli ya Mamlaka halisi ili tusiweze kuwachanganya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya usanifu inaendelea sasa hivi kuanzia tarehe 01 Julai, 2019 kazi hiyo imeanza na wakati wowote tutapata *inspection report*, kwa maana ya *reportya* awali itakapokuwa imepatikana tutaweza kufanya sasa maamuzi, kwa sababu tutakuja na *alternative* kama tatu, halafu Serikali iamue tuende hatua ya mwisho sasa ya kukamilisha michoro pamoja na kuona kwamba tunapata gharama halisi za kuwafidia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo uvute subira kazi inaendelea na ninalishukuru sana Bunge lako limetupitishia fedha kwa ajili ya kazi hii ya usanifu wa hii barabara na kwamba kazi itaisha haraka sana, katika mwaka huu wa fedha kwa sababu fedha tunazo na kazi inaendelea itakamilika, gharama zitajulikana na wananchi tutawajulisha wale watakaopitiwa na mradi na Mheshimiwa Mbunge kwa sababu tuko pamoja hapa taarifa hizi za kuhusu wananchi ni wepi watapitiwa na mradi ili tuweze kuwalipa fidia tutaweza kuwasiliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Gashaza.

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kazi kubwa inayofanya na Serikali katika kuboresha miundombinu ya barabara, lakini kipo kipande cha barabara kutoka eneo la Rusaunga kuelekea Rusumo mpakani barabara inayoelekeea Rwanda kimeharibika kuna mashimo utafikiri ni mahandaki, hii inapelekea magari kuharibika na kusababisha ajali zisizo za lazima. Magari sasa yanacheputa kupitia barabara ya Rusaunga, Rurenge, Mrugarama ambayo ni ya vumbi na hivyo kuendelea kusababisha uharibifu kwenye barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini *commitment* ya Serikali katika kuhakikisha kwamba barabara hii inatengenezwa kwa kiwango kinachostahili ukizingatia kwamba ni barabara ya kluchumi? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI UJENZI (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara hii kutoka Rusaunga kwenda Rusumo kilomita 92 ni barabara ambayo imechoka imechakaa ina mashimo, ina mahandaki na imekuwepo kwa miaka mingi sana ni zaidi ya miaka 34 na Serikali imekuwa ikifanya juhudhi ya kuiboresha barabara hii kwa sababu imejengwa muda mrefu kutoka Isaka kwenda Rusumo, kwa sehemu kubwa ya barabara hii matengenezo yamekuwa yakifanyika tumebakiza hizo kilomita 92.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote katika Mkoa huu wa Kagera kwamba tumetenga fedha kwenye Bunge hili la kuifanyia matengenezo upya barabara hii, lakini kwa hatua za awali kuboresha haya mahandaki ambayo Mheshimiwa Mbunge anayaaita kuna fedha tayari Serikali imeshatoa na tulikuwa tunakamilisha hatua za manunuzi, mkandarasi ameshapatikana tutaanza kwanza kuboresha ili kuyapunguza haya mashimo Mheshimiwa Mbunge, tutayapunguza wakati harakati zile za kuanza mradi

mkubwa wa kuboresha barabara hii haya mashimo tutakuwa tumeyaondoa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante tumeshakuelewa, Mheshimiwa Mbarouk.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu baada ya kupiga kelele hatimae kuna kila dalili za kujengwa barabara ya Pangani. Nataka kujua sasa je, wale wananchi amba walielezwa kwamba wasiendeleze mashamba na majengo waliyoko pembezoni mwa barabara, ni lini wataanza kulipwa fidia zao? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wka kifupi.

NAIBU WAZIRI UJENZI (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejipanga vizuri kujenga barabara hii ya Tanga - Pangani kama Mheshimiwa Mbunge ulivyosema, lakini ni utaratibu wa Serikali ni kulipa fidia kwanza kabla ya ujenzi kuanza, kwa vile Mkandarasi ameshapatikana niwahakikishie tu wakazi wa maeneo haya amba mradi utapita watalipwa fidia yao mara moja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sitta, Mheshimiwa Kisangi.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali kwa kutupa barabara nzuri ya kutoka Ndono mpaka Urambo na inakatisha mpaka katikati ya Mji, naishukuru sana Serikali kwa niaba ya wananchi wa Urambo. Swali ni kwamba ni lini Mheshimiwa Waziri atakuja kuangalia *round about* ambayo wameiweka pale inasababisha ajali kwa jinsi ambavyo kona iliyopo ni kali sana, magari yanapata ajali, watu wanapata ajali. Kwa heshima na taadhima naomba kujua ni lini Serikali itakuja kutusaidia *round about* ya Urambo. Ahsante sana?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa kifupi ni lini utakwenda.

NAIBU WAZIRI UJENZI (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisha kwenda Urambo lakini nitakwenda tena kwa sababu nafikiri kuliwa na zoezi hili la kuangalia sehemu bora zaidi ya kufanya marekebisho kuweka *round about* katika Mji ule. Kwa hiyo, Mama yangu nikuhakikishe kwamba tutakwenda lakini wataalam wanaendelea kukamilisha ili kuona ni wapi patafaa vizuri ili tuweze kuweka huo mzunguko. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kisangi, Mheshimiwa Magige jiandae Mheshimiwa Kabati.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza. Swali la kwanza napenda nipongeze Serikali kwa kusikia kilio chetu Wabunge na kilio cha wananchi sasa wameanza kufanya tathmini ya barabara ya Kirwa *Road* kutoka eneo la Mbagala Kokoto kwenda Kongowe, eneo ambalo lilikuwa na msongamano mkubwa wa magari naiopongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kusikia kilio chetu Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi wa eneo la Mbagala Kokoto mpaka Kongowe wameanza sasa kufanyiwa tathmini ya maeneo yao na kuwekewa alama ya X. Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba wananchi hawa watalipwa kwa wakati ili kupisha zoezi hilo la upanuzi wa barabara ya Kirwa *Road*. Ahsante sana? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu. Jiandae Mheshimiwa Catherine Magige, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Rhoda Kunchela na Mheshimiwa Bonnah Kaluwa.

NAIBU WAZIRI UJENZI (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mbunge najua tumezungumza miradi mingi sana na anafahamu

juhudu ambazo zinafanyika ndio maana anatoa pungezi, kwa niaba ya Serikali nazipokea pungezi hizo.

Mhehimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumejipanga kuboresha barabara hii ili kuweza kupunguza pia msongamano ambao unajitokeza na usumbufu ambao unajitokeza, nami eneo hili nimelitembelea. Vile vile niwahakikishie tu wananchi hawa kwamba tumejipanga vizuri kwa sababu hata kwenye bajeti tuna fedha kwa ajili ya kuendeleza maendeleo ya maeneo haya na kulipa fidia, tutawalipa mara moja wakati tukiendelea kuboresha mradi huu. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Magige.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuwa barabara ya Karatu - Mang'ola katika Mkoa wa Arusha imekuwa ikitengenezwa mara kwa mara na kuisababishia Serikali gharama kubwa. Je, ni lini Serikali itajenga barabara hii kwa kiwango cha lami kwa sababu eneo la Mang'ola ndilo linalotegemewa kwa uchumi wa Karatu kwa sababu lina ulimaji Mkubwa wa zao la vitunguu? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi. Jiandae Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Rhoda Kunchela na Mheshimiwa Bonnah Kaluwa.

NAIBU WAZIRI UJENZI (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejipanga vizuri kuijenga barabara hii. Barabara hii ni muhimu inaunganisha Mkoa wa Arusha pamoja na Mikoa mingine Ukanda wa Ziwa, kwa hiyo, tuko katika hatua za mwisho kwa sababu kazi ya kufanya usanifu katika barabara hii ilishafanyika tunafanya *reviewna* mara tu tutakopopata fedha barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Rhoda Kunchela na Mheshimiwa Bonnah Kaluwa na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swalii dogo la nyongeza. Kwa kuwa changamoto iliyopo katika *Bypass* ya Babati inafanana kabisa na katika Jimbo letu la Iringa Mjini ambako Serikali imeshabooma makazi ya watu lakini ujenzi haujaanza. Je, Serikali itaanza lini ujenzi huo ili kupunguza adha kubwa kabisa wanayopata wananchi kwenda katika stendi mpya ya Igumbilo? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI UJENZI (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejjipanga kujenga barabara hiyo ni kilomita Saba na katika bajeti ya mwaka huu tumetenga fedha kuanza ujenzi wa barabara hiyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ritta Kabati ninakupongeza tu unafuatilia sana barabara hili lakini nikuhakikishie pia kwamba tumejjipanga vizuri tunajua usumbufu wananchi wa Iringa Mjini wanaopata wa magari makubwa yanayopita katika ya Mji, kwa hiyo ujenzi wa barabara hii utaanza tu mara moja kwa sababu tumeshajipanga vizuri na tutaendelea kutoa *feedback*. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante ujenzi unaanza, Mheshimiwa Rhoda jiandae Mheshimiwa Bonah, Mheshimiwa Mwingulu.

MHE. RHODA E. KUMCHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante pamoja na changamoto za kulipa fidia wananchi katika Taifa hili lakini Mkoa wa Katavi katika barabara ya kutoka Sumbawanga kuelekea Kigoma wakazi wa Kata ya Mpanda hoteli Misukumilo pamoja na llembu pamoja na Milala walirukwa katika masuala ya fidia mpaka sasa ni mwaka wa nne hawajalipwa pesa hizo. Je, ni kwanini Serikali mnawazungusha kuwalipa watu hawa amba walitumia gharama kubwa kujenga nyumba zao?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri fidia.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa

Mwenyekiti, niseme tu kwa ujumla hii Serikali hii inawajali sana wananchi wake na hakuna sababu ya kutokumlipa mwananchi haki yake. Kwa hiyo, naomba tu nilichukuwe hili kama ni suala mahususi ili nilifuatilie nione nini kilitokea kwa sababu ni nia ya Serikali kuwahudumia vema wananchi na kuwalipa haki zao kwa hiyo, tutalifuatilia suala hili.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Bonnah, ajiandae Mheshimiwa Mwigulu wa mwisho.

MHE. BONAH KAMOLI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Mheshimiwa Waziri Serikali ina mpango gani kuhusiana na Barabara ya Kimanga, kwa sababu *last time* Naibu Waziri alienda kufanya ziara lakini ile barabara mpaka sasa hivi imeachwa kutengenezwa. Pia nauiliza kuhusiana na daraja la Segerea Seminari ambalo limechukuliwa na maji tangu mwaka 2012 lakini pia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais mpaka leo halijatengenezwa ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu anapigania sana barabara za eneo la jimbo lake. Lakini niseme tu ile barabara ya Kimanga kulikuwa na mradi unaendelea nitafuata tu ufuatilaji nione nini kimetokea kama ule mradi unasua sua na tutawasiliana na Mheshimiwa Mbunge tukatembelee mradi tuone changamoto iliyokuwepo ili tuweze kuitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu lile daraja la upande ule wa Seminari, nilitembelea eneo hili tunahitaji kuweka daraja kubwa pale, Serikali bado inajipanga kutafuta fedha za kutosha hili tuweze kuboresha katika eneo hili. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge naomba uvute Subira tutajipanga vizuri tutaporesha eneo hili kwa sababu linahitaji fedha nyingi ili kuweza kuboresha mahali hapa ambapo ni sehemu korofii ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwigulu.

MHE. MWIGULU L. NCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa barabara ya Singida, Sepuka, Ndago, Kizaga kwa kiwango cha lami ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na ipo kwenye ilani ya uchaguzi ukurasa wa 56. Kwa kuwa upembuzi yakinifu katika barabara hii ulishafanyika na Mheshimiwa Naibu Waziri alishafanya ziara kukagua masuala yote katika barabara hiyo ni lini sasa ujenzi kwa kiwango cha lami utaanza katika barabara hiyo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Mbunge nakupongeza sana kwa sababu nimefuatilia kweli barabara hii muhimu na niseme tu ni mwaka wa fedha uliopita ndiyo tulikuwa tunaendelea kufanya kazi ya usanifu wa kina kwa ajili ya Ujenzi wa lami wa barabara hii. Mheshimiwa Mbunge vuta subira kwa sababu tunakwenda kwa hatua baada ya kukamilisha hili zoezi ambalo tulikuwa tunalifanya sasa tunatafuta fedha ili tuweze kuijenga kwa kiwango cha lami barabara hii muhimu.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa tunaendelea, Wizara hiyo hiyo swali la Mheshimiwa David Mathayo David kwa niaba yake Mheshimiwa Anne Malecela.

Na. 38

Hitaji la Mawasiliano ya simu – Same Magharibi

MHE. ANNE K. MALECELA (K.n.y. MHE. DAVID M. DAVID)
aliuliza:-

Je, ni lini Serikali kwa kushirikiana na Mashirika ya Simu itawapelekea huduma ya simu wananchi wa Kata za Msindo Mshewa, Mhezi, Vumari, Vudee, Tae, Suji, Gavao, Saweni na Ruvu Jiungeni?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuptitia Mfuko wa Mawasiliano Kwa wote imetoa ruzuku kwa ajili ya ujenzi wa minara ya mawasiliano katika Wilaya ya Same ambapo wakazi zaidi ya 13,531 wamefikiwa na huduma za mawasiliano katika Kata za Bombo, Maore, Mshewa, na Ruvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuptitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kuflikisha huduma za mawasiliano nchi nzima. Kwa upande wa Same Magharibi, Serikali ilivianisha Vijiji vya Kata za Vumari, Suji na Ruvu Jiungeni ili kuangalia mahitaji halisi ya mawasiliano na hatimaye vimeingizwa katika orodha ya vijiji vya zabuni ya Awamu ya Nne. Zabuni hiyo ilitangazwa tarehe 18 Julai, 2019 ambapo mwisho wa kurudisha vitabu vya zabuni hiyo ni tarehe 3 Oktoba, 2019, ikifuatiwa na tathmini ya zabuni husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Mshewa imefikishiwa huduma za mawasiliano ambapo minara miwili (2) ya tigo imejengwa na kuihudumia kata hii. Pamoja na jitihada hizi na uwepo wa minara hii baadhi ya maeneo ya kata hii yanaonekana kuwa na changamoto za mawasiliano. Kata hii itafanyiwa tathmini zaidi ili kubaini maeneo mahususi ambayo bado yana changamoto ya mawasiliano ili yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuptitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF) imevipokea vijiji vya kata za Msindo, Mhezi, Vudee Tae, Gavao na Saweni na itavifanya tathmini kuangalia mahitaji halisi ya mawasiliano na kasha kuviiingiza katika orodha ya vijiji vya zabuni zitatazotekelawa

kulingana na upatikanaji wa fedha hususani katika mwaka wa fedha 2019/2020.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Malecela.

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Mwenyekiti, kata hizi alizotitaja Mheshimiwa Dkt. David Mathayo ni Kata ambazo ziko kwenye milima mirefu. Naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba alikuja Same Mheshimiwa Dkt. Mathayo akaingia kwenye gari yake na mimi nikaingia kwenye gari yake tukazzungukia kata hizi zote ambazo zimetajwa hapa na Kata ya Vuje, kata ya Bombo, Kata ya Mtina kata ya Lugulu.

Mheshimiwa Waziri uliona hali halisi ya kata hizi kwamba ni korofi mno hazina mawasiliano ya uhakika pamoja na mawasiliano ya Barabara, Mheshimiwa Waziri unakuja na mikakati gani sasa ya kuhakikisha hizi kata ambazo ziko milimani zinaondoka na matatizo haya ahsante Mheshimiwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza uniruhusu tu nitoe shukrani kwamba nilivyofanya ziara katika maeneo haya nilipata ushirikiano wa hali ya juu sana kwa Mheshimiwa Mbunge lakini pia kwa viongozi wa wilaya, kwa hiyo nakupongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na niseme tu yapo maeneo mbalimbali ambayo yanakuwa na changamoto kutokana na hali ya geografia, eneo la Same hili linamilima lakini yapo maeneo mengine ambayo yana misitu ambayo hii ni vikwazo kwa mawasiliano kwa hiyo utaona changamoto ya mawasiliano imekuwa kubwa katika eneo hili kwa sababu ya hali ya geografia kwa maana hiyo milima na misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumejipanga kama Serikali ndiyo maana utaona katika awamu ya nne

tuko kwenye hatua ya manunuzi, tutaendelea kuweka hiyo minara ambayo imetajwa na katika eneo hili tutakuwa na kata tano vijiji kumi na tatu na baada kusimika hiyo minara tutafanya tadhimini kuona maeneo yapi kutokana na geografia ambayo yatakuwa hayajapata tena mawasiliano kwahiylo hizi changamoto tunaendelea kuziondoa tunavyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge mkakati mkumbwa uliokuwepo ni kuhakikisha kwamba tunaweka maeneo haya katika mipango yetu kupitia mfuko wa mawasiliano kwa wote. Lakini pia tunaweka bajeti ya kutosha tunavyokwenda ili sasa tuhakikishe kwamba baadaye tunamaliza changamoto ya mawasiliano katika eneo hili lakini unafahamu pia tunaendelea kufanya usanifu mkubwa katika barabara kutoka Same kwenda Mkomazi lakini tutakwenda mkinga kule tumejipanga ili tuondolee shida wananchi wa maeneo haya ambayo hali ya geografia inawaathiri sana kwa maana ya usafiri wa barabara hali ni mbaya lakini pia upande wa mawasiliano ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Gekul, Mheshimiwa Haonga.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza, Mheshimiwa Waziri nimekuwa nikiuliza mara nyingi katika Bunge hili vijiji vya Imbilili, Imiti na Chemchem kwamba havina mawasiliano na nimekuwa nikipatiwa majibu ya Serikali kwamba dawa ya tatizo hili ni kuongezea nguvu minara ya Voda na Airtel, lakini kazi hii haifanyiki naomba nifahamu ni lini sasa kazi hii itafanyika ili wananchi wa maeneo hayo waweze kupata mawasiliano.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mbunge kwa sababu

tumeongea mara nyingi sana kuhusu changamoto za jimbo lake Mheshimiwa Mbunge na sisi tumejipanga. Kama nilivyozungumza juzi kwamba katika mradi huu wa Awamu ya IV ya kupunguza changamoto ya mawasiliano tunazo kata mia tano 21 na vijiji 1222 ambayo viko kwenye mpango. Nimuombe tu Mheshimiwa Gekul kwa sababu kile kijitabu ninacho hapo baadaye tuwasiliane ili tupitie kwa pamoja uweze kuona namna tulivyojipanga kutatua changamoto za mawasiliano katika eneo la kwako na tutaendelea kufanya hivyo mpaka wananchi waweze kuwasiliana vizuri katika maeneo yao ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Haonga, ajiandae Mheshimiwa Asha Mshua na Mheshimiwa Aysharose.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana mwaka 2016 Serikali illtuambia sisi Wabunge tuweze kuorodhesha maeneo yote ambayo hayana mawasiliano Wabunge tulifanya hivyo na tena mwaka huu Serikali ikatuambia tuweze kufanya hivyo tena, na mimi baadhi ya maeneo yangu kwa mfano kata ya Halungu, Kata Nambizo, Bara Magamba, Itaka na maeneo mengine hayana mawasiliano ya simu. Je, ni lini Serikali sasa itapeleka mawasiliano ya simu katika maeneo hayo ambayo ni muhimu sana kwa wananchi wa Jimbo la Mbozi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kama nilivyozungumza, tumekuwa tukiwasiliana na Waheshimiwa Wabunge vizuri ili kutatua tatizo la changamoto ya mawasiliano katika maeneo mbalimbali. Na kuititia huu utaratibu ambao tunaufanya kupata maoni na ushauri wa Wabunge ndiyo maana katika Awamu ya IV tumekuja na orodha kubwa sana ambayo tunaendelea kutatua matatizo yaliyokuwa maeneo yetu, vijiji 1222, ni vijiji vingi sana lakini kuititia kwenye awamu zilizopita tumeendelea kufanya hivi ninavyozungumza iko miradi mingine ambayo inaendelea wakati tutakuja na awamu

nyingine ya nne. Kwa hiyo, Mheshimiwa Haonga nikutoe hofu tu kwamba ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba suala la mawasiliano litakuwa kwa wote kama tulivyoanzisha mfuko na nishukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru Bunge Iako kuanzisha Mfuko wa mawasiliano kwa wote umekuwepo kwa miaka kumi na kazi kubwa sana imefanyika ili kuhakikisha mawasiliano yanakuwa bora katika maeneo ya nchi yetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asha Mshua, Aysharose.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi napongeza sana Serikali kwa hatua zake za kusambaza na kusimamia mawasiliano pamoja na kujenga minara sehemu zote. Pamoja na hayo nataka niulize Serikali ina mikakati gani na ya haraka kwa kiasi gani katika kudhibiti au kuimarisha kikosi kazi cha kupambana na hawa wahuni kila siku wanaosumbua wananchi katika kuwaibia pesa zao kupitia mtandaoni kwa kuwaambia tuma hela hii kwa namba hi, tuma hela hii kwa namba hii, Serikali inafanya nini kuwadhibiti wahuni hawa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo mikakati mingi ya kupambana na hali hii ambayo inajitokeza kwa sababu ya ukuwaji wa teknolojia pia changamoto nazo zinakuwa zipo nyingi, tunao mkakati kwanza wa kuelimisha wananchi ili kuwaokoa na hii hali ambayo inajitokeza lakini pia mara kwa mara mnaona tunaendelea kuboresha Sheria na Kanuni hata hili zoezi la uandikishaji wananchi kwa kupitia alama za vidole kufanya usajili wa simu ni hatua hizo madhubuti za kuhakikisha tutaeendelea kumbambana nahii changamoto ambayo ipo. Kwa hiyo, ni kuahakikishie tu kwamba kila wakati changamoto inapojitokeza kama sisi Serikali tunachukuwa hatua hii kuwafanya wananchi wetu kuwa salama.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Aysharose, jiandae Mheshimiwa Mpakate.

MHE. AYSHAROSE N. MATEMBE: Mheshimiwa Mwenyezekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza, changamoto ya mawasiliano iliyopo Same Magharibi inafanana kabisa na changamoto iliyopo Singida Magharibi. Je, ni lini Serikali itapeleka mawasiliano katika maeneo ya lyumbu, Ingombwe, Mtunduru, Sepuka, Mwaru, Ingrasoni, na Irisia ili kuhakikisha kwamba wananchi wa maeneo hayo hawaachwi nyuma na mawasiliano ya simu za mkononi nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ni lini? Wewe waambie mkakati upo tayari karibuni tunaanza kazi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyezekiti, kama nilivyozungumza kwamba maeneo nchi nzima tunafanya juhudizi kuhakikisha kwamba tunaboresha mawasiliano na iko orodha ndefu tu katika Mkoa wa Singida. Nimsihi tu Mheshimiwa Aysharose Matembe na nimpongeze sana kwa kweli hata nilivyo fanya ziara Singida nilipokea orodha ndefu sana kwa ajili ya kuboresha mawasiliano katika mkoa huu. Kwa hiyo, nikuombe tuonane tu ili tuweze kuititia hii orodha ili ufanye kazi ya kuwaelimisha wananchi kwamba Serikali inajipanga mwaka huu wa fedha kuna kazi kubwa itafanyika kwa ajili ya kuendeleza kuboresha...

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mpakate, Mheshimiwa Maftah.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Mwenyezekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swalii la nyongeza Kijiji cha Misaje kilichopo katika Kata ya Malumba na Kijiji cha Imani na Kaza moyo kilichopo Kata ya Lukumbule havina mawasiliano. Je, ni lini Serikali itajenga minara katika vijiji hivyo ili kuwapa mawasiliano wananchi hao?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi ni lini.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naompongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu nilivyofanya ziara Mkoani Ruvuma tulikuwa na mawasiliano mazuri sana kulikuwa na changamoto nydingi sana na hasa hasa maeneo haya ambayo yapo mpakani. Kwa hiyo, nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge avute subira kama nilivyo sema tunaorodha ndefu sana, aje tu tupitie kwa pamoja halafu tutakapoweka minara hii katika maeneo ambayo yameainishwa tutaangalia tena tuone kama kuna maeneo bado yanachangamoto Serikali itakuwa ipo tayari kuendelea kupunguza tatizo ambalo lipo katika maeneo yetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maftah, Mheshimiwa Flatey, Mheshimiwa Olivia.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nimekuwa nayataja maeneo kadhaa ambayo yapo jimbo la Mtwara mjini kwa muda mrefu ndani ya Bunge hili na maeneo hayo, Naulongo, Mkunjanguo, Namayanga, na Mbawala Chini ambapo hakuna mawasiliano ya simu kabisa. Nilikuwa naomba *commitment* ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba ni lini atafanya ziara ya Mtwara MJINI kuja kukagua mguu kwa mguu maeneo haya ili aweze kudhibitisha kwamba maeneo haya yanahitaji mawasiliano kwa simu?

MWENYEKITI: Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anaomba nifanye ziara katika Mkoa wa Mtwara na sisi unafahamu Mheshimiwa Mbunge tuna miradi mingi sana ambayo Wizara yangu inasimamia, nitafanya ziara mapema baada ya Bunge hili katika Mkoa huu wa Mtwara.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Flatei, Mheshimiwa Oliver.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza Kijiji cha Yaeda Chini, Masieda, Endamilay na Mbullu Vijijini wamesaini mikataba ya kujenga minara TTCL na Holotel wameondoka. Je, ni lini Mheshimiwa Waziri watarudi hawa TTCL kujenga minara Mbullu Vijijini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ni lini? Jiandae Mheshimiwa Oliver, jiandae Mheshimiwa Malocho.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatei, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu *TTCL* wamepewa kandarasi ya kujenga minara maeneo mbalimbali. Tatizo au changamoto ambayo ilikuwepo kidogo ni kwamba *TTCL* wanavyopewa kazi sambamba na wakandarasi wengine kwa maana hawa Tigo, Airtel, Vodacom kidogo tumekwenda kusuasua, siyo kusuasua kwa sababu wenyewe sasa kama taasisi ya Serikali lazima wafuate Sheria ya Manunuzi ambayo imetuchelewesha kwenda kusimika minara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, hatua za manunuzi ziko vizuri kwa maana *TTCL* watakuja katika eneo lake na kusimika ile minara ambayo wamepewa fedha na Mfuko wa Mawasiliano. Kwa hiyo, avute tu subira wanakuja na tutaweka hiyo minara kuongeza mawasiliano katika eneo lake.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Oliver.

MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona niulize swali dogo la nyongeza. Matatizo ya usikivu wa simu yaliyopo Same Magharibi ni sawa na matatizo yaliyopo katika Wilaya ya Ngara, Kata za Keza, Mganza, Mrusagamba, Mgoma, Kabanga na Rusumo, ambapo yanaingiliana na nchi jirani

za Rwanda na Burundi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha usikivu wa mawasiliano katika kata hizi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oliver Semuguruka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia maendeleo katika eneo lake. Niseme tu maeneo ya mipakani yanazo changamoto za kuingiliana kwa mawasiliano. Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote jambo hili tumeshalitambua na tuna mkakati wa kuwasiliana na wenzetu nchi za jirani kwa sababu upo utaratibu ambao tunajiwekea kwamba ile minara iwekwe umbali fulani ili ipunguze changamoto hii ya kuingiliana kwenye mawasiliano. Pia, tunaendelea kusimika minara katika maeneo haya ya mipakani ili kuhakikisha wananchi wetu wa maeneo hayo hawapati changamoto hii ya kuingiliana kwa mawasiliano.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Malocha.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Yapo mawasiliano hafifu katika Kijiji cha Kamnyazia, Kata ya Lusaka, Vitongiji vya Mpande. Halotel walishajenga *foundation* toka mwaka jana mwezi Agosti hawajaonekana. Ni lini sasa watakwenda kumalizia kazi ile ili wananchi waweze kupata huduma?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Malocha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wameuliza maswali mengi sana kuonesha kwamba tunazo changamoto kubwa za minara katika maeneo yetu. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge swali hili alilouliza kuhusu mnara wa Halotel nilichukue tu kama suala mahsusili tuweze kujua nini kilichotokea ili tuweze kuliondoa tazito hilo na hatimaye mnara huu uweze kukamilishwa. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mpakate.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Katika Jimbo langu la Nkasi Kusini kuna Vijiji sita vya Kisambala, Ng'undwe, Mlalambo, Kasapa na Izinga, mara nyingi nimepeleka orodha Wizarani ili vipatiwe mawasiliano. Je, ni lini Serikali itavipatia mawasiliano vijiji hivi? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, swali la mwisho kwa kifupi, baada ya hapo ukanywe chai.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu changamoto zilizoko katika maeneo haya sababu ya jiografia yake, naona ndio maana amekaa na jirani yake pale Mheshimiwa Malocha. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba eneo hili ambalo analizungumzia tutaweka msukumo wa kipekee ili tuone changamoto hizi zinakaa vizuri kwa sababu nafahamu kwamba kuna changamoto nyingi sana kwenye eneo lake, kwa hiyo, avute subira. Pia, naomba tuonane na Mheshimiwa Mbunge ili aweze kuona kwenye orodha namna ambavyo tumejipanga ili aweze kwenda kusema kwa wananchi kwamba Serikali hii imejipanga kuhakikisha kweli mawasiliano yanakuwa mawasiliano kwa wote.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, ni bora sasa muweke kanuni ili kuепusha kero hii ya mawasiliano, kila mtu akipewa leseni ya *service provider* aweke mtandao nchi nzima. Mtu anapewa leseni anakuwa Arusha, Dar es Salaam na Mwanza, mikoa mingine hawaendi, wekeni kwenye kanuni hiyo. (*Makofii*)

Tunaendelea na swali la mwisho la Wizara ya Habari, linaulizwa na Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda.

Na. 39

Ufadhilli wa Michezo Inayohusu Wanawake Nchini

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA aliuliza:-

Michezo mingi ikiwemo mpira wa miguu inapata ufadhilli sana hapa nchini kupitia kampuni mbalimbali binafsi na za Kiserikali:-

Je, ni lini Serikali itahakikisha ufadhilli unapatikana kwenye michezo inayohusu wanawake hususan michezo ya ngumi kwa wanawake?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nisahihishe dhana ya kwamba michezo inayowahusisha wanaume inapata "ufadhili sana" nikinukuu maneno aliyatumia Mheshimiwa Mbunge, kuliko inayowahusisha wanawake. Mfano hai ni Ligi Kuu ya Mpira wa Miguu upande wa Wanaume kwa msimu wa 2018/2019 ambayo ilikosa

udhamini na kusababisha matatizo makubwa ya maandalizi na usafiri kwa timu zote 20 zilizoshiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufadhilli haushinikizwi na Serikali bali ni suala la hiari upande wa wafadhili ambao huchukua hatua hiyo wakishaziona fursa za kibashara na kijamii upande wao. Wajibu wa Serikali ni kujenga mazingira rafiki ya ufadhilli huo bila kujali jinsia. Hivi sasa Tanzania ina Ligi Kuu ya Mpira wa Miguu kwa Wanawake ambayo inadhaminiwa na Kampuni ya Vinywaji ya *Serengeti Breweries* kuititia bia yake ya *Serengeti Lite*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa riadha, Kampuni ya *Multichoice* imekuwa mstari wa mbele kudhamini wanariadha bora wanaojitokeza na kuandaa makambi ya mazoezi bila ubaguzi wa jinsia. Kampuni ya *SportPesa* pekee imejitokeza kumfadhilli Mwanamasumbwi Mwakinyo aliyekuwa namba 174 kwa ubora Duniani katika uzito wake, baada ya kumtwanga Eggington wa Uingereza, wakati huo namba akiwa 8 kwa ubora duniani. Hakuna kigezo kingine kilichotumika na *SportPesa* kumfadhilli Mwakinyo zaidi ya weledi alionunesha katika mchezo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwaomba wadau wote wa michezo nchini wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, kusaidia kushawishi makampuni, taasisi na wadau wenye uwezo kifedha, kudhamini na kufadhili maendeleo ya michezo yote nchini ukiwemo mchezo wa ndondi upande wa wanawake.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sophia.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kutohana na jibu la msingi la Serikali, Serikali inao wajibu wa kuwekeza kwenye michezo yote ndipo wafadhili wanafuatia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, mchezo wa ngumi kama navyoutetea hauna ufadhilli wa Serikali ili kupata timu nzuri itakayotuwakilisha kimataifa. Ni lini Serikali itaandaa

maeneo ya wanamichezo hawa kufanya mazoezi ili waweze kuwa vizuri na kuweza kushinda katika timu za kimataifa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Wizara husika, hasa kwenye ngumi, ameonesha jitihada za kusaidia wachezaji wa ngumi kwa sasa. Serikali kwa wachezaji wa ngumi wanaume tayari wameonesha jitihada ni lini sasa watafanya hivyo kwa wachezaji wa ngumi wa kike ambao bado wako nyuma kwenye vifaa vyta kufanya mazoezi ili waweze kushinda? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumile fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa sababu ni miongoni mwa mapromota wanawake wachache kabisa ambao tunao nchini Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikianza na swalii lake la kwanza ambapo amesema kwamba Serikali ina wajibu wa kuwekeza katika michezo yote. Ni kweli kwamba sisi kama Serikali tuna wajibu wa kusimamia lakini kazi kubwa ya Serikali ni kuandaa miundombinu na kuweka mazingira wezeshi ya kisera pamoja na sheria. Suala la ufadhilli wa michezo yote nchini Tanzania ni la vyama pamoja na mashirikisho ambayo ndiyo yanasmamia michezo hiyo vilevile kwa kushirikiana na wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, sisi kama Serikali tunao mpango wa kuhakikisha kwamba tunafanya uwekezaji mkubwa zaidi katika michezo. Ndiyo maana umeona katika kipindi cha hivi karibuni nchi yetu imepata fursa ya kuweza kushiriki kwenye mashindano mbalimbali na sisi kama Serikali tumejipanga kuhakikisha kwamba tunaeendelea kushirikiana na wadau kuhakikisha kwamba tunafanya ufadhilli katika michezo mbalimbali ukiwepo michezo wa ngumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye swali lake la pili pia ametaka kujua ni lini sasa Serikali itaanza kuweka mkakati kuhakikisha kwamba tunakuza mchezo huu wa ngumi. Kama ambavyo amezungumza ni kweli sisi kama Wizara ya Michezo kwa kipindi cha hivi karibuni tumefanya jitihada kubwa sana ya kuhakikisha kwanza tunaboresha mchezo huu wa ngumi na jambo la msingi ambalo tumelifanya ni kuhakikisha kwamba tunaunda Kamisheni ya mchezo huu wa ngumi. Lengo ilikuwa ni kuhakikisha kwamba mchezo huu wa ngumi unapata mafanikio makubwa kitaifa na kama ambavyo tumeshuhudia kwamba ni mchezo ambao tunaamini kabisa kama uwekezaji ukifanyika vizuri utakuwa na mafanikio makubwa

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi kwa upande wa Serikali tayari tulishaanza kuweka mikakati na matunda yameanza kuonekana ndiyo maana jana tulishuhudia wanamasumbwi watatu wamekuja hapa na mikanda ya kutosha kabisa. Kwa hiyo, kama Serikali tunatambua umuhimu wa mchezo huu na tunaahidi kwamba tutaedelea kufanya uwekezaji mkubwa vilevile kwa kushirikiana na wadau. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha, swali la mwisho la nyongeza ni la Mheshimiwa Dkt. Kikwembe.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara hii imekuwa na maswali machache, naomba niulize swali langu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Kavuu, usikivu wa *TBC radio* pamoja na *television* umekuwa ni wa shida. Je, Serikali inawaeleza nini wananchi wa Kavuu na kwamba ni lini watapata mawasiliano hayo kwa uhakika kwa kuwa suala hili linaangukia katika Wizara hii?

MWENYEKITI: Swali lako halitokani na swali la msingi, kwa hiyo, naomba radhi Mheshimiwa Waziri hataweza kulijibu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni kipindi cha wageni. Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambaye ni Ndg. Augustine Masubo, ni Mwandishi wa Vitabu vya Kiswahili kutoka Musoma Mkoa wa Mara. Karibu. (*Makofii*)

Wageni 34 wa Mheshimiwa Mwita Waitara, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya TAMISEMI ambao ni Watendaji wa Kata kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Mkoani Mara. (*Makofii*)

Wageni 36 wa Mheshimiwa George Lubeleje ambao ni Kwaya ya Nazareti ya Kanisa la Anglikana Chamwino liliopo Jijini Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Aidan Nzala. Karibuni. (*Makofii*)

Wageni 21 wa Mheshimiwa Martha Mlata na Mheshimiwa Mwigulu ambao ni Watendaji wa Kata kutoka Wilaya ya Iramba, Mkoa wa Singida. (*Makofii*)

Sehemu na Ibara mbalimbali za Muswada huu ambayo kwa sehemu kubwa yamezingatiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maelezo ya Jumla kuhusu uchambuzi wa Muswada. Kamati ilipitia na kufanya uchambuzi wa Ibara zote Hamsini na Mbili (52) na vifungu vyote vya sheria vinavyopendekezwa kurekebishwa. Uchambuzi huo ulizingatia mfumo wa sasa wa Sheria (Legal Framework) na kitaasisi (Institutional Framework) katika kusimamia sekta zinazoguswa na Muswada huu, kama ifuatavyo:-

- (a) Marekebisho yenye kutekeleza Hati Idhini ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Mwaka wa 2018, kupitia Hati Idhini yiliyochapishwa katika Matangazo ya Serikali Na. 48, Na. 49 na Na. 50 ya Mwaka 2018, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alifanya Mabadiliko katika Mfumo wa Kisheria (*Legal Regime*) yenye kuanzisha mfumo mpya wa uwakilishi na utetezi wa Serikali na Taasisi zake zote katika Masuala ya Kisheria ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mabadiliko hayo, mfumo wa Sekta ya Sheria nchini kupitia ofisi mbalimbali za kiusimamizi na kiutekelezaji zililitaji kufanyiwa marekebisho ili kuzingatia mabadiliko hayo ya kimfumo kwa lengo la kuondoa changamoto za kiutendaji mionganoni mwa Taasisi husika kupitia vifungu mbalimbali vya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, marekebisho yanayopendekezwa chini ya Sheria ya Mawakili, Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sheria Mashauri dhidi ya Serikali na Sheria ya Taifa ya Mashtaka, kupitia Muswada huu Na. 4 wa Mwaka 2019 ni mwendelezo wa mjadala wa Kamati ya Katiba na Sheria katika Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 mwaka 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ili kuweka vizuri kumbukumbu za Bunge lako Tukufu, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, sharti la kuzuia Mawakili wa Serikali na Maafisa wa Sheria ambao ni Watumishi wa Umma kutotoa huduma za Uwakili wa Kujitegemea linalopendekezwa chini ya Sheria ya Mawakili na Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali halikuwepo kwenye marekebisho ya Mwaka 2018.

(b) Marekebisho yenyne Mwelekeo wa Misingi ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, yapo masuala yanayopendekezwa katika Muswada huu Na. 4 Mwaka 2019 ambao msingi wake ni Makubaliano ya Kimataifa yaliyordhiwa na nchi ya Tanzania. Miiongoni mwa masuala yaliyobainika kuwa na Misingi ya Makubaliano ya Kimataifa ni pamoja na:-

(i) Marekebisho yanayopendekezwa chini ya Sheria ya Urejeshwaji wa Wahalifu, Sura 368, katika sehemu ya Tano ya Muswada, ambapo Ibara ya 19 inaongeza kifungu cha 8(a) ili kumuwezesha Waziri anayehusika na masuala ya Sheria kuwa na mamlaka ya kumkabidhi mhalifu wa nje kwa mtu wa nchi nyingine aliyeidhinishwa na hiyo nchi inayoomba kukabidhiwa mhalifu (*International Criminal Proceedings under International Obligations*). Sheria hii ni sehemu ya utekelezaji wa Ibara ya 9 ya *International Convention for the Protection of all Persons from enforced disappearance*), ikisomwa pamoja na *International Covenant on Civil and Political rights-ICCPR, 1966* pamoja na *Bilateral Extradition Treaties* ambazo zimeridhiwa na Tanzania.

(ii) Marekebisho yanayopendekezwa chini ya Sheria ya Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania, Sura 66. Madhumuni ya msingi ya marekebisho haya pamoja na masuala mengine pamoja yanalenga kukidhi masuala mawili ya msingi:-

Moja; Kuifanya sheria hii itumike Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar pamoja na Mbili; ni Kupanua wigo wa

majukumu na Mamlaka ya Chama hicho ili kukidhi viwango vya Kimataifa (*International Standards*).

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa, Sheria ya Chama cha Msalaba Mwekundu, ni sehemu ya utekelezaji wa Mkataba wa *Geneva Convention on International Federation of Red Cross and Red Cross Societies of 1949 and It's Protocols of 1977*(Currently named *The Geneva International Committee of Red Cross*) ambao Tanzania ni Mwanachama. Hivyo, Majukumu ya Chama hicho msingi wake ni Mikataba ya Kimataifa ambayo kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania, majukumu yake hayatakiwi kutekelezwa upande mmoja tu wa Tanzania Bara kama ilivyo kwenye Sheria ya sasa, kwa kuwa ni suala la Muungano, hivyo sheria hiyo ilitakiwa itumike Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Kwa misingi hiyo, marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria hili, pamoja na kuimarisha Chama hicho pia yanalenga kuondoa dhaifu huo.

(c) Marekebisho ya usimamizi wa Haki jinai chini ya Ofisi za Mkurugenzi wa Mashtaka na TAKUKURU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nyakati tofauti, Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameonesha nia yake njema ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuhakikisha haki jinai nchini inatolewa kwa wakati. Hii ni pamoja na kupunguza mlundikano wa majalada ya makosa ya kijinai ikiwemo makosa ya Rushwa chini ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na TAKUKURU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo Marekebisho yanayopendekezwa chini ya Sheria ya Taifa ya Mashtaka, Sura 430 na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura 329 pamoja na masuala mengine muhumu, yana lengo la kupunguza mlundikano wa majalada ya mashauri ya kijinai na kuharakisha utoaji haki jinai kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uchambuzi huo wa kimaudhui na kimantiki katika Muswada kwa kila Sheria inayopendekezwa kurekebishwa, naomba kuthibitisha kuwa,

yapo masuala mbalimbali yaliyobainishwa na Kamati ambayo kwa maoni ya Kamati, Bunge lako Tukufu linaweza kuyazingatia wakati wa kupitia Ibara kwa Ibara. Masuala hayo yanahu:-

(i) Zuijio la Mawakili na Maafisa wa Sheria katika Utumishi wa Umma kuzuiwa kutoa huduma za Uwakili wa Kujitegemea, kama ilivyobainishwa katika Merekebisheso ya Sheria ya Mawakili Sura 341, pamoja na Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura 268.

(ii) Utekelezaji wa Mamlaka ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka na Wasaidizi wake katika kusimamia masuala ya '*Plea Bargaining*' na '*Plea Agreement*' na masuala mengine ya Kijinai kama ilivyobainishwa katika Marekebisheso ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura 20.

(iii) Uzingatiaji wa Misingi ya Katiba kwa Mali ya Mtu asiyehusika na Makosa ya jinai kushikiliwa kwa ajili ya kutaifishwa baada ya kuhusishwa na Makosa ya Jinai kama yalivyoainishwa katika Marekebisheso ya Sheria ya Mapato yatokanayo na Uhali, Sura 256.

(iv) Upanuaji wa Huduma za Chama cha Msalaba Mwekundu ili zitolewe kwa pande zote za Muungano kama ilivyuoainishwa katika Sheria ya Chama cha Msalaba Mwekundu, Sura 66.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni hayo, Kamati inakubalina na nia njema ya Serikali ya kuleta Muswada huu unaopendekeza marekebisheso katika Sheria Kumi na Moja pamoja na kupendekeza marekebisheso machache katika Muswada huu, ambayo kwa ujumla yamepokelewa kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisheso lilioletwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Serikali imekubaliana na Kamati ya kufanya marekebisheso makubwa kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisheso. Kwa

ujumla, Kamati inaipongeza Serikali kwa kubainisha upungufu katika sheria hizi na kuandaa mapendekezo ya kuboresha yaliyowasilishwa katika Muswada huu kupitia Jedwali la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo kwa kila Ibara. Ili kulisaidia Bunge lako Tukufu kupitia Ibara kwa Ibara na kufanya uamuzi bora wa Kibunge, Kamati ilifanya mapitio ya Ibara zote Hamsini na Mbili katika sehemu Kumi na Mbili za Muswada huu. Matokeo ya hatua hii kwenye ngazi ya Kamati ni pamoja na kubaini baadhi ya Ibara za Muswada huu kuwa zinatafaa kuboreshwa zaidi. Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 84(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilishauri ipasavyo mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa, ushauri huo umechangia kuwasilishwa kwa Jedwali la Marekebisho lilitolewa na Mtoa Hoja. Kwa ujumla mapendekezo ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya maboresho. Marekebisho ya Kiuandishi; Kamati imebaini kuwa Ibara 12 zenye dosari mbalimbali za kiuandishi, na kutoa mapendekezo ambayo yote yamekubaliwa na Serikali, kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili ni marekebisho ya msingi. Pamoja na kubaini dosari za kiuandishi, pia Kamati ilibaini baadhi ya Ibara za Muswada kuwa na dosari zinazohitaji marekebisho ya msingi ili kuziwezesha sheria hizi kuleta mantiki illyokusudiwa na kurahisisha utekelezaji wake, kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Marekebisho. Hivyo, Kamati inapendekeza marekebisho yafanyike katika ibara hizo kama ifuatavyo:-

(a) Ibara ya 5 chini Merekebisho ya Sheria ya Mawakili Sura 341 pamoja na Ibara ya 44 katika Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura 268 zinazoweka zuio kwa Mawakili na Wanasheria katika Utumishi wa Umma kutoa huduma za

uwakili wa kujitegemea, Kamati imependekeza zifayiwe marekebiso ili waruhusiwe huduma mbalimbali zisizohusisha Serikali kama vile huduma za viapo na uanzishaji wa hati mbalimbali, kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Marekebiso. Kimsingi Serikali imekubali kufanya marekebiso ambayo Kamati imeridhia.

(b) Marekebiso yanayopendekezwa chini ya Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo, Sura 108, yameboreshwa na Kamati kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebiso chini ya Ibara ya 8 ya Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Msingi wa marekebiso haya umeainishwa katika Ibara ya 7 inayorekebisha kifungu cha 3 cha Sheria na Ibara ya 8 inayorekebisha kifungu cha 5 cha Sheria hii, ambapo, wigo wa mfumo wa Usajili wa Vizazi na Vifo umepanuliwa na kurekebishwa ili kuiwezesha Serikali kusambaza rasilimali kwa wananchi kupitia Msajili Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni pamoja na kuwatambua Watendaji wa Kata na Vijiji kama Wasajili Wasaidizi baada ya kukasimiwa mamlaka hayo na Msajili Mkuu, pamoja na kuweka utaratibu rasmi wa kufuata wakati wa kuasili mtoto (*adoption*) na utaratibu wa kutoa Hati ya Usajili baada ya uasili wa mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebiso haya yanamlenga Msajili Mkuu na Watendaji wa Vijiji na Kata pamoja na Watoto walaji (*beneficiaries*), ambapo taratibu zinazoainishwa katika marekebiso haya zitatekelezwa na Watendaji wa Kata na Vijiji kwa niaba ya Msajili Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhia mapendekezo haya kama yalivyo kwa kuwa yanalenga kuboresha haki na ustawi wa mtoto na yanazingatia misingi ya Kimataifa ya Haki za Mtoto chini ya ya *UN Convention on the Rights of a Child 1989*, ambayo Tanzania ni Mwanachama. Aidha, Marekebiso haya yanalenga kuzingatia misingi ya kisheria iliyokwisha ainishwa katika Sheria Mbalimbali

zinazohusu Haki za Mtoto, kama vile Sheria ya Mtoto, Sura 13, *The Law of The Child Act, 2009, (Sura 13)*, pamoja na Kanuni zake kama zilivyoanishwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapendekeza marekebisho katika Ibara ya 16 kwenye Kifungu cha 194 (a), (1) kuruhusu ndugu au rafiki wa karibu wa mtuhumiwa kuwepo wakati wa kufanya *Plea Bargaining* au *Plea Agreement*, kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Marekebisho. Aidha, Kamati inapendekeza marekebisho katika Kifungu Kipyaa cha 194 (c) ili kuainisha sharti la kuwepo kibali cha maandishi kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kabla ya Wasaidizi wake kufanya *Plea Agreement*. Lengo la marekebisho haya ni kuzuia matumizi mabaya ya Mamlaka kwa waendesha Mashtaka nchini wakati wa utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapendekeza kuwa, Ibara ya 26 chini ya Sheria ya Taifa ya Mashtaka, Sura 430, ifanyiwe marekebisho kwa kuainisha Maafisa ambao Mkurugenzi wa Mashtaka atakasimu mamlaka yake kutoa ridhaa katika ngazi ya Mikoa na Wilaya, kama ilivyoainishwa katika jedwali la Marekebisho. Kimsingi Serikali imeridhia kufanya marekebisho haya ili kuwaruhusu Mawakili wa Serikali Wafawidhi wa Mikoa na Wilaya kuendelea kutoa idhini ya kushtaki kwa niaba Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho haya yanalenga kupunguza majalada ya mashauri ya kijinai ambayo yamekuwa ni kero kubwa sana kwa muda mrefu kwa wananchi kwa sharti la kusubiri kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya jumla Kamati ilibaini masuala mbalimbali ya jumla ambayo muhimu yakaboreshwa kwa lengo la kuleta ufanisi wa kutosha kwenye sekta husika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Maelezo ya Serikali yameainisha kuwa, ipo nia njema ya kuweka zuio la

Maafisa wa Sheria katika Utumishi wa Umma kutojihusisha na huduma za Uwakili wa Kujitegemea, ikiwa ni pamoja na kuondoa mgongano wa mastlahi binafsi kwa Mashauri ambayo yanahusu Serikali. Na kwa kuwa, hatua ya Serikali kuboresha sharti hilo kwa kuwaruhusu Mawakili na Maafisa wa Sheria husika kutumia Muhuri wa Mwanasheria wa Serikali kutoa huduma za viapo na huduma ndogo ndogo za kisheria zisizohusisha utetezi Mahakamani, hakuondoi chochote chenye tija kwa wanataaluma hao ambao wametumia rasilimali nyingi sana ikiwemo muda hadi kufikia hatua hiyo muhimu na maalum katika sekta ya sheria. Na kwa kuwa, hatua hiyo inapunguza kipato halali za kundi hilo la Wanataaluma na hata inaweza kuwapunguzia weledi kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, Kamati inashauri Serikali kuwa Mawakili na Maafisa wa Sheria ambao ni Watumishi wa Umma waanze kulipwa posho ya kitaaluma yenye kuambatana na mishahara yao (*Professional Allowance*)na kuwaboreshea mazingira yao ya kazi kwa ujumla, ili kuwaongeza motisha na kipato cha kumudu mahitaji ya familia zao, naomba nirejee sehemu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo kamati inaishauri Serikali kuwa Mawakili na Maafisa wa Sheria ambao ni Watumishi wa Umma waanze kulipwa posho ya kitaaluma yenye kuambatana na mishahara yao (*professional allowance*) na kuwaboreshea mazingira yao ya kazi kwa ujumla ili kuwaongeza motisha na kipato cha kumudu mahitaji yao na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, kuwepo mafunzo ya mara kwa mara ya ndani na nje ya nchi kwa Mawakili na Maafisa wa Sheria wa Serikali ili kuendelea kuwaongeza weledi kwa lengo la kuongeza ufanisi zaidi katika majukumu yao ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, udhibiti wa masuala ya kijinai ni majukumu mtambuka pasipo kuathiri Mamlaka na Wajibu wa Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa

Mashtaka, kwa mujibu wa Ibara ya 59 (b),(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,1977. Na kwa kuwa, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ni mdau muhimu kwa udhibiti wa makosa ya jinai yanayohusu rushwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, Kamati inashauri kuwa, Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka ishirikiane kwa ukaribu sana na Ofisi za TAKUKURU katika ngazi ya Wilaya na Mikoa yote nchini ili kupunguza mlundikano wa majalada kwa kurahisisha utoaji Haki Jinai kwa wakati, bila kuwanyanyasa watuhumiwa na bila kuathiri misingi ya utawala bora iliyowekwa kwa mujibu wa sheria za nchi kati ya vyombo hivi pamoja na vyombo vingine husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, pamoja na Kamati kuridhia marekebisho yanayopendekezwa Sehemu ya Tatu ya Muswada katika Sheria ya Vizazi na Vifo, Sura 108, na kwa kuwa, marekebisho haya yanalenga kusogezza huduma za usajili na usaili wa mtoto hadi kwenye ngazi ya Kata na Vijiji, na kwa kuwa utekelezaji wa marekebisho haya unahuishisha pia Sheria mbalimbali nchi kama zilivyoainishwa katika taarifa hii.

Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali kuwa ijiandae kuwajengea uwezo Watendaji wote wa Kata na Vijiji Nchini ili waweze kuwa na weledi wa kutosha katika kusimamia na kutekeleza majukumu yao mapya kwa ufanisi uliokusudiwa. Hii ni pamoja na kuwapatia rasilimali mbalimbali zitakazohitajika wakati wa utekelezaji wa majukumu yao kwa mujibu wa Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena naomba nimkushukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kutoa kibali ili kamati yangu ya Katiba na Sheria iweze kuufanya kazi Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba niwatambue kwa kuwashukuru wadau Mbalimbali waliofika na kutoa

Maoni yao na Ushauri wao kwa Kamati yangu ambao umesaidia kuboresha Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumtambua na kumshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Prof. Adelardus Kilangi, Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustine P. Mahiga, (Mbunge), Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, (Mbunge) pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali bila kumsahau Prof. Mchome, Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Katiba na Sheria. Kwa dhati kabisa wameisaidia Kamati kukamilisha uchambuzi wa Muswada huu kwa wakati. Aidha, Kamati inatambua na kumshukuru sana kila Waziri na watendaji wote waliofika mbele ya Kamati hii kwa lengo la kuisaidia Kamati kukamilisha kazi hii kwa ufanisi mkubwa na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa weledi na umahiri wao waliouonesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa Mapendekezo ya msingi ya kuboresha. Naomba Majina yao yote yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge yaani *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususanii Katibu wa Bunge, Mchapakazi Ndugu Stephen Kagaigai kwa Uongozi thabitii ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati yangu. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald Magili, Mkurugenzi Msaidizi wa Kitengo cha Huduma za Kisheria Bungeni, Ndugu Leocardio Kapongwa, Mwanasheria wa Serikali Mkuu, Ndugu Prudens Rweyongeza, Wanasheria Wasaidizi wa Bunge, Ndugu Maria Mdulugu, Ndugu Fungo Matamus, Ndugu Thomas Shawa, Ndugu Evelyn R. Shibandiko, Ndugu Hawa Manzurya, Katibu wa Kamati Ndugu Stanslaus Kagisa, pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Rahel Masima waliofanikisha kazi ya Uchambuzi na

uratibu wa shughuli za Kamati hii kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI (NA.4) WA MWAKA 2019 (*THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.4) BILL, 2019*)
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, tarehe 26 Juni, 2019, wakati wa Kikao cha Hamsini na Tatu cha Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.4 wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2019*] ulisomwa mara ya kwanza Bungeni. Baada ya hapo, Mheshimiwa Spika alizingatia Masharti ya Kanuni ya 84(1) kwa pamoja na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 na kuupeleka Muswada huo kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa, Kamati iliujadili Muswada huo kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni za Kudumu za Bunge hususan Sehemu ya Nane ya Kanuni za Bunge inayohusu masharti ya Jumla kuhusiana na kutunga Sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria Kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) Wa Mwaka 2019 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2019*), kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza masharti ya Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilikutana na Serikali katika **Ukumbi Na.9** uliopo Jengo la Utawala katika Ofisi za Bunge Dodoma, mnamo tarehe 21 Agosti, 2019 ili kupokea maelezo kuhusu Muswada husika.

Mheshimiwa Spika, Maelezo ya Serikali yalionesha kuwa, Muswada huu unakusudia kufanya marekebisho katika Sheria Kumi na Moja (11) ili kuondoa upungufu ambao umebainika wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo. Orodha ya Sheria Kumi na Moja (11) zinazopendekezwa kufanyiwa Marekebisho ni hizi zifuatazo:-

- a) Sheria ya Mawakili, Sura 341,
- b) Sheria ya Usajili wa Viazi na Vifo, Sura 108,
- c) Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura 20,
- d) Sheria ya Urejeshwaji wa Wahalifu, Sura 368,
- e) Sheria Mashauri dhidi ya Serikali, Sura 5,
- f) Sheria za Mahakama ya Mahakimu Wakazi, Sura 11,
- g) Sheria ya Taifa ya Mashitaka, Sura 430,
- h) Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura 329,
- i) Sheria ya Mapato yatokanayo na Uharifu, Sura 256,
- j) Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura 268, na

- k) Sheria ya Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania, Sura 66.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea maelezo hayo, Kamati ilizingatia masharti ya **Kanuni ya 84(2)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kutuma mialiko kwa Asasi za Kiraia Kumi na kutoa matangazo ya kuwaalika wadau mbalimbali wafike mbele ya Kamati kwa lengo la kuisaidia katika Uchambuzi wa Muswada huu.

Kwa mialiko hiyo, jumla ya Asasi za kiraia Saba (7) ziliwakilishwa na Jumla ya Wadau Kumi na Watano (15). Wadau hao, walipewa fursa ya kusikilizwa wakiwasilisha maoni yao na wengine wakiwasilisha maoni yao kwa njia ya maandishi. Orodha ya Taasisi hizo ni kama ifuatavyo:

- (a) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*Legal and Human Rights Centre*) – *LHRC*;
- (b) TWAZEZA;
- (c) Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (*Tanganyika Law Society -TLS*);
- (d) UDOM (Shule ya Sheria),
- (e) *Tanzania Music Foundation*;
- (f) Shirikisho la Sanaa za Ufundii-TAFCA; na
- (g) Umoja wa Wasanii Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wadau wote kwa ushirikiano wao na Bunge lako tukufu, ambao kwa nyakati tofauti, wakiwasilisha maoni yao kuisaidia Kamati kuboresha Muswada huu. Nakiri kuwa michango ya Wadau hao imewezesha Wajumbe kufikia hatua hii.

2.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia masuala ya awali katika utangulizi wa Taarifa hii, napenda kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu maoni ya Kamati ambayo yametokana na maelezo ya Serikali pamoja na uchambuzi wa Kamati katika Sehemu na Ibara mbalimbali za Muswada na ambayo kwa sehemu kubwa yamezingatiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

2.1 *Maelezo ya Jumla kuhusu uchambuzi wa Muswada*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia na kufanya uchambuzi wa Ibara zote Hamsini na Mbili (52) na vifungu vyote vya Sheria vinavyopendekezwa kurekebishwa. Uchambuzi huo ulizingatia mfumo wa sasa wa Sheria (*Legal Framework*) na kitaasisi (*Institutional Framework*) katika kusimamia Sekta zinazoguswa na Muswada huu, kama ifuatavyo:-.

a) Marekebisho yenyeye kutekeleza Hati Idhini ya Rais;

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Mwaka wa 2018, kupitia *Hati Idhini yillyiochapishwa katika Matangazo ya Serikali Na.48, 49 na 50 ya Mwaka 2018*, Mhe.Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alifanya Mabadiliko katika Mfumo wa Kisheria (*Legal Regime*) yenyeye kuweka/kuanzisha mfumo mpya wa uwakilishi na Utetezi wa Serikali na Taasisi zake zote katika Masuala ya Kisheria ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kutoptanana na mabadiliko hayo, mfumo wa Sekta ya Sheria nchini kupitia Ofisi mbalimbali za kiusimamizi na kiutekelezaji zililitaji kufanyiwa marekebisho ili kuzingatia (*to encorporate*) mabadiliko hayo ya kimfumo

kwa lengo la kuondoa changamoto za kiutendaji miongoni mwa Taasisi husika kuitia vifungu mbalimbali nya Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, marekebisho yanayopendekezwa chini ya Sheria ya Mawakili, Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sheria Mashauri dhidi ya Serikali na Sheria ya Taifa ya Mashitaka, kuitia Muswada huu Na. 4 wa Mwaka 2019 ni mwendelezo wa mjadala wa Kamati ya Katiba na Sheria katika Muswada wa Sheria ya Mrekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.2 mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ili kuweka vizuri kumbukumbu za Bunge lako tukufu, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, sharti la kuzuia Mawakili wa Serikali na Maafisa wa Sheria ambao ni Watumishi wa Umma kutotoa huduma za uwakili wa kujitegemea linalopendekezwa chini ya Sheria ya Mawakili na Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali halikuwepo kwenye marekebisho ya Mwaka 2018.

b) Marekebisho yenye muelekeo wa Misingi ya Kimataifa:-

Mheshimiwa Spika, pia uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, yapo masuala yanayopendekezwa katika Muswada huu Na.4 Mwaka 2019 ambayo msingi wake ni Makubaliano ya Kimataifa yaliyordhiwa na Nchi ya Tanzania. Miongoni mwa masuala yaliyobainika kuwa na Misingi ya Makubaliano ya Kimataifa ni pamoja na:-

i) Marekebisho yanayopendekezwa chini ya Sheria ya Urejeshwaji wa

Wahalifu, Sura 368, katika sehemu ya Tano ya Muswada, ambapo Ibara ya 19 inaongeza kif.cha 8A ili kumuwezesha Waziri anayehusika na masuala ya Sheria kuwa na mamlaka ya kumkabidhi mhalifu wa nje kwa mtu wa nchi nyingine aliyeidhinishwa na hiyo nchi inayoomba kukabidhiwa mhalifu (*International Criminal Proceedings under International Obligations*).

Mheshimiwa Spika, Sheria hii ni sehemu ya **utekelezaji wa Ibara ya 9 ya International Convention for the Protection for all Persons from enforced disappearance**), ikisomwa pamoja na **International Covenant on Civil and Political rights-ICCPR, 1966** pamoja na **Bilateral Extradition Treaties** ambazo zimeridhiwa na Tanzania.

- ii) **Marekebisho yanayopendekezwa chini ya Sheria ya Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania, Sura 66** katika sehemu ya Kumi na Mbili ya Muswada, kuanzia Ibara ya 45 hadi 52, yenye jumla ya vifungu Vitano(5) (Kif. cha 1, 2, 3 na 7) vinavyorekebisha katika Ibara ya 46, 47, 49, 50 na 51, na 52.

Mheshimiwa Spika, Madhumuni ya msingi ya marekebisho haya pamoja na masuala mengine muhimu, yanalenga kukidhi masuala mawili ya msingi:-

- i) Kuifanya sheria hii itumike Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar pamoja na;

- ii) Kupanua wigo wa majukumu na Mamlaka ya Chama hicho ili kukidhi viwango vya Kimataifa (*International Standards*).

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa, Sheria ya Chama cha Msalaba Mwekundu, ni sehemu ya utekelezaji wa Mkataba wa *Geneva Convention on International Federation of Red Cross and Red Cross Societies of 1949 and It's Protocols of 1977(Currently named The Geneva International Committee of Red Cross) ambao Tanzania ni Mwanachama.*

Hivyo, Majukumu ya Chama hicho msingi wake ni Mikataba ya Kimataifa ambayo kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania, majukumu yake hayatakiwi kutekelezwa upande mmoja tu wa Tanzania Bara kama ilivyo kwenye Sheria ya sasa, kwa kuwa ni suala la Muungano, hivyo Sheria hiyo ilitakiwa itumike Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Kwa misingi hiyo, marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria hii, pamoja na kuimarisha Chama hicho pia yanalenga kuondoa dhaifu hilo.

- c) **Marekebisho ya usimamizi wa Haki jinai chini ya Ofisi za DPP na TAKUKURU;**

Mheshimiwa Spika, kwa nyakati tofauti, Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameonesha nia ya njema ya Serikali ya awamu ya Tano ya kuhakikisha haki jinai nchini inatolewa kwa wakati. Hii ni pamoja na kupunguza mlundikano wa majalada ya makosa ya kijinai ikiwemo makosa ya Rushwa chini ya Ofisi ya DPP na TAKUKURU.

Kwa msingi huo, **Marekebisho yanayopendekezwa chini ya Sheria ya Taifa ya Mashtaka, Sura 430 na Sheria ya Kuzua na Kupambana na Rushwa, Sura 329** pamoja na masuala mengine muhumu, yana lengo la kupunguza mlundikano wa majalada ya mashauri ya kijinai na kuharakisha utoaji haki jinai kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uchambuzi huo wa kimaudhui na kimantiki katika Muswada kwa kila Sheria inayopendekezwa kurekebishwa, naomba kuthibitisha kuwa, yapo masuala mbalimbali yaliyobainishwa na Kamati ambayo kwa maoni ya Kamati, Bunge lako tukufu linaweza kuyazingatia wakati wa kupitia ibara kwa ibara. Masuala hayo yanahuusu:

- i) Zuio la Mawakili na Maafisa wa Sheria katika Utumishi wa Umma kuzuiwa kutoa huduma za Uwakili wa Kujitegemea, kama ilivyobainishwa katika **Merekebisho ya Sheria ya Mawakili (Sura 341)** pamoja na **Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura 268**,
- ii) Utekelezaji wa Mamlaka ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka na Wasaidizi wake katika kusimamia masuala ya '**Plea Bargaining**' na '**Plea Agreement**' na masuala mengine ya kijinai kama ilivyobainishwa katika **Marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai**, Sura 20,
- iii) Uzingatiaji wa Misingi ya Katiba kwa Mali ya Mtu asiyehusika na Makosa ya

jinai kushikiliwa kwa ajili ya kutaifishwa baada ya kuhusishwa na Makosa ya Jinai kama yalivyoainishwa katika *Marekebisho ya Sheria ya Mapato yatokanayo na Uharifu, Sura 256*, na

- iv) Upanuaji wa Huduma za Chama cha Msalaba Mwekundu ili zitolewe kwa pande zote za Muungano kama ilivyoainishwa katika *Sheria ya Chama cha Msalaba Mwekundu, Sura 66*.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni hayo, Kamati inakubalina na nia njema ya Muswada huu unaopendekeza marekebisho katika Sheria Kumi na Moja (11) pamoja na kupendekeza marekebisho machache katika Muswada huu, ambayo kwa ujumla yamepokelewa kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho lililoletwa na Serikali.

Kwa ujumla, Kamati inaipongeza Serikali kwa kubainisha upungufu katika sheria hizi na kuandaa mapendekezo ya kuboresha yaliyowasilishwa katika Muswada huu kuitia Jedwali la Serikali.

2.2 *Maoni na Mapendekezo kwa kila Ibara*

Mheshimiwa Spika, ili kulisaidia Bunge lako tukufu kuitia ibara kwa ibara na kufanya uamuzi bora wa Kibunge, Kamati ilifanya mapitio ya ibara zote Hamasini na Mbili (52) katika Sehemu Kumi na Mbili za Muswada huu. Matokeo ya hatua hii kwenye ngazi ya Kamati ni pamoja na kubaini baadhi ya ibara za Muswada huu kuwa zinafaa kuboreshwa zaidi. Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 84(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilishauri ipasavyo Mtoa hoja.

Naomba kutoa taarifa kuwa, ushauri huo umechangia kuwasilishwa kwa Jedwali la Marekebisho lilitolewa na Mto Hoja. Kwa ujumla mapendekezo ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

2.2.1 Mapendekezo ya Marekebisho ya kiuandishi

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini jumla ya **ibara 12** zenyet dosari mbalimbali za kiuandishi, ambazo ni Ibara ya 8, 10, 11, 12, 16, 20, 21, 23, 24, 43, 49 na 51 na kutoa mapendekezo yake ambayo yote yamekubaliwa na Serikali, kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Marekebisho.

2.2.2 Mapendekezo ya Marekebisho ya Msingi

Mheshimiwa Spika, pamoja na kubaini dosari za kiuandishi, pia Kamati ilibaini baadhi ya ibara za Muswada kuwa na dosari zinazohitaji marekebisho ya msingi ili kuziwezesha Sheria hizi kuleta mantiki iliyokusudiwa na kurahisisha utekelezaji wake, kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Marekebisho. Hivyo, Kamati inapendekeza marekebisho yafanyike katika ibara hizo kama ifuatavyo:-

- a) **Ibara ya 5** chini Merekebisho ya Sheria ya Mawakili(Sura 341) pamoja na Ibara ya 44 katika Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura 268 zinazoweka zuij kwa Mawakili na Wanasheria katika Utumishi wa Umma kutoa huduma za uwakili wa kujitegemea, zifanyiwe marekebisho ili waruhusiwe kutoa huduma mbalimbali zisizohusisha Serikali kama vile huduma za viapo na uidhinishaji wa hati mbalimbali, kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Marekebisho.
- b) Marekebisho yanayopendekezwa chini **Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo, Sura 108,**

yameboreshwa na Kamati kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho chini ya Ibara ya 8 ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Msingi wa marekebisho haya umeainishwa katika Ibara ya 7 inayorekebisha Kif.cha 3 cha Sheria na Ibara ya 8 inayorekebisha Kif.cha 5 cha Sheria hii, ambapo, wigo wa mfumo wa usajili wa vizazi na vifo unapanuliwa na marekebisho ili kuiwezesha Serikali kusambaza rasilimali kwa wananchi kupitia Msajili Mkuu.

Hii ni pamoja na kuwatambua Watendaji wa Kata na Vijiji kama Wasajili wasaidizi baada ya kukasimwi mamlaka hayo na Msajili Mkuu, pamoja na kuweka utaratibu rasmi wa kufuata wakati wa kuasili Mtoto (*adoption*) na utaratibu wa kutoa hati ya usajili baada ya uasili wa Mtoto.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya yanamlenga Msajili Mkuu na Watendaji wa Vijiji na Mitaa pamoja na Watoto (walaji/ beneficiaries), ambapo taratibu zinazoainishwa katika marekebisho haya zitatekelezwa na Watendaji wa Kata na Vijiji kwa niaba ya Msajili Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhia mapendekezo haya kama yalivyo kwakuwa yanalenga kuboresha haki na ustawi wa Mtoto na yanazingatia Misingi ya Kimataifa ya haki za Mtoto chini ya ya *UN Convention on the Rights of a Child 1989*, ambayo Tanzania ni Mwanachama.

Aidha, Marekebisho haya yanalenga kuzingatia misingi ya kisheria iliyokwisha

ainishwa katika Sheria mbalimbali zinazohusu haki za Mtoto, kama vile Sheria ya Mtoto, Sura 13 (*The Law of The Child Act, 2009, (Sura 13)*), pamoja na Kanuni zake ambazo ni:-

- i) Kanuni za Uasili wa Mtoto za Mwaka 2012(GN.164),
 - ii) Kanuni za Malezi ya Kambo za Mwaka 2012(GN.165)
 - iii) Kanuni za Makao ya Watoto za Mwaka 2012(GN.166)
 - iv) Kanuni za Ajira za Watoto za Mwaka 2012(GN.168), na
 - v) Kanuni za Usalama wa Watoto za Mwaka 2012(GN.169).
- c) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inapendekeza marekebisho katika Ibara ya 16 kwenye Kifungu cha 194(A)(1) kuruhusu Ndugu au rafiki wa karibu wa Mtuhumiwa kuwepo wakati wa kufanya '*Plea Bargaining*' au '*Plea Agreement*', kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Marekebisho.

Aidha, Kamati inapendekeza marekebisho katika kifungu kippa cha 194C ili kuainisha sharti la kuwepo kibali cha maandishi kutoka kwa DPP kabla ya Wasaidizi wake kufanya '*Plea Agreement*'. Lengo la marekebisho haya ni kuzuia matumizi mabaya ya Mamlaka kwa waendesha Mashtaka nchini wakati wa utekelezaji wa sheria hii.

- d) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inapendekeza kuwa, Ibara ya 26 chini ya Sheria ya Taifa ya Mashitaka, Sura 430, ifanyiwe marekebisho

kwa kuainisha maafisa ambao DPP atakasimu mamlaka yake ya kutoa ridhaa katika ngazi ya Mikoa na Wilaya, kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya yanalenga kupunguza majalada ya mashauri ya kijinai ambayo yamekuwa kero ya muda mrefu kwa wananchi kwa sharti la kusubiri kibali cha DPP.

2.2.3 Mapendekezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini masuala mbalimbali ya jumla ambayo muhimu yakaboreshwa kwa lengo la kuleta ufanisi wa kutosha kwenye sekta husika kama ifuatavyo:-

a) Mheshimiwa Spika,

Kwa kuwa, Maelezo ya Serikali yameainisha kuwa, ipo nia njema ya kuweka zuio la Mawakili na Maafisa wa Sheria katika Utumishi wa Umma kutojihusisha na huduma za uwakili wa Kujitegemea, ikiwa ni pamoja na kuondoa mgongano wa maslahi binafsi kwa Mashauri ambayo yanahusu Serikali,

Na kwa kuwa, hatua ya Serikali kuboresha sharti hilo kwa kuwaruhusu Mawakili na Maafisa wa Sheria husika kutumia Mhuri wa Mwanasheria wa Serikali (*State Attorney*) kutoa huduma za viapo na huduma ndogo ndogo za kisheria zisizohusisha utetezi Mahakamani, hakuongozi chochote chenye tija kwa Wanataaluma hao ambao wametumia rasilimali nyingi ikiwemo muda hadi kufikia hatua hiyo muhimu na maalum katika Sekta ya Sheria,

Na kwa kuwa, hatua hiyo inapunguza kipato halali za kundi hilo la Wanataaluma na hata inaweza kuwapunguzia weledi kwa namna moja au nyingine,

Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali kuwa:-

- i) Mawakili na Maafisa wa Sheria ambao ni Watumishi wa Umma waanze kulipwa Posho ya kitaaluma yenye kuambatana na mishahara yao (*professional Allowance*) na kuwaboreshea mazingira yao ya kazi kwa ujumla, ili kuwaongezea motisha na kipato cha kumudu mahitaji ya familia zao, na
 - ii) Kuwepo mafunzo ya mara kwa mara ya ndani na nje ya nchi kwa Mawakili na Maafisa wa Sheria wa Serikali ili kuendelea kuwaongezea weledi kwa lengo la kuongeza ufanisi zaidi katika majukumu yao ndani ya Serikali.
- b) **Mheshimiwa Spika,**

Kwa kuwa, udhibiti wa masuala ya kijinai ni majukumu mtambuka pasipo kuathiri Mamlaka na Wajibu wa Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka, kwa mujibu wa Ibara ya 59(B)(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,1977,

Na kwa kuwa, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ni mdau muhimu kwa udhibiti wa makosa ya jinai yanayohusu Rushwa nchini,

Hivyo basi, Kamati inashauri kuwa, Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka ishirikiane kwa ukaribu na Ofisi za TAKUKURU katika ngazi ya

Wilaya na Mikoa yote nchini ili kupunguza mlundikano wa majalada kwa kurahisisha utoaji haki jinai kwa wakati, bila kuwanyanyasa watuhumiwa na bila kuathiri misingi ya Utawala Bora iliyowekwa kwa Mujibu wa Sheria za nchi kati ya Vyombo hivi pamoja na vyombo vingine husika.

c) **Mheshimiwa Spika,**

Kwa kuwa, pamoja na Kamati kuridhia marekebisho yanayopendekezwa Sehemu ya Tatu ya Muswada katika Sheria ya Vizazi na Vifo, Sura 108,

Na kwa kuwa, marekebisho haya yanalenga kusogeza huduma za usajili na uasili wa Mtoto hadi kwenye ngazi ya Kata na Vijiji,

Na kwa kuwa, utekelezaji wa marekebisho haya unahuishisha pia Sheria nyngine za nchi kama zilivyoainishwa katika taarifa hii,

Hivyo basi, Kamati inashauri kuwa, Serikali ijiandae kuwajengea uwezo Watendaji wote wa Kata na Vijiji nchini ili waweze kuwa na weledi wa kutosha katika kusimamia na kutekeleza majukumu haya mapya kwa ufanisi uliokusudiwa. Hii ni pamoja na kuwapatia rasilimali mbalimbali zitakazohitajika wakati wa kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Sheria hii.

3.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyngine naomba nikushukuru sana wewe kwa kutoa kibali ili kamati ya Katiba na Sheria iweze kuufanya kazi Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue na kuwashukuru wadau Mbalimbali waliofika na kutoa Maoni na Ushauri wao kwa Kamati ambao umesaidia kuboresha Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kumtambua na kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Prof. Adelardus Kilangi, Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Augustine P. Mahiga, (Mb), Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe.Dkt.Harrison Mwakyembe, (Mb) pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati ulioiwezesha Kamati kukamilisha Uchambuzi wa Muswada huu kwa wakati. Aidha, Kamati inatambua na kumshukuru kila Waziri na Watendaji wake waliofika mbele ya Kamati kwa lengo la kuisaidia Kamati kukamilisha kazi yake kwa ufanisi mkubwa na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa weledi na umahiri wao waliouonesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa Mapendekezo ya msingi ya kuboresha.
Naomba Majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu rasmi za Bunge (HANSARD).

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb- **Makamu/Mwenyekiti**
3. Mhe.Joseph Kizito Mhagama, Mb-Mjumbe;
4. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe;
5. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe;
6. Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb - Mjumbe;
7. Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb - Mjumbe;
8. Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mb - Mjumbe;
9. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb - Mjumbe;
10. Mhe. Nimrod Elirehemah Mkono, Mb - Mjumbe;
11. Mhe. Susan Peter Maselle, MB - Mjumbe;-
12. Mhe. Alfredina Apilinary Kahigi, Mb - Mjumbe;
13. Mhe. Latifah Hassan Chande,Mb - Mjumbe;

14. Mhe. Ally Abdulla Saleh, Mb - Mjumbe;
15. Mhe. Jacqueline Kandidus Ngonyani Msongozi, Mb - Mjumbe;
16. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe;
17. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda, Mb - Mjumbe;
18. Mhe. Hassan Seleman Kaunje, Mb - Mjumbe;
19. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe;
20. Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb - Mjumbe;
21. Mhe. Emmanuel A.Mwakasaka, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Dkt.Susan Alphonse Kolimba, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususan Katibu wa Bunge **Ndg. Stephen Kagaigai** kwa Uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaldizi Ndg. Gerald Magili, Mkurugenzi Msaidizi wa Kitengo cha Huduma za Kisheria Bungeni, Ndg. Leocardo Kapongwa, Mwanasheria wa Serikali Mkuu, Ndg. Prudens Rweyongeza, Wanasheria Wasaidizi wa Bunge, Ndg. Maria Mdulugu, Ndg. Fungo Matamus, Ndg. Thomas Shawa, Ndg. Evelyn R. Shibandiko, Ndg. Hawa Manzurya, Katibu wa Kamati Ndg. Stanslaus Kagisa, pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Rahel Masima waliofanikisha kazi ya Uchambuzi na uratibu wa shughuli za Kamati kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)



Mohamed Omary Mchengerwa, Mb
MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA
5 Septemba, 2019

MWENYEKITI: Ahsante. Umesoma vizuri sana Mbunge wa Rufiji, Tawire Mundu kwa hiyo sasa namuita Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhus Muswada wa Sheria ya marekebisho ya Sheria, Mheshimiwa Lathifah.

MHE. LATHIFAH H. CHANDE - (K.n.y MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA): Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (No. 4), ya Mwaka 2019, yaani *The Written Laws Miscelaneous Amendments (No.4) Act, 2019* yanatolewa chini ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili, kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (No.4), ya Mwaka 2019, unapendekeza marekebisho ya sheria mbalimbali 11. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Mawakili, (sura ya 341), Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo, (sura ya 108), Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, (Sura ya 20), Sheria ya Urejeshwaji wa Wahalifu, (Sura ya 368), Sheria ya Mashauri dhidi ya Serikali, (Sura ya 5), Sheria ya Mahakama za Mahakimu Wakazi (Sura ya 11), Sheria ya Taifa ya Mashitaka, (Sura ya 430), Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, (Sura ya 329), Sheria ya Mapato yatokanayo na Uhali, (Sura ya 256), Sheria ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, (Sura ya 268) na Sheria ya Chama cha Msalaba Mwekundu, (Sura ya 66).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa marekebisho yanayopendekezwa yanahu Sheria nyingi ambazo zina athari za moja kwa moja kwa wananchi.

Kutokana na Sheria hizo kugusa maisha na shughuli za wananchi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitegemea kuwa Serikali ingewashirikisha kwa utoshelevu wadau wote ambao wanaguswa na marekebisho ya Sheria hizo ili watoe maoni yao na hatimaye Bunge liweze kutunga Sheria bora ambayo ni rafiki kwa wadau wote na hivyo kurahisisha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na mategemeo hayo, ushiriki wa wadau ulikuwa duni jambo ambalo mosi, linatoa picha kuwa hakuna nia njema katika marekebisho yanyopendekezwa, lakini pili utekelezaji wa sheria ambayo haina maridhiano kwa wadau wote utakuwa mgumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na upungufu huo wa ushiriki hafifu wa wadau ambao matokeo yake ni kutungwa kwa Sheria ambayo itaanza kupingwa hata kabla ya kuanza kutekelezwa na hivyo kusababisha kuleta Muswada mwagine wa marekebisho ndani ya muda mfupi jambo ambalo ni hasara kwa Serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kwamba, Serikali itanue wigo wa ushiriki wa wadau ili sheria inayotungwa ipokelewe na kutekelezwa vyema na wananchi wanaoguswa na sheria hiyo yaani *compliance* na hivyo kupunguza gharama za kufanya marekebisho ya Sheria mara kwa mara kutokana na Sheria husika kuwa na mapungufu mengi yanayotokana na ukosefu wa mawanda mapana wa maoni ya wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, ufuatao ni uchambuzi wa baadhi ya vifungu vinavyopendekezwa kufanyiwa marekebisho na maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu mapendeleko hayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekebisho ya Sheria ya Mawakili, (Sura ya 341); kifungu cha 39 cha sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipycha cha "(2) kinachosomeka kama ifuatavyo: "A law Officer or State

Attorney shall not, for the whole period of service as a Law Officer or State Attorney be issued with a practicing certificate".

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinatoa zio kwa Mawakili wa Serikali kupewa hati au kibali cha kufanya shughuli za uwakili nje ya mfumo wa Serikali kwa kipindi chote watachokuwa katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinawabana mawakili wa Serikali wasiweze kufanya shughuli zozote za uwakili nje ya ajira ya Serikali kwa lengo la kujiongeza kipato. Kwa mantiki hiyo, licha pendekezo hilo kuwaathiri kiuchumi, lakini pia linawaondolea motisha ya kufanya kazi bila msongo wa mawazo yaani *stress unaotokana na ugumu wa maisha*. Aldha, pendekezo hilli linapoka haki ya wananchi kupata msaada wa kisheria kutoka kwa mawakili wa Serikali kama vile viapo, kushuhudia mikataba na makubaliano n.k.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kuwa taaluma ya Sheria ni taaluma kama zilivyo taaluma nyingine, na kwa sababu hiyo, mawakili wa Serikali wana haki ya kufanya shughuli binafsi za kiwakili baada ya muda wa kazi kama ambavyo waajiriwa wengine wa Serikali wanavyoruhusiwa kufanya shughuli binafsi zinazohusiana na taaluma zao baada ya muda wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuikumbusha Serikali kuzingatia kaulimbiu yake ya "Hapa Kazi Tu" na pia msisitizo wake kwa Wananchi kujiajiri na kujipatia kipato ili kuondokana na umaskini kwa kuwaruhusu mawakili wa Serikali kufanya shughuli binafsi za uwakili ili kutimiza azma hiyo. Hapa tunasisitiza kuwa muda wa mwanataaluma yoyote kujiajiri ni wakati akiwa na nguvu ya kufanya kazi. Kuwazuia mawakili kufanya kazi hizo kwa kipindi chote cha ajira yao ni kuwadhulamu kwa kuwa hawataweza kufanya shughuli hizo kwa ufanisi baada ya kustaafu ajira ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu iliyotolewa kuhalilisha pendeleko la kuwazuia mawakili wa Serikali kufanya kazi ya uwakili wa kujitegemea ni pamoja na kuondoa mgongano wa maslahi ikiwa Wakili huyo atakuwa anamwakilisha mtu mwenye shauri dhidi ya Serikali ilhali Wakili huyo ni mwajiriwa wa Serikali. Hoja inaweza kuwa na pande mbili; ukweli na uongo, kwani yapo matukio kadhaa ambapo imeshuhudiwa maslahi binafsi yakipewa kipaumbele hasa katika teuzi mbalimbali. Kwa mfano wapo Mawakili binafsi waliowahi kuteuliwa kuwa Majaji wa Mahakama Kuu au kuwa watendaji wakuu katika Ofisi na Idara za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inapenda kufahamisha Serikali kwamba siyo mara zote Mawakili wa Serikali watakuwa wanafanyakazi wa kuitetea Serikali tu. Kwa sababu hiyo, Mawakili wa Serikali waruhusiwe kufanya uwakili wa kujitegemea ilimradi katika utekelezaji wa shughuli hiyo kusiwe na maslahi ya Serikali. Hivyo, ni vyema kazi ambazo hazina uhusiano na kuitetea Serikali wakaruhusiwa kuzifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kinachokwenda kutokea ikiwa kifungu hiki cha kibaguzi hakitafutwa, kazi ya Uwakili wa Serikali itakosa mvuto kwa wanataluma wa Sheria kutokana na maslahi duni jambo ambalo linaweza kusababisha upungufu wa Mawakili wa Serikali au Serikali kuwa na Mawakili wasio na sifa stahiki yaani *competent lawyers* na hivyo kupelekea Serikali kushindwa katika mashauri mengi dhidi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai (Sura ya 20); dhana ya makubaliano baina ya mwendesha mashitaka na mtuhumiwa wa kosa la jinai kukiri kosa ili kupunguziwa adhabu yaani *Plea Bargaining* ni nzuri kwa ujumla wake kutokana na sababu zilizo wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha cha 16 cha Muswada kinachoanzisha kifungu kipywa cha 194(f) kimeorodhesha makosa ambayo hayatahusika na utaratibu

wa makubaliano ya kupunguziwa na kufutiwa adhabu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina inapendekeza kwamba; makosa yaliyoainishwa katika kifungu cha 194F(b),(c),(d) na (e) ambayo yanahu su uhaini, umiliki na ufanyaji wa biashara ya dawa za kulevyta, ugaidi na umiliki wa nyara za Serikali kinyume na Sheria yaingizwe katika utaratibu wa *Plea Bargaining*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa mapendekezo haya ni kutokana na ukweli kwamba makosa tajwa katika vifungu hivyo yanahu su mtandao hatari, hivyo ni muhimu sana kuufahamu mtandao husika kupitia kwa Mtuhumiwa. Kama mtuhumiwa asipoingizwa kwenye makubaliano na Mwendesha mashtaka au na Wakili wake kuna uwezekano mkubwa walioko nje wakaendelea na uhalifu mbaya zaidi. Kwa mfano, kama unataka kufahamu wale wanaoleta madawa ya kulevyta, unatakiwa uingle makubaliano na wanaotumia ili kujua wanauziwa na nani ili kuubaini mtandao mzima unaojishughulisha na dawa za kulevyta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika ili kutokomeza ugaidi ni lazima kushughulika na mtando mzima na sio mtuhumiwa mmoja. Ni vigumu kuvunja kambi au makundi ya siri yaliyo kimya yaani *sleeping cells* au hata kama kuna uhaini hautaweza kufika mwisho wa mzizi, kama hapatakuwa na watu wa kutoa taarifa kwa njia hii ya *Plea Bargaining*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Serikali kuyaondoa makosa yanayohusisha mtandao hatari kama vile uhaini, ugaidi na biashara ya dawa za kulevyta katika orodha ya makosa yanayoweza kushughulikiwa kwa makubaliano kati ya mtuhumiwa na mwendesha mashtaka ni sawa na Serikali kujifunga na kujizuia kubaini wahalifu wa mitandao hatari na kuwachukulia hatua ili kukomesha kabisa makosa ya aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekebisho ya Sheria ya Mashauri dhidi ya Serikali, (Sura ya 5); Sheria hii ni muhimu sana katika dhana ya haki na usawa mbele ya sheria. Aidha,

ni muhimu Wananchi wakafahamu kwamba Serikali inaweza kushtakiwa iwapo itakiuka misingi ya utawala bora na utoaji wa haki katika utekelezaji wa shughuli zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 22 cha kinachoanzisha kifungu kipywa cha 6A ambacho kinampa mamlaka Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia kati shauri lolote liliofunguliwa na Serikali au dhidi ya Serikali kwa Wizara, Idara au Taasisi yoyote ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba kifungu hiki kinaondoa dhana ya uwajibikaji wa viongozi na watendaji wa umma kwa makosa watakayoyatenda kwa kuwa wanajua Mwanasheria Mkuu wa Serikali atasimama badala yao. Kwa kuwa idara na Taasisi za Serikali zimepewa mamlaka kamili kwa mujibu wa Sheria ya kushtaki na kushtakiwa; zinatakiwa kutumia mamlaka hayo vilevile kuwajibika pale zinapokabiliwa na mashitaka ili kujenga dhana ya uwajibikaji, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kwamba ikiwa watendaji waliopewa dhamana katika ofisi za umma watafanya mambo ambayo ni kinyume cha Sheria na wakawajibika wao binafsi bila kuhusishwa kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuleta nidhamu katika utendaji wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Taasisi za umma kujificha kwenye kivuli cha mwanasheria Mkuu wa Serikali kunapotokea mashauri dhidi ya Taasisi hizo kinatoa taswira kwamba Wanasheria katika Taasisi hizo dhaiju hawawezi kusimama na kutetea Taasisi zinapokabiliwa na mashauri ya Kisheria. Kama Serikali itang'ang'ania Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia mashauri ya Kisheria katika idara na Taasisi za umma, basi Wanasheria walioajiriwa katika Taasisi hizo wafutwe kazi au wabadilishiwe majukumu kwa kuwa watakuwa wanalipwa mishahara kwa madaraka ambayo hawayafanyii kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie; Kama Serikali itang'ang'ania Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia

mashauri ya Kisheria katika idara na Taasisi za umma, basi Wanasheria walioajiriwa katika Taasisi hizo wafutwe kazi au wabadilishiwe majukumu kwa kuwa watakuwa wanalipwa mishahara kwa madaraka ambayo hawayafanyii kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa; marekebisho kama yanavyoelekezwa kwenye kifungu cha 29 cha Muswada kwa kuongeza kifungu kidogo kipy cha 2 kinachohitaji utoaji wa idhini au kibali toka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mashauri ya rushwa ambayo hayahusiani na makosa yaliyoelezwa katika kifungu cha 15 cha Sheria Mama ya TAKUKURU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba; kitendo cha TAKUKURU kutokuwa na mamlaka ya kupeleka Mahakamani mashtaka ya rushwa kubwa kadiri ya mapendekezo yanayotolewa na Serikali kinatoa picha kwamba, Taasisi hiyo ya kiuchunguzi haiaminiki katika utendaji wake na ndio maana inakuwa ni Taasisi ya kupewa maelekezo ya nini cha kufanya na wakati gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kifungu cha 9 cha sheria ya Taifa ya mashtaka kinachofafanua aina ya mashtaka ambayo DPP anatakiwa kupewa taarifa au kushirikishwa, ni dhahiri kuwa TAKUKURU itabakia kuwa Taasisi isiyokuwa na meno. Kambi Rasmi ya Upinzani inashangazwa sana na mapendekezo haya kwani yanatoa taswira kwamba TAKUKURU haina uwezo kiutendaji wa kuweza kuwafungulia mashtaka watuhumiwa wa makosa ya rushwa mpaka ipate kibali cha Mwendesha Mashtaka wa Serikali. Aidha, mapendekezo hayo yanakwenda kinyume na bango linalobebwa na Serikali ya Awamu ya Tano kuwa inapambana na Rushwa ilihali inaidhibiti TAKUKURU kufanya kazi kwa uhuru kwa kupoka madaraka yake na kuyahamishia kwa mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali; kama kweli inataka kupambana na rushwa kwa vitendo basi ilete Muswada wa Sheria utakaoifanya TAKUKURU kuwa Taasisi huru. Kifungu hiki kinachopendekezwa katika Muswada huu kinainyima TAKUKURU uhuru wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 9 cha Sheria ya Taifa ya Mashitaka kinaonyesha jinsi ambavyo TAKUKURU imepokwa mamlaka ya kushughulikia Mafisadi na wala rushwa. Kifungu hiki kitasomeka katika ukurasa wa 12 na 13 ambapo naomba sitokisoma lakini naomba kiingizwe katika Hansard.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha kutoipa TAKUKURU uhuru wa kujitegemea kimamlaka kitasababisha mwendelezo wa vitendo vya rushwa, kwani makosa yote ya rushwa kubwa kubwa yataishia ofisini kwa DPPna TAKUKURU haitakuwa na uwezo au mamlaka ya kuhoji chochote kuhusu mwenendo wa mashauri hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hofu ya Serikali ni kupoteza au kupunguza madaraka ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kwamba Serikali ifanye utafiti katika nchi nyingine kuona ni namna gani Ofisi za Waendesha Mashtaka wa nchi hizo wanafanya kazi zao bila kuathiri mamlaka nyingine zenye majukumu ya usimamizi wa utekelezaji wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya Sheria ya Mapato yatokanayo na uhalifu, Sura ya 256. Kifungu cha 37 cha Muswada kinafanya marekebisho kifungu cha 22 cha sheria mama kwa kufuta kifungu cha 4 na kukiandika upya kifungu hicho kinachohusu adhabu ya makosa ambayo yanakiuka vifungu vya sheria yoyote ya ndani au nje ya nchi na adhabu zake ni kifo au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi kumi na mbili na pia utaifishaji mali iliyopatikana kutokana na makosa hayo. Kwa muktadha huo, kifungu cha 4(c) kinasema kuwa, pale maombi ya adhabu yanapotolewa

dhidi ya mtuhumiwa wa makosa tajwa (*serious offence*), mali ya mtuhumiwa kukamatwa, itahusu pia mali ambayo alikuwa anamiliki miaka mitano nyuma kabla ya pale kosa alilohukumiwa nalo halijatendeka. Naomba nirudie, kifungu cha 4(c) kinasema kuwa pale maombi ya adhabu yanapotolewa dhidi ya mtuhumiwa wa makosa tajwa (*serious offence*), mali ya mtuhumiwa kukamatwa, itahusu pia mali ambayo alikuwa anamiliki miaka mitano nyuma kabla ya pale kosa alilohukumiwa nalo halijatendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kifungu hiki kina nia ovu ya kuwalenga baadhi ya watu hususan wenyewe mtazamo tofauti na Serikali ili kuwabambikizia kesi za uhujumu uchumi na kuafilisi kwa kutaifisha mali zao kabla hata kesi hizo kutolewa uamuzi na Mahakama. Ukitazama kwa makini mapendekezo ya Serikali utagundua pia kwamba Serikali inataka kuijwekea kinga ya kisheria ya kutokulipa madeni makubwa inayodaiwa na watu na pia kuwahujumu watu wenyewe mgogoro na Serikali kwa kuwa itakuwa ni rahisi kwa Serikali kuwageuzia kibao watu wenyewe mgogoro nao au wenyewe madai dhidi yake na kuafilisi mali zao kupitia sheria hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kushangaza zaidi ni pale Serikali inapopendekeza kutaifisha mali halali iliyopatikana kwa kipindi cha miaka mitano nyuma kabla ya kosa halijatendeka. Jambo hili halikubaliki kwa kuwa litaathiri familia nzima ilhali aliyetenda kosa ni mmoja. Kama ilivyo desturi, mali za familia huchuma pamoja kwa maana ya mke na mume au ndugu wa familia, hivyo kama ni mtu mmoja ametenda kosa inahalalisha vipi ufilisi wa mali ambazo ni za familia? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maelezo ni kwa namna gani itatenganisha mali binafsi za mtenda kosa na mali za familia ili kutoquingiza familia nzima kwenye adhabu kwa kosa la mtu mmoja. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kifungu chote cha 4 kifutwe kabisa, ni kifungu ambacho badala ya kuangalia ustawi wa nchi yetu

kinalenga kuwavizia watu wenyewe mtazamo tofauti na Serikali na kuwa filisi mali zao na pia kitapunguza morali ya wawekezaji hapa nchini kwa kuwa na hofu ya kuflisiwa kutokana na hila za kisiasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya Sheria ya Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania, Sura ya 66. Lengo la marekebisho haya ni kutaka kuifanya sheria hii kutumika katika pande zote mbili za Muungano na vilevile kuongeza mawanda ya nembo ya msalaba mwekundu kuwa pia ni mwezi mwekundu. Hata hivyo, uko mkanganyiko kuhusu matumizi ya sheria hii kwa kuwa sheria itatumika pande zote mbili za Muungano lakini Waziri anayepewa dhamana ya kusimamia sheria hii ni Waziri wa Katiba na Sheria, Wizara ambayo siyo ya Muungano. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza Waziri atakayekuwa na dhamana na sheria hii awe Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo ni Wizara ya Muungano na siyo Waziri wa Sheria kama Muswada unavyopendekeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Napenda kumalizia hotuba yangu kwa kuiasa Serikali kwamba utunzi wa sheria unalenga kuweka utaratibu wa uendeshaji wa mambo katika jamii. Ili utaratibu huo uweze kufanya kazi, ni lazima uwe unafahamika na unakubalika na jamii nzima. Kwa sababu hiyo, ipo haja kubwa kuishirikisha jamii katika mchakato mzima wa utunzi wa sheria ili jamii iweze kuziheshimu sheria hizo ili ziweze kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na dhana hiyo ya ushiriki mpana wa wananchi katika utunzi wa sheria, kumekuwa na desturi mbaya ya Serikali kuwaita wadau wachache kuchambua Miswada huku idadi kubwa ya wananchi ambayo ndiyo walengwa wa sheria husika wakiwa hawajui chochote kuhusu sheria hizo. Kwa kutambua upungufu huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kupitia CHADEMA imeweka bayana katika Sera yake ya Utawala Bora, Sura ya 2.1 kuhusu ushirikishwaji wa wananchi katika kutunga sharia. Sehemu ya sera hiyo inasema kwamba,

naomba kunukuu: "CHADEMA itawashirikisha wananchi kutoa maoni na mapendekezo katika mchakato wa kutunga sheria zote za nchi ili kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa sheria hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofi/Vigelegele*)

**MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU
MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA
MBALIMBALI (NA. 4) YA MWAKA 2019 [*THE WRITTEN LAWS
(MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 4) ACT, 2019 KAMA
YALIVVOWASILISHWA MEZANI***

(Yanatolewa chini ya kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la Januari 2016)

A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, Kwa heshima kubwa napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu,kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili, kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya sheria mbalimbali.
2. **Mheshimiwa Spika**, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (No. 4), ya Mwaka 2019, unapendekeza marekebisho ya sheria mbalimbali kumi na moja (11). Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Mawakili, (Sura ya 341), Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo, (Sura 108), Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai,(Sura ya 20), Sheria ya Urejeshwaji wa Wahalifu, (Sura ya 368), Sheria ya Mashauri dhidi ya Serikali,(Sura ya 5), Sheria ya Mahakama za Mahakimu Wakazi (Sura ya 11), Sheria ya Taifa ya Mashitaka, (Sura ya 430), Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, (Sura ya 329), Sheria ya

Mapato yatokanayo na Uhalifu, (Sura ya 256), Sheria ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, (Sura ya 268) na Sheria ya Chama cha Msalaba Mwekundu, (Sura ya 66).

3. **Mheshimiwa Spika**, ni ukweli usiopingika kuwa marekebisho yanayopendekezwa yanahu sheria nydingi, ambazo zina athari za moja kwa moja kwa wananchi. Kutokana na Sheria hizo kugusa maisha na shughuli za wananchi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitegemea kuwa Serikali ingewashirikisha kwa utoshelevu wadau wote ambao wanaguswa na marekebisho ya sheria hizo ili watotoe maoni yao na hatimae Bunge liweze kutunga sheria bora ambayo ni rafiki kwa wadau wote na hivyo kurahisisha utekelezaji wake.
4. **Mheshimiwa Spika**, tofauti na mategemo hayo; ushiriki wa wadau ulikuwa duni jambo ambalo mosi, linatoa picha kuwa hakuna nia njema katika marekebisho yanyopendekezwa; lakini pili utekelezaji wa sheria ambayo haina maridhiano kwa wadau wote utakuwa mgumu.
5. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na upungufu huo wa ushiriki hafifu wa wadau ambao matokeo yake ni kutungwa kwa sheria ambayo itaanza kipingwa hata kabla ya kuanza kutekelezwa na hivyo kusababisha kuleta muswada mwagine wa marekebisho ndani ya muda mfupi jambo ambalo ni hasara kwa Serikali; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kwamba; Serikali itanue wigo wa ushiriki wa wadau ili sheria inayotungwa ipokelewe na kutekelezwa vyema na wananchi wanaoguswa na sheria hiyo (compliance) na hivyo kupunguza gharama za kufanya marekebisho ya sheria mara kwa mara kutokana na sheria husika kuwa na mapungufu mengi yanayotokana na ukosefu wa mawanda mapana wa maoni ya wadau.

6. **Mheshimiwa Spika**, baada ya utangulizi huo, ufuatao ni uchambuzi wa baadhi ya vifungu vinavyopendekezwa kufanyiwa marekebisho na maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu mapendekezo hayo.

B. UCHAMBUZI WA VIFUNGU VYA MUSWADA

- i. **Marekebisho ya Sheria ya Mawakili,**
(Sura ya 341)
7. **Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 39 cha sheria mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipywa cha "(2) kinachosomeka kama ifuatavyo: "*A law Officer or State Attorney shall not, for the whole period of service as a Law Officer or State Attorney be issued with a practicing certificate*".
8. **Mheshimiwa Spika**, kifungu hiki kinatoa zuijio kwa mawakili wa Serikali kupewa hati au kibali cha kufanya shughuli za uwakili nje ya mfumo wa Serikali kwa kipindi chote watachokuwa katika utumishi wa umma.
9. **Mheshimiwa Spika**, kifungu hiki kinawabana mawakili wa Serikali wasiweze kufanya shughuli zozote za uwakili nje ya ajira ya Serikali kwa lengo la kujiongezea kipato. Kwa mantiki hiyo, licha pendekezo hilo kuwaathiri kiuchumi, lakini pia linawaondolea motisha wa kufanya kazi bila msongo wa mawazo (stress) unaotokana na ugumu wa maisha. Aidha, pendekezo hili linapoka haki ya wananchi kupata msaada wa kisheria kutoka kwa mawakili wa Serikali kama vile viapo, kushuhudia mikataba na makubaliano nk.
10. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kuwa taaluma ya sheria ni taaluma kama zilivyo taaluma nyingine, na kwa sababu hiyo, mawakili wa Serikali wana haki ya kufanya shughuli

binafsi za kiwakili baada ya muda wa kazi kama ambavyo waajiriwa wengine wa Serikali wanavyoruhusiwa kufanya shughuli binafsi zinazohusiana na taaluma zao baada ya muda wa kazi.

11. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuikumbusha Serikali kuzingatia kaulimbiu yake ya "Hapa Kazi Tu" na pia msisitizo wake kwa wananchi kujijiri na kujipatia kipato ili kuondokana na umaskini kwa kuwaruhusu mawakili wa Serikali kufanya shughuli binafsi za uwakili ili kutimiza azma hiyo. Hapa tunasisitiza kuwa muda wa mwanataaluma yoyote kujijiri ni wakati akiwa na nguvu ya kufanya kazi. Kuwazuia mawakili kufanya kazi hizo kwa kipindi chote cha ajira yao ni kuwadhulumu kwa kuwa hawataweza kufanya shughuli hizo kwa ufanisi baada ya kustaafu ajira ya Serikali.
12. **Mheshimiwa Spika**, sababu iliyotolewa kuhalilisha pendekezo la kuwazuia mawakili wa Serikali kufanya kazi ya uwakili wa kujitegemea ni pamoja na kuondoa mgongano wa maslahi ikiwa wakili huyo atakuwa anamwakilisha mtu mwenye shauri dhidi ya Serikali ilhali wakili huyo ni mwajiriwa wa Serikali. Hoja inaweza kuwa na pande mbili; ukweli na uongo, kwani yapo matukio kadhaa ambapo imeshuhudiwa maslahi binafsi yakipewa kipaumbele hasa katika teuzi mbalimbali. Kwa mfano wapo mawakili binafsi waliowahi kuteuliwa kuwa majaji wa Mahakama Kuu; au kuwa watendaji wakuu katika Ofisi na Idara za Serikali.
13. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inapenda kufahamisha Serikali kwamba; sio mara zote mawakili wa Serikali watakuwa wanafanyakazi wa kuitetea serikali tu. Kwa sababu hiyo, mawakili wa Serikali waruhusiwe kufanya uwakili wa kujitegemea ilimradi katika utekelezaji wa shughuli hiyo kusiwe na maslahi ya Serikali. Hivyo, ni vyema

kazi ambazo hazina uhusiano na kuitetea Serikali wakaruhusiwa kuzifanya.

- 14. Mheshimiwa Spika**, Kinachokwenda kutokea ikiwa kifungu hiki cha kibaguzi hakitafutwa; kazi ya Uwakili wa Serikali itakosa mvuto kwa wanataaluma wa Sheria kutokana na maslahi duni; jambo ambalo linaweza kusababisha upungufu wa mawakili wa Serikali au Serikali kuwa na mawakili wasio na sifa stahiki (competent lawyers) na hivyo kupelekeea Serikali kushindwa katika mashauri mengi dhidi yake.

ii. **Marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai (Sura ya 20)**

- 15. Mheshimiwa Spika**, dhana ya makubaliano balna ya mwendesha mashitaka na mtuhumiwa wa kosa la jinai kukiri kosa ili kupunguziwa adhabu (*Plea Bargaining*) ni nzuri kwa ujumla wake kutokana na sababu zilizo wazi.
- 16. Mheshimiwa Spika**, kifungu cha cha 16 cha Muswada kinachoanzisha kifungu kipycha cha 194F Kimeorodhesha makosa ambayo hayatahusika na utaratibu wa makubaliano ya kupunguziwa au kufutiwa adhabu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina inapendekeza kwamba; makosa yaliyoainishwa katika kifungu cha 194F (b),(c),(d) na (e) ambayo yanahu uhaiini, umiliki na ufanyaji wa biashara ya dawa za kulevyta, ugaidi na umiliki wa nyara za Serikali kinyume cha Sheria yaingizwe katika utaratibu wa ***Plea Burgaining***.
- 17. Mheshimiwa Spika**, msingi wa pendekezo hili ni kutokana na ukweli kwamba makosa tajwa katika vifungu hivyo yanahu mtandao hatari, hivyo ni muhimu sana kuufahamu mtandao husika kuitia kwa Mtuhumiwa. Kama mtuhumiwa asipoingizwa kwenye makubaliano na Mwendesha mashtaka au na wakili wake kuna uwezekano mkubwa walioko

nje wakaendelea na uhalifu mbaya zaidi. Kwa mfano, kama unataka kufahamu wale wanaoleta madawa ya kulevyta, unatakiwa uingie makubaliano na wanaotumia ili kujua wanauziwa na nani ili kuubaini mtandao mzima unaojishughulisha na dawa za kulevyta.

18. Mheshimiwa Spika, halikadhalika ili kutokomeza ugaidi ni lazima kushughulika na mtando mzima na sio mtuhumiwa mmoja. Ni vigumu kuvunja kambi au makundi ya siri yaliyo kimya (sleeping cells) au hata kama kuna uhaini hautaweza kufika mwisho wa mzizi, kama hapatakuwa na watu wa kutoa taarifa kwa njia hii ya *Plea Bargaining*.

19. Mheshimiwa Spika kitendo cha Serikali kuyaondoa makosa yanayohusisha mtandao hatari kama vile uhaini, ugaidi na biashara ya dawa za kulevyta katika orodha ya makosa yanayoweza kushughulikiwa kwa makubaliano katika ya mtuhumiwa na mwendesha mashtaka ni sawa na Serikali kujifunga na kujizuia kubaini wahalifu wa mitandao hatari na kuwachukulia hatua ili kukomesha kabisa makosa ya aina hiyo.

iii. Marekebisho ya Sheria ya Mashauri dhidi ya Serikali, (Sura ya 5)

20. Mheshimiwa Spika, Sheria hii ni muhimu sana katika dhana ya haki na usawa mbele ya sheria. Aidha, ni muhimu wananchi wakafahamu kwamba Serikali inaweza kushtakiwa iwapo itakiuka misingi ya utawala bora na utowaji wa haki katika utekelezaji wa shughuli zake.

21. Mheshimiwa Spika kifungu cha 22 cha kinaanzisha kifungu kipyta cha 6A ambacho kinampa mamlaka Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia kati shauri lolote lililofunguliwa na Serikali au dhidi ya Serikali kwa wizara, idara au taasisi yoyote ya umma.

22. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba kifungu hiki kinaondoa dhana ya uwajibikaji wa viongozi na watendaji wa umma kwa makosa watakayoyatenda kwa kuwa wanajua Mwanasheria Mkuu wa Serikali atasimama badala yao. Kwa kuwa idara na taasisi za Serikali zimepewa mamlaka kamili kwa mujibu wa sheria ya kushtaki na kushtakiwa; zinatakiwa kutumia mamlaka hayo vile vile kuwajibika pale zinapokabiliwa na mashitaka. Ili kujenga dhana ya uwajibikaji, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kwamba ikiwa watendaji waliopewa dhamana katika ofisi za umma watafanya mambo ambayo ni kinyume cha sheria na wakawajibika wao binafsi bila kuhuishwa kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuleta nidhamu katika utendaji wa umma.

23. **Mheshimiwa Spika**, kitendo cha taasisi za umma kujificha kwenye kivuli cha mwanasheria Mkuu wa Serikali kunapotokea mashauri dhidi ya taasisi hizo kinatoa taswira kwamba wanasheria katika taasisi hizo dhaifu hawawezi kusimama na kutetea taasisi zinapokabiliwa na mashauri ya kisheria. Kama Serikali itang'ang'ania Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia mashauri ya kisheria katika idara na taasisi za umma; basi wanasheria walioajiriwa katika taasisi hizo wafutwe kazi au wabadilishiwe majukumu kwa kuwa watakuwa wanalipwa mishahara kwa madaraka ambayo hawayafanyii kazi.

iv. **Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, (Sura ya 329)**

24. **Mheshimiwa Spika**, marekebisho kama yanavyoelekezwa kwenye kifungu cha 29 cha muswada, kwa kuongeza kifungu kidogo kipyaa cha 2 kinachohitaji utoaji wa idhini au kibali toka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mashauri ya rushwa ambayo hayahusiani na makosa yaliyoelezwa katika kifungu cha 15 cha sheria mama ya TAKUKURU.

25. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba; kitendo cha TAKUKURU kutokuwa na mamlaka ya kupeleka mahakamani mashtaka ya rushwa kubwa kadiri ya mapendekezo yanayoletwa na Serikali kinatoa picha kwamba, taasisi hiyo ya kiuchunguzi haiaminiki katika utendaji wake na ndio maana inakuwa ni taasisi ya kupewa maelekezo ya nini cha kufanya na wakati gani.
26. **Mheshimiwa Spika**, Ukiangalia kifungu cha 9 cha sheria ya Taifa ya Mashtaka kinachofafanua aina ya mashtaka ambayo DPP anatakiwa kupewa taarifa au kushirikishwa, ni dhahiri kuwa TAKUKURU itabakia kuwa taasisi isiyokuwa na meno. Kambi Rasmi ya Upinzani inashangazwa sana na mapendekezo haya kwani yanatoa taswira kwamba TAKUKURU haina uwezo kiutendaji wa kuweza kuwafungulia mashtaka watuhumiwa wa makosa ya rushwa mpaka ipate kibali cha Mwendesha Mashtaka wa Serikali. Aidha, mapendekezo hayo yanakwenda kinyume na bango linalobebwa na Serikali ya Awamu ya Tano kuwa inapambana na Rushwa ilhalii inaidhibiti TAKUKURU kufanya kazi kwa uhuru kwa kupoka madaraka yake na kuyahamishia kwa mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali.
27. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali; kama kweli inataka kupambana na rushwa kwa vitendo; basi ilete muswada wa sheria utakaoifanya TAKUKURU kuwa taasisi huru. Kifungu hiki kinachopendekezwa katika muswada huu kinainyima TAKUKURU uhuru wa kufanya kazi.
28. **Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 9 cha Sheria ya Taifa ya Mashitaka kinaonyesha jinsi ambavyo TAKUKURU imepokwa mamlaka ya kushughulikia mafisadi na wala rushwa. Kifungu hicho kinasomeka kama ifuatavyo; naomba kunukuu:-

9.-(1) Notwithstanding the provisions of any other law, the functions of Director shall be to-

(a) decide to prosecute or not to prosecute in relation to an offence;

(b) institute, conduct and control prosecutions for any offence other than a court martial;

(c) take over and continue prosecution of any criminal case instituted by another person or authority;

(d) discontinue at any stage before judgement is delivered any criminal proceeding brought to the court by another person or authority; and

(e) direct the police and other investigative organs to investigate any information of a criminal nature and to report expeditiously.

(2) The functions referred to in sub-section (1) shall include institution conducting of summary proceedings, committal proceedings or a preliminary hearing under the Criminal Procedure Act, the Magistrates' Courts Act or any other law relating to criminal proceedings.

(3) Nothing in this section shall prevent the Director to take over and continue proceedings in the name of the person or authority that instituted those proceedings.

(4) The Police Officer or the Officer of any other investigative organ in-charge of any area or authority to be specified by the Director shall, in respect of offences alleged to have been committed within that area, report to the Director any-

- (a) offence punishable with death;
- (b) offence in respect of which a prosecution is by law required to be instituted with the consent of the Director;
- (c) case in which a request for information is made by the Director;
- (d) case in which it appears to such Police Officer or the Officer of any other investigative organ that the advice or assistance of the Director is desirable; or
- (e) other offence specified by the Director to be an offence in respect of which a report under this section is necessary.

(5) The term "area" or "authority" as used in subsection (4) means and includes a geographical jurisdiction of a police post, station, district, region or zone, a corresponding office of any other investigative organ or a person to whom a command or a directive may be issued as the case may be.

29. **Mheshimiwa Spika**, kitendo cha kutoipa TAKUKURU uhuru wa kujitegemea kimamlaka kitasababisha mwendelezo wa vitendo vyatrushwa, kwani makosa yote ya rushwa kubwakubwa yataishia ofisini kwa DPP na TAKUKURU haitakuwa na uwezo/ mamlaka ya kuhoji chochote kuhusu mwenendo wa mashauri hayo.
30. **Mheshimiwa Spika** kama hofu ya Serikali ni kupoteza au kupunguza madaraka ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kwamba, Serikali ifanye utafiti katika nchi nyingine kuona ni namna gani Ofisi za Waendesha Mashtaka wa nchi hizo wanafanya

kazi zao bila kuathiri mamlaka nyingine zenye majukumu ya usimamizi wa utekelezaji wa sheria.

v. *Marekebisho ya sheria ya Mapato yatokanayo na Uhali, sura ya 256*

31. **Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 37 cha muswada kinafanya marekebisheso kifungu cha 22 cha sheria mama, kwa kufuta kifungu cha 4 na kukiandika upya. Kifungu hicho kinachohusu adhabu kwa makosa ambayo yanakiuka vifungu nya sheria yoyote ya ndani au nje ya nchi na adhabu zake ni kifo au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi kumi na mbili; na pia utaifishaji mali iliyopatikana kutokana na makosa hayo. Kwa muktadha huo, kifungu cha 4(c) kinasema kuwa pale maombi ya adhabu yanapotolewa dhidi ya mtuhumiwa wa makosa tajwa "*serious offense*", mali ya mtuhumiwa kukamatwa, itahusu pia mali ambayo alikuwa anamiliki miaka mitano nyuma kabla ya pale kosa alilohukumiwa nalo halijatendeka.
32. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kifungu hiki kina nia ovu ya kuwalenga baadhi ya watu hususan wenyewe mtazamo tofauti na Serikali ili kuwabambikizia kesi za uhujumu uchumi na kuafilisi kwa kutaifisha mali zao kabla hata ya kesi hizo kutolewa uamuza na mahakama.
33. **Mheshimiwa Spika**, ukitazama kwa makini mapendekezo ya Serikali utagundua pia kwamba Serikali inataka kijiwekea kinga ya kisheria ya kutolipa madeni makubwa inayodaiwa na watu na pia kuwahujumu watu wenyewe mgogoro na Serikali kwa kuwa itakuwa ni rahisi kwa Serikali kuwageuzia kibao watu wenyewe mgogoro nayo au wenyewe madai dhidi yake na kuafilisi mali zao kupitia sheria hii.

34. Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza zaidi ni pale Serikali inapopendekeza kutaifisha mali halali iliyopatikana kwa kipindi cha miaka mitano nyuma kabla kosa halijatendeka. Jambo hili halikubaliki kwa kuwa litaathiri familia nzima ilhali aliyetenda kosa ni mmoja. Kama ilivyo desturi mali za familia huchumwa pamoja kwa maana ya mke na mume au ndugu wa familia, hivyo kama ni mtu mmoja ametenda kosa inahalalisha vipi ufilisi wa mali ambazo ni za familia? Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maelezo ni kwa namna gani itatenganisha mali binafsi za mtenda kosa na mali za familia ili kutoiingiza familia nzima kwenye adhabu kwa kosa la mtu mmoja. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kifungu chote cha 4 kifutwe kabisa kwani ni kifungu ambacho badala ya kuangalia ustawi wa nchi yetu, kinalenga kuwavizia watu wenye mtazamo tofauti na Serikali na kuwafilisi mali zao na pia kitapunguza morali ya wawekezaji hapa nchini kwa na hofu ya kufilisiwa kutokana na hila za kisiasa.

**vi. Marekebisho ya Chama cha Msalaba
Mwekundu Tanzania, Sura ya 66**

35. Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kutaka kuifanya sheria hii kutumika katika pande zote mbili za Muungano, na vile vile kuongeza mawanda ya nembo ya Msalaba mwekundu kuwa pia ni mwezi mwekundu. Hata hivyo, uko mkanganyiko kuhusu ya matumizi ya sheria hii kwa kuwa sheria itatumika pande zote mbili za Muungano, lakini waziri anayepewa dhamana ya kuisimamia sheria hii ni Waziri wa Katiba na Sheria – wizara ambayo si ya Muungano. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapopendekeza waziri atakayekuwa na dhamana na sheria hii awe waziri wa Mambo ya ndani ya nchi ambayo ni wizara ya Muungano na sio waziri wa sheria kama muswada unavyopendekeza.

C. HITIMISHO

36. **Mheshimiwa Spika**, napenda kumalizia hotuba yangu kwa kuiasa Serikali kwamba; utunzi wa Sheria una lengo kuweka utaratibu wa uendeshaji wa mambo katika jamii. Ili utaratibu huo uweze kufanya kazi ni lazima uwe unafahamika na uwe unakubalka na jamii nzima. Kwa sababu hiyo, ipo haja kubwa ya kuishirikisha jamii katika mchakato mzima wa utunzi wa sheria ili jamii iweze kuziheshimu sheria hizo ili ziweze kufikia malengo yaliyokusudiwa.
37. **Mheshimiwa Spika**, tofauti na dhana hiyo ya ushiriki mpana wa wananchi katika utunzi wa sheria, kumekuwa na desturi mbaya kwa Serikali kuwaita wadau wachache kuchambua miswada huku idadi kubwa ya wananchi ambao ndio walengwa wa sheria husika, wakiwa hawajui chochote kuhusu sheria hizo.
38. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuutambua upungufu huo; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kupitia chadema, imeweka bayana katika sera yake ya Utawala Bora (Sura ya 2.1) kuhusu ushirikishwaji wa wananchi katika kutunga sheria. Sehemu ya sera hiyo inasema kwamba; naomba kunukuu.. *"Chadema itawashirikisha wananchi kutoa maoni na mapendekezo katika mchakato wa kutunga sheria zote za nchi ili kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa sheria hizo".*
39. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Lathifah H Chande (Mb)
MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI KATIKA
WIZARA YA KATIBA NA SHERIA
5 Septemba, 2019

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaanza michango, tunaanza na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga atafuatiwa na Mheshimiwa Alberto.

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza lakini pia nitumie fursa hii...

MWENYEKITI: Dakika kumi...

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Niseme sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniongezea mwaka mmoja wa umri wangu nikiwa na afya njema na uzima. Nashukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali na timu yake yote pamoja na Serikali kwa ujumla kwa kuweza kufikiria kuleta marekebisho ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.4 ya mwaka 2019 kwa wakati huu ambao naamini ni muafaka kabisa. Lengo na dhamira ya kuleta marekebisho haya ni kuziba mianya (*gaps*) ambazo zipo katika sheria hizo ambazo ni 11 katika Muswada huu ulioletwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana na kumpongeza AG kwa usikivu na umakini wake wakati tunashirikiana na Kamati kiasi kwamba ameweza kupokea ushauri mwangi wa Kamati na kuufanya marekebisho kama ambavyo tumeona kwenye Jedwali la Marekebisho. Kwa hiyo, usikivu wake umeweza kuleta Muswada ulio bora kwa maslahi ya Watanzania wote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na Sheria ya Mawakili, Sura ya 341. Ni lazima nikubaliane na Serikali kwamba mfumo wetu wa sheria unaendana na mfumo wa Sheria ya Jumuiya za Madola na wenzetu katika nchi hizo kwa muda mrefu wamegundua kwamba taaluma hii ya sheria inapokuwa katika mazingira ya Serikali ikiwa itachanganywa na *private sector* inaweza kuleta migongano

mikubwa ya kimaslahi katika nchi yetu tofauti kabisa na taaluma nyingine kama vile madaktari, walimu na wengineo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kukubaliana na maono hayo ya Serikali ili tuendane na *International Standards* za nchi za wenzetu ambao tunaiga mifumo yao ya sheria, Serikali hatuna budi pia kufikiria mazingira halisi ya nchi yetu na wananchi wake. Kwa hiyo, nina imani kubwa Mwanasheria Mkuu na Serikali kwa ujumla wanaweza kuyafikiria maoni na ushauri uliotolewa kwenye Kamati kuhusiana na hawa Mawakili ambao wanafanya kazi Serikali na kuweza kuweka mfumo bora ambao utasaidia kurahisisha kazi ndogo ndogo ambazo hazileti migongano ya kimaslahi kwa maslahi ya wananchi wa nchi yetu lakini pia kwa manufaa machache ya Mawakili wenywewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini ushauri huo Serikali yangu sikuvi itasikiliza na kuweza kuweka mfumo bora na kuwaruhusu hawa Mawakili ambao wanafanya kazi Serikali ambao utasaidia kuwasaidia hasa wananchi wetu walioko vijijini ambapo pengine kwenye Halmashauri kuna Mawakili wawili tu Serikalini kwa hiyo ili kuwafuata sasa Mawakili wengine ili kupata huduma ya hati za viapo, mikataba pamoja na hati nyingine basi tufikirie namna bora ya kuweza kuruhusu kulingana na mazingira ya Kitanzania na mazingira ya wafanyakazi wetu. Naamini hilo utakuwa umelisikia vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tukija kwenye Sheria ya Vizazi na Vifo, hii nayo imekuja wakati mzuri, wakati Taifa letu bado tunaendelea kuzaa na vifo vinaendelea lakini na wale ambao watakuwa nje ya nchi basi sheria hii itakuwa imewafaidisha kuweza kujua takwimu sahihi na hata katika sensa zitakapotokea itakuwa imesaidia sana katika uweka idadi kamili ya Watanzania tulipo na wale ambao wamepoteza maisha yao. Sheria hii pia inakwenda kutekeleza misingi bora ya Sheria ya Mtoto ile ya mwaka 2019 ambayo inataka tutimize haki na ustawi wa jamii wa mtoto katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuwepo kwa sheria hii ilioletwa hapa kama ni marekebisho ya sheria hii itasaidia kurahisisha kazi hasa baada ya kushusha yale mamlaka ya usajili kwa Wasaidizi Wasajili ambao wako katika kata na halmashauri zetu badala ya kumuachia Msajili Mkuu. Kwa hiyo, kazi itarahisika na mambo yatakwenda vizuri na ndiyo maana nasema kwamba kazi hii ni nzuri na imekuja kwa wakati muafaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu *Red Cross* (Chama cha Msalaba Mwekundu). Sheria hii imekuja katika nchi yetu kwa muda mrefu sana na ni chama ambacho kimefanya kazi kubwa sana katika kuokoa maisha ya watu wetu katika nchi yetu popote pale yanapotokea majanga Tanzania nzima. Hata hivyo, Tanzania Zanzibar pia imekuja ikifanya kazi kwa miaka mingi ya nyuma pamoja na kwamba sheria hii ilikuwa ikitumika Tanzania Bara tu. Kwa hiyo, kuletwa kwa marekebisho haya kutasaidia na Zanzibar kuonekana ni sehemu ya sheria hii na hivyo wigo wake mpana kufanyika bila uvunjaji wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, sheria hii inakuja kuweka wazi maana halisi ya Chama cha Msalaba Mwekundu. Dhana potofu ya watu wachache katika nchi hii ni fikra kwamba chama hiki ni cha dini fulani lakini sheria hii inakuja kuweka sawa kwamba Chama cha Msalaba Mwekundu ni chama ambacho kinatoa msaada Tanzania na dunia nzima bila kujali dini au kundi la aina yoyote. Kwa hiyo, sheria hii inakuja kuweka sawa mambo hayo na wigo mpana wa chama hiki utasaidia Taifa letu katika viwango vya Kimataifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni makubaliano ya awali baina ya Mwendesha Mashtaka na mtuhumiwa katika kesi hizi za jinai ambazo zimeelezewa hapa (*Plea Bargaining*) ambayo imeletwa kwa madhumuni ya kupunguza mrundikano wa kesi Mahakamani lakini pia kupunguza kiwango cha adhabu ambacho pengine mtu angepewa wakati ameshajua kwamba hili kosa mimi

nimefanya. Kwa hiyo, iko vizuri na naamini itasaidia sana katika kupunguza hayo mambo ambayo tumekusudia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni marekebisho ya Sheria ya Mali itokanayo na uhalifu, Sura ya 256. Nchi yetu kwa muda mrefu imekuwa kimya na kuachilia watu wachache wakijilimbikizia mali kwa njia ambayo siyo ya halali na kujinufaisha wenyewe huku Watanzania walio wengi wakiumia na hali ngumu ya maisha. Kwa hali hii tunayoenda nayo sasa na Awamu ya Tano ya Serikali yetu ambayo inapinga vikali suala hilo, sheria hii imekuja sasa kuweka sawa hali nzuri ambayo itasaidia watu wanaojilimbikizia mali kuzikosa mali hizo itapothibitika kwamba wamepata kwa njia isyo ya halali. Kwa hiyo, watu kama hao wakae tayari na wajue kwamba mwisho wa kufanya ubaya ni kuona haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuwadhulumu Watanzania kwa kujilimbikizia mali ambazo siyo halali na kuwafanya wengine waendelee kuwa wanyonge sio jambo zuri kwa sheria za nchi wala sheria za Mungu. Kwa hiyo, hilo ni jambo zuri na naunga mkono sheria hii lakini ni matumaini yangu makubwa kwamba Serikali itazingatia Katiba ya nchi na misingi yake kwa kutowahisha wale ambao wanahisi kwamba wanashirikiana na hao wahalifu wakubwa kwa kuzishika mali zao na pengine kuzitaifisha wakati ushiriki wao si wa *principal offender* ambaye ye ye ndiye mhusika mkuu. Naamini kabisa Serikali yangu itazingatia Katiba na kutekeleza sheria hii kwa mujibu wa sheria. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono Muswada huu na naomba tuupitishe kwa moyo mmoja. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Alberto, jiandae Mheshimiwa Lathifah.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kabla sijachangia kwenye vifungu, nataka niseme vitu viwili vya mwanzo. Cha kwanza nataka ku-

appreciate jinsi ambavyo Serikali imekuwa ikifanya kazi na Kamati yetu kwa maana ya kwamba imekuwa ikisikiliza na baadhi ya mengi ambayo tuliyapendekeza yamekuwa *incorporated* kwenye sheria hii. Hata hivyo, tulikuwa na mengine ambayo tungependa pia yabadilishwe, hayakubadilishwa lakini ndiyo *give and take* katika mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nataka niunge mkono maoni ya Kambi kwamba kuna tatizo kubwa la *public hearing*. Sijui tunakosea wapi msemo wa siku hizi lakini hatupati watu wa kutosha kuchangia katika Miswada. Maana yake ni kwamba hatupati maoni ya kushiba tuwajue wadau wanataka nini ili sheria zikirekebishwa ziwe *robust* na ziweze kudumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri kuna haja ya Bunge kutafuta utaratibu mzuri zaidi wa kupata maoni pengine Kamati itoke nje ya Dodoma iwaafuate watu *regionally* au vituo maalum kupata maoni kuliko kutegemea wadau waje hapa katika mzunguko huu wa uhaba wa fedha kiasi ambacho pengine inakuwa vigumu kwa wadau kuja Dodoma. Wakati mwingine sheria zinatolewa anakuja mdau anasema mimi nilikuwa nikiandika kwenye gari kwa maana taarifa nilipata juzi, jana niko kwenye gari nasafiri, njiani naandika ndiyo nimekuja kutoa maoni kuliko kuiacha nafasi ikapotea bure. Naomba sana suala hili tulirekebishe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia suala la Mawakili ambalo limetajwa katika sehemu mbili kwenye sheria hii. Kusema kweli tulizungumza sana juu ya haja ya Mawakili wa Serikali kuweza kufanya kazi zao kama ambavyo Mawakili wengine wa binafsi wanafanya lakini tukaambiwa kwamba *practice* hii inafanywa sehemu nydingine ya kuwazuia Mawakili wa Serikali wasiwe *engaged* katika *private businesses* lakini Serikali haikuja na chochote kile kuthibitisha Uingereza, Sri Lanka au China wako hivi, hawakuja na mifano halisi. Wamesema tu kwamba hii ni *standard practice* kwamba Mawakili wa Serikali hawafanyi kazi za binafsi lakini wanashahau kwamba hao Mawakili wa Uingereza wasiofanya

kazi za binafsi, Uingereza inajitosheleza kwa Mawakili, Uingereza haina *remote places* ambazo Wakili hafiki, Uingereza haina sehemu ambazo Halmashauri pengine kuna mwanasheria mmoja naye ni Hakimu lakini pia huko katika Halmashauri zetu au katika vijiji kuna mwanasheria mmoja tu ambaye pengine angeweza kusaidia lakini kwa bahati mbaya au bahati nzuri yuko Serikalini lakini anazuiwa asifanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona hapa na *na-appreciate* Serikali kwamba wameweza kutengeneza mazingira kwamba wanaweza kufanya utaratibu huyu Wakili akaweza angalau kufanya kazi kama za viapo, kusimamia masuala ya mikataba lakini pia katika mazingira maalumu anaweza hata aka-*practice* lakini kwa taratibu zilizowekwa. Tunaomba hizo taratibu zisiwe *restrictive*, ziwe pana ili kuruhusu uwezekano wa mtu kupata nafasi ya kuwa Wakili binafsi tukizifanya *restrictive* itakuwa halsaidii kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hotuba ya Kambi imesema inawezekana siku zijazo tukapata watu wakakataa kuwa Mawakili wa Serikali au waajiuliza mara mbili kuwa Wakili wa Serikali ikiwa tutakuwa na *very restrictive* Kanuni pengine mtu asiweze kupata fursa ya kufanya vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi kwenye suala la *Registrar General*/kwamba hivi sasa uandikishaji wa masuala ya vizazi na vifo unashuka chini. Kusema kweli *this is a very good spirit* kwa sababu huko kutasababisha takwimu zikusanywe vizuri zaidi lakini pia vile vyeti vyya kuzaliwa vitatengenezwa kwa haraka zaidi kuliko hivi sasa pengine mtu ana sehemu kubwa ya kwenda au anatumia muda mrefu kwenda sehemu hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nalotaka kuzungumzia ni mali zinazopatikana kwa njia ya uhalifu. Kwanza nitazungumza habari ya *Plea Bargaining*, hii ni dhana mpya. Tuliiambia Serikali katika Kamati kwamba tungependa tupate mifano ya *Plea Bargaining*. Wanasema kwamba hii ipo lakini sasa inarasimishwa zaidi lakini sisi Wajumbe wa

Kamati kama ilivyo mara nyingi huwa si rahisi Serikali kuturuhusu tudurusu vya kutosha juu ya dhana ambayo wanaileta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli walikuja wakafanya semina, lakini bado mimi binafsi kama Mjumbe wa Kamati sikushiba, sikuona ule uelewa kwamba napitisha sheria hii ili baadaye ije ipate picha gani? Kwa sababu, sikuletewa mifano mingi, naambiwa tu kwamba, inatumika kwingine na kwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tumeweka vifungu ambavyo tunajitia pingu wenyewe. Tumesema yako maeneo ambayo hayatakuwa katika *plea-bargaining* tunesema uhaini, makosa ya ugaidi na mengine. Sasa makosa mengine ambayo ningependa yawe katika *plea-bargaining* ndio yametolewa wakati ukiyaweka katika *plea-bargaining* unaweza ukapata fursa ya kuyafanya kazi na ukayaua kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Kambi imesema hapa, kwa mfano kwenye mambo ya *drugs* ambayo nimefurahi Serikali imeongeza kiwango kutoka shilingi milioni 10 kwenye dawa za kulevyaa hadi 20 na hali kadhalika kwenye nyara za Serikali imeongeza shilingi milioni 20 ili haya yasemwe katika *plea-bargaining*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utavunjaje mitandao ikiwa wewe hutaki kufanya *plea-bargaining*? Mtu umemkamata *drug lord*, pengine ana biashara ya shilingi bilioni 50, ana mtandao wa watu 200 wako nchi nyingi duniani, unakataa kuingia naye *plea-bargaining* unasema kwamba, suala la dawa za kulevyaa hakuna *plea-bargaining*, ina maana hata ukimfunga, ndiyo yale yanatokezea kwamba mtu yuko ndani, bado anaweza akapata huduma, anaweza akawa anaendesha biashara yake wakati yuko ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Serikali ingefikiri sana katika hili ili kuhakikisha kwamba, inawezekana

kwamba *plea-bargaining* isiwe maeneo haya au tusijifunge kuyaondoa yote kwa sababu yanaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni mali zinazopatikana kwa njia ya uhalifu. Msemaji aliyejita hapa amezungumzia kwamba, hii sheria ni nzuri, lakini pia kuna ubaya wake kwa sababu, ubaya wake mmoja ni kwamba, inawezekana sasa mtu anakamatwa au unaundiwa kosa na kama ilivyosema hotuba ya kambi kwamba ili wakukamate vizuri wanakwambia mali hii uliyopata hapa tunaichukua kwa sababu imo ndani ya miaka mitano ambayo wewe unashitakiwa kwa kosa la uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajuliza, hivi kigezo gani Serikali imetumia kusema miaka mitano? Kwa nini isingekuwa mitatu? Mimi niliuliza kwenye Kamati, kwa nini iwe miaka mitano? *You go back so much time.* Miaka mitano pengine mtu alikuwa akifanya biashara halali, unazuia mali zake mpaka watakaptopo kuthibitisha *otherwise*. Halafu hukuna kifungu au njia yoyote ya kupata fidia ikiwa mali yake ile iliyozuiliwa kwa miaka wakati wa kesi, Serikali ikashindwa kuthibitisha kwamba alikuwa na kosa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ingawa taratibu zitawekwa, lakini ningependa hii iwe *very strict* na *due process* itumike ili Serikali ithibitishe Mahakamani *beyond doubt* kwamba au ithibitishe kwa kiasi kikubwa kwamba shaka ya mali ile iliyopatikana kwa njia haramu inaweza ikatumika na Mahakama kuliko Mahakama kushawishiwa tu kwamba hasa ilivyokuwa ni *ex parte*. Serikali itakwenda peke yake itasema mali ya Musa au mali ya Juma tuna shaka imepatikana miaka mitano ndani ya kipindi cha uhalifu, *ex parte* peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini isifanye basi ikawa *argued* Mahakamani ili kuthibitisha? Matokeo yake ni kwamba, kwa sababu wanakwenda upande mmoja tu, nayo ni *very dangerous*, inawezekana ikawa hasara kwamba mtu anakamatiwa mali yake wakati pengine ile mali haikuwa ya uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha mwisho nitakachozungumzia ni suala la *Red Cross*. Nilihoji kwa nini *Red Cross* inafanya suala la Muungano? Nikahoji kwamba kuna sheria nyingi za Kimataifa au Mikataba ya Kimataifa kwa mfano Mkataba wa Watoto, Zanzibar imeweza kusimama yenewe bila ya kufanya kwamba ni suala la Muungano ingawa huu ni Mkataba wa Kimataifa. Kwa sababu, tunaongeza mambo ya Muungano *unnecessarily*. Hakuna haja hata *Red Cross* kufanya suala la Muungano, mimi sioni kwa sababu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli ni Mkataba wa Kimataifa, kweli unatekelezwa Kimataifa, lakini mbona mikataba mingine ya Kimataifa Zanzibar inatunga kanuni zake, ingawa unaridhiwa na Serikali ya Muungano, lakini inatunga sheria zake yenewe. Kuna ulazima gani *Red Cross* kuifanya ifanye kazi mpaka Zanzibar?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mna abandon mambo mengi na kama iliyosema Hotuba ya Kambi ya Upinzani, unaichukua *Red Cross* unakwenda kupeleka kwa Waziri ambaye sio wa Muungano. Au inapelekwa sehemu ambayo utekelezaji wake utakuwa mgumu kwa sababu mnaongeza mambo ya Muungano pasipo haja ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwamba kwa muda huu tumefanya vizuri sana na upande wa Serikali nashukuru kwamba, walikuwa wasikivu, lakini waendelee kuwa wasikivu ili tuweze kutoa ya moyoni kwa maana ya kujenga nchi. Sote tunajenga nyumba moja tufanye kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lathifah, jiandae Mheshimiwa Daniel Mtuka.

MHE. LATHIFAH H. CHANDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote ningependa kuzungumzia juu ya marekabisho ya Sheria ya *Proceeds of Crime*, yaani mali zinazotokana na uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 37 ambayo inaenda kufanya marekebisho ya sheria mama ya Kifungu cha 22 ambacho kinaenda kufuta kabisa kifungu Kidogo cha (4) na kuleta Kifungu Kipyä cha 4C ambacho kinasema, mtu akikutwa na mashitaka ambayo yapo katika *serious offences* ikiwemo utakatishaji fedha na uhujumu uchumi, basi mali alioipata ndani ya miaka mitano iliyopita itashikiliwa na kuchukuliwa kama mali iliyopatikana kutokana na uhalifu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kiko kinyume na sheria kwani inawezekana kabisa ikawa mapendekezo haya ya sheria yana nia ovu ya kuwakamata watu na kuwabambikiza na kesi za uhalifu kwa nia tu ya kuweza kukamata mali zao ambazo inawezekana kabisa mali hizi walizipata kihalali kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu, inawezekana kabisa mtu akawa amepata mali kihalali, baada ya miaka mitano akaja kutenda lile kosa. Sasa kushikilia baadhi ya hizi mali ni kinyume na sheria ya umiliki wa mali kwa sababu, zitenda kuguswa hata mali ambazo hazihusiani na mtuhumiwa. Mfano, mali ambazo zimechumwa na mke na mume, lakini pia zitaenda kugusa hata mali ambazo zimetokana na mirathi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Serikali ifute kabisa Kifungu cha 4C kuepusha kuleta shida na kwenda kutekeleza sheria hii ambayo mimi naiona ina nia ovu. Watu watakuja kukamatwa kwa makosa ambayo wanafanya leo mali zao zichukuliwe walizozimiliki miaka mitano iliyopita, haiko sahihi kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kushauri kwamba, pamoja na haya, tuangalie kwamba kila mali

kabla haijawa seized kuwe kuna *hearing* ya uthibitisho wa mali hii ilipatikana vipi? Yaani kuwe kuna *separate hearing* ya kila mali ambayo itachukuliwa na kuunganishwa na huo uhalifu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa ningependa kuzungumzia juu ya marekebisho ya Sheria ya Mawakili. Ibara ya 5 inazuia Mawakili kupewa vibali vya kufanya shughuli za kiuwakili wa Kiserikali kwa muda wote wa utumishi wao katika Serikali. Ibara hii inaenda kinyume na Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ndogo ya (2) inayosema, naomba nisome, "*Ni marufuku kwa sheria yoyote iliyotungwa na mamlaka yoyote katika Jamhuri ya Muungano kuweka sharti lolote ambalo ni la kibaguzi ama kwa dhahiri au kwa taathira yake.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa hiyo Ibara ya 5 ya Marekebisho ya Sheria ya Mawakili tunavyoiona inalenga kubagua taaluma ya sheria ikiwa kama taaluma ya sheria ni taaluma kama ilivyo taaluma nydingine. Kwa mfano, daktari ambaye ni Mtumishi wa Umma anaruhusiwa ku-practice taaluma yake nje ya utumishi wake wa Umma. Ikiwa kama Mhasibu anaruhusiwa ku-practice taaluma yake nje ya utumishi wa Umma kwamba anaweza hata akafanya shughuli za *financial consultancy*, na kadhalika, vilevile *lecturer* anaruhusiwa ku-practise taaluma yake nje ya Utumishi wa Umma, sasa iweje Mwanasheria azuiliwe ku-practice taaluma yake nje ya Utumishi wa Umma? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala ambalo haliko sahihi hata kidogo. Ikumbukwe kwamba baadhi ya hawa Mawakili wa Serikali wengine wamesomeshwa kwa pesa binafsi, vilevile kuna ambao wamesomeshwa kuitia mikopo ya elimu, mwisho wa siku wanahitaji kulipa mikopo hii. Isitoshe wanahitaji kukidhi maisha yao na wana majukumu katika familia zao. Sasa unapowakatalia hili maana yake ni kwamba unawaambia wategemee kipato kinachotokana na Utumishi wa Umma na wakati ni dhahiri wote

tunatambua kwamba kipato kinachotokana na Utumishi wa Umma hakitoshlezi kukidhi mahitaji haya yote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu kwamba kumnyima Wakili wa Serikali kwenda kufanya shughuli hizi za kiuwakili kunaenda kumkata miguu, lakini pia vilevile jamii inaenda kunyimwa fursa ya kuweza kupata *service* kutoka kwa Mawakili hawa wa Serikali. Mfano mkubwa ni sisi wenyewe, siyo kwamba Mawakili wale binafsi hawana uwezo wa kufanya hizi shughuli, lakini kuna wakati mtu ambaye ni wakaribu kabisa anakuwa ni yule Wakili wa Serikali, tunategemea kupewa huduma kutoka huko. Mfano, tumekuta sisi wenyewe Wabunge humu ndani, mara ngapi tunahitaji *affidavits* *signed?* Mara ngapi tunahitaji *forms* za maadili zikasainiwe ambapo watu hawa wamekuwa wakitufanyia *stamping* muhuri, tunaupata kutoka kwa hao hao Mawakili wa Serikali? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanya hivi ni kwenda kufanya kitu ambacho siyo kwamba kitamnyima tu haki yake yule Wakili wa Serikali, lakini hata na jamii nzima ambayo inawategemea. Hii pia, itaenda kudhoofisha taaluma nzima ya sheria, kwa sababu watu watakosa *interest* ya kwenda kwenye taaluma ya sheria. Sio hivyo tu, watu watakuwa hawataki wajiriwe wawe watumishi wa Umma na kusababisha Serikali kukosa Mawakili wa kutosha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba Ibara hii ya 5 iondolewe na badala yake pamoja na kwamba dhamira ilikuwa ni nzuri, lakini badala yake ili kuepusha Wakili wa Serikali kwenda kufanya shughuli za kiuwakili ambazo zitakuwa na *conflict of interest* na Serikali, basi kwa kuwa haya ni masuala ambayo yana mwelekeo wa kinidhamu na kiutendaji, kwa nini Serikali isije na utaratibu wa kuweka mwongozo ambao utakuwa wa kiutumishi, aidha kwa kupitia Utumishi au kwa kupitia kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote, napenda kuzungumzia suala la Serikali kutuletea Miswada

ya mabadiliko ya sheria kwa kupitia Hati ya Dharura. Hili suala haliko sawa hata kidogo kwa sababu, ukiangalia hata hizi sheria ambazo zimeenda kurekebishesha, mnataka kuniambia kuna udharura gani wa kufanya marekebishesha ya Sheria ya Mawakili? Kuna udharura gani wa kufanya marekebishesha ya Sheria za Usajili wa Vizazi na Vifo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Serikali iangalie hili kwa umakini zaidi kwa sababu, tunavyoendelea kuletewa haya marekebishesha ya sheria kwa Hati ya Dharura matokeo yake kunakuwa kuna ushirikishwaji finyu sana wa hao wadau ambao ndio wadau wakuu wa hizi sheria na kuwanyima haki wadau hawa kuweza kushiriki kikamilifu kwa kutupatia sisi maoni ya kutosheleza kwa sababu, mwisho wa siku tunaishia kutunga sheria na baada ya miaka michache tu mbele, hizi sheria zinaenda kuonekana kuwa na upungufu. Kwa hiyo, nasi kama Bunge mwisho wa siku tunakuwa tunatunga sheria mara kwa mara kutokana na upungufu huo ambao usikute kungekuwa kuna ushirikishwaji wa ukamilifu wa wadau hawa tungeweza kutunga sheria ambazo zinaweza zikawa *everlasting*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi baada ya kusema haya yote, naomba nikushukuru, ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Nimeshamwita Mheshimiwa Daniel Mtuka, ajiandae Mheshimiwa Asha Abdallah Juma.

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii nami nitoe mchango wangu katika Muswada huu. Kwanza niipongeze sana Serikali kuleta marekebishesha haya. Nitajikita zaidi katika ukurasa wa 21 wa Muswada, *Part No. 9*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 29 ya Muswada huu inaleta marekebishesha ya Sheria ya *PCCB* kwa maana ya *PCCA*. *Ni-declare interest* tu kwamba mimi nilifanya kazi kwenye ofisi hizi. Kwa hiyo, haya nitakayoyazungumza nimeyaishi na baadhi nimeyaishi na kuyafanya nikiwa katika utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali imeongeza sasa *sub-section* kwenye Kifungu cha 57 cha Sheria ya Makosa ya Rushwa kwa maana ya *PCCA*, zimekuwa *sub-section* tatu. Naomba ninukuu tu sasa itakavyokuwa inasomeka hasa ile *Sub-Section (2)* kwa maana ya 57(2) itasomeka kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unisikilize kwa makini. *"Consent under Sub-Section (1) shall be obtained in accordance with the provisions of Section 9 of the National Prosecution Act, ile number (2),* lakini ya mwisho ya tatu sasa itasomeka, *"The DPP shall within 60 days,"* hii sina tatizonayo. Tatizo langu kwenye Kifungu cha hiyo *sub. (2)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeenda nimetazama hiyo *NPSS* ya mwaka 2008, pia nikaisoma kwamba sasa ule mfumo au mlolongo wa kupata kibali utafuata ile sheria ya Taifa, *The National Prosecution Act*. Nikaiendea nikaisoma inasema hivi, naomba ninukuu, *"For the purpose of Sub-Section (6) The Director may by notice publish in the gazette specify offences or threat a threshold of value involved in a case the prosecutions of which shall require the consent of the director in person and the power consenting the prosecution of which, may be exercised by such officer or officers subordinate to him as he may specify acting in accordance with his general or special instructions."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio changu hapa mamlaka sasa ya Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU hayapo. Mkurugenzi Mkuu kumbuka kwenye Sheria yake ya *PCCA Section No. 5 PCCB* ni Taasisi inayojitegemea, sasa iweje tena huyu *Director* wa *PCCB* aanze kupokea maelekezo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ni kitu ambacho sasa tunaiua TAKUKURU kabisa, nayasema haya nikiitaza nchi yangu siyo ushabiki wa mambo mengine yoyote yale adui rushwa ni mgogoro mkubwa sana katika nchi hii, hapa kwa kweli bado tunatwanga maji kwenye kinu tuaishia kuloa, hapa narudia kuna shida. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kwenye kifungu hicho cha 57 (1) naomba sana viongezewe vifungu

kupanua wigo. Kifungu kinasema hivi *except for the offences under section No. 16 tuongezee section* zingine kwenye ile PCCA tupunguze sasa mlolongo wa makosa kwenda kwa DPP hawa wawe na uwezo wa ku-prosecute makosa mengi zaidi. Kwa mfano, ukiangalia Kanuni ya adhabu *Penal Code* Polisi wana uwezo wa kufanya *prosecution* makosa ya kwa mfano Kifungu cha 265 juu ya wizi, *forgery*, ubakaji, hawapiti kwa DPP, lakini makosa yanayofanana na haya ambayo yako kwenye Sheria ya PCCB kwanini waende kwa DPP?.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukienda kwenye Kifungu cha Na. 22 kutumia nyaraka ya kumdanganya Mwajiri si ndiyo ni sawa na kama *forgery* kule *penal code*, matumizi mabaya ya madaraka Na. 31 haihitaji kwenda kwa DPP. Rushwa za ngono haihitaji kwenda kwa DPP mbona Polisi wanaenda moja kwa moja kwenye mambo ya ubakaji. Kwa hiyo, haya makosa yote yarudishwe sasa yaongezewe hapa kwenye isiwe 15 peke yake, iwe 15, iwe 22, iwe 31 pamoja na 28 nadhani mambo ya ubakaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *Traffic* hapo hapo kwa mfano, makosa ya *traffic* yote unayoyajua Mheshimiwa Mwenyekiti hayaendi kwa DPP. Kwa nini sheria ya TAKUKURU inabanwa kiasi hiki, ninaomba sana baada ya mazungumzo haya mafupi niseme tu kwa ufupi sana tuitazame sana nchi yetu hii. Tukiibana hapa TAKUKURU juhudzi za Mheshimiwa Rais na juhudzi za Serikali ya Awamu ya Tano na zinazofuata itakuwa ni kazi bure.

MWENYEKITI: Ahsante, nitakupa nafasi kwenye vifungu utayasema hayo tena. Mheshimiwa Asha Abdallah Juma jiandae Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) ningependa kwanza kuanza kwa kupongeza kazi kubwa sana iliyo fanywa na Kamati yetu ushiriki uliowakilishwa na wadau katika kuja kutoa maoni yao, walishiriki vizuri

Mwanasheria wetu naye kasimamia vizuri mambo hayo ya sheria naye kabobe na hii kazi anaiweza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuongelea juu ya hili rekebisho la sheria kwenye Usajili wa Vizazi na Vifo Sura 108. Marekebisho haya ni muafaka na yamekuja wakati ndiyo sana, kwa sababu tumeona kwamba vifo na vizazi vingi vinakuwa havisajiliwi mpaka sasa tatizo hilo bado lipo na imani yangu kwamba nchi haiwezi kuendelea kama haiwezi kujua idadi kamili ya watu wake wale amba wanaishi na wale amba wanazaliwa kwa hivyo mipango inaweza kupata ugumu. Kwa nini sijui hampigi makofi wakati mimi nasema maneno ya maana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwakabidhi rekebisho hili linalowapa nafasi Watendaji wa Vijiji kuweza kufanya hii kazi itarahisisha sana kwa sababu itarudisha ile huduma chini sana kwa hivyo kutapunguza kuhangaika kwa wananchi wetu katika kutafuta huduma hii. Hili vilevile litaendana na agizo la kidunia *Convention on the Rights of the Child* ya mwaka 1989 inalooana na sheria ya *The Child Act* Sura Na. 13 pamoja na Kanuni zake zote zilizoko pale. Kwa hivyo, tutakuwa tunakwenda kama dunia inavyotaka twende lakin ningeshauri tu kwenye hili hawa watendaji waweze kupewa mafundisho au maelekezo rasmi ili hili zoezi liweze kufanyika kwa wepesi. Nikisema hivyo nina maana kwamba waweze kurekodi hali halisi kama inavyokuwa kwa sababu hili ni jambo ambalo litakaa na ni jambo ambalo tunalihitaji kwa kupanga mipango yetu ya baadaye

Mheshimiwa Mwenyekiti, rekebisho lingine katika haya ambayo nataka kuyazungumzia ni hili la mapato la kushughulikia mapato ambayo yanatokana na uhalifu Sura 256. Hili limekuja wakati muhimu sana, tunakumbuka sote kwamba kumekuwa na desturi ya kupiga, kupiga maana yake kuiba kwa kitaalamu watu kujilimbikizia mali kwa njia wanazozijua wao halafu baadaye wazungu wanasema wakaenda *scot free* kwa sababu baada ya muda hakuna sheria inayowaba kuweza kuzirudisha zile mali na kuikosesha Serikali mapato yake ambayo ni muhimu katika maendeleo

ya nchi hii. Kwa hivyo, sheria hii itawabana kama wewe umeiba basi utabanza siyo unaiba halafu unakwenda kumpa mkeo Ester Bulaya halifai, tutambana huko huko. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tushughulike nao hawa wapigaji kama mkubwa wetu anavyosema. Rais kila siku anasema nchi hii imepigwa na imepigwa kweli kweli, kwa hivyo marekebisho haya yamekuja wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haki yako ipo na sheria tunaamini ipo inazingatia basi utaipata, hata kama ukiwa mke wa mtu lakini ikiwa ile mali imesemekana wewe umeipata kwa kupiga basi utathibitisha kama kweli wewe ni mke wa fulani lakini mali hii hukuipata kwa kupiga, kwa hivyo itarudi kwako hamna wasiwasni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiwe na wasi wasi tuiamini Serikali yetu sheria hizi na wasimamizi wa sheria zetu hizi wako vizuri na wamebobea kisheria, ndiyo maana tunaona kwa sababu sheria ni msumemo inakata kote na ndiyo maana kwa jithada na ubobezi wa wanasheria wetu ndege yetu imerudi, ingekuwa hakuna sheria na hakuna wabobezi wa sheria wa kusimamia basi ndege yetu ingepotea. Kwa hiyo, niwapongeze Wanasheria wa nchi hii mnafanya kazi nzuri sana. (*Makofi*)

MHE. ESTER A. BULAYA: Na wewe ukipiga?

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Nishughulikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninalotaka kuzungumzia ni hii Sheria ya Kurejesha Wahalifu Sura Na. 368 ikiongeza Kifungu Na. 8 (a) inamwezesha Waziri Mamlaka kumkabidhi yule mhalifu aliyekimbilia huku kwetu, kama umeharibu lazima uende ukawajibishwe huko huko, nasi tutakuwa siyo kama kisiwa tunaishi peke yetu dunia nzima tunaona. Tunakumbuka pia Manuel Noriega alichukuliwa huko kwa sababu alifanya uhalifu fulani akarudishwa, yule alikuwa ni Rais wa Panama lakini alirudishwa. Kwa hivyo, hii

mimi naona sawa sawa na ninawaamini Mawaziri wetu hawa wana uwezo wa kutosha siyo kama akiwa Waziri ndiyo ye ye ataamua tu hata hazingatii, kwa hivyo nchi yetu hii inaendeshwa kwa utawala wa sheria hovyo, itazingatia mambo yote hayo

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho mengine ni ya Sheria ya Msalaba Mwekundu sheria ya msalaba mwekundu Sura 66 ambayo imeweka Ibara ya 45 na 52 ni jambo zuri kwa sababu sharia itaweza kutumika bila matatizo yoyote kwa pande zote za Muungano. Vilevile sheria hii inaweza kutoa ufanuzi kabisa kwa sababu watu wengi mara nyingi wakiona msalaba mwekundu wanafikiria wanapelekea upande mwingine lakini hii ni *organization* ambayo iko kushughulikia wakati wa maafa. Maafa ni mambo ambayo *unpredictable* yanaweza yakatokezea wakati wowote, kwa hivyo kuiwekea nafasi nzuri illi iweze kuhudumu vizuri hii Jumuiya ya Msalaba Mwekundu ni jambo zuri sana hizi sheria zote naona zimekuja kwa wakati mzuri sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria nyingine ni hii Sura ya 341 ya Kazi za Mawakili. Nafikiri ni wakati muafaka Serikali kuweza kudhibiti Mawakili wake, kama wewe unatumwa na Serikali basi ukatumike na Serikali vizuri, laa kama unataka kufungua *Firm* yako mwenyewe fungua ukashughulike huko, lakini haiwezekani nchi yetu saa nyingine watu wetu ndani ya Serikali yetu, badala ya kuitetea Serikali wanakwenda kuiangamiza Serikali hilo halikubaliki katika uongozi huu wa John Pombe Magufuli hatutakubali tunataka wewe uiteteet Serikali ili tuweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri narudia tena ni huu uliofanywa na Mawakili wetu kutetea mpaka ndege yetu ikarudi hongereni sana Mawakili wa Serikali, nakupeni kongole kubwa sana endeleeni hivyo iteteeni Serikali yenu, teteeni mali zetu wapigaji wasipate nafasi, wakitaka kupiga wakapige majumbaji kwao, kwa wake zao huko na wapenzi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mhesimiwa Profesa Maghembe.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii nami nichangie walau neno katika mabadiliko haya ya Sheria Mbalimbali (Na.4) ya Mwaka 2019. Kwanza ni sema wazi kama mimi naunga mkono hoja hii iliyoko mbele yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati naunga hoja basi nichomekee vitu viwili, vitatu. Kwanza ningependa sana nimpongeze Mheshimiwa Rais pamoja na Azimio letu la jana basi niongeze kumpongeza kwa jinsi walivyo endesha Mkutano wa 39 wa SADC. Pili ningependa sana nimpongeze rafiki yangu na Shemeji yangu Mheshimiwa Miraji Mtaturu kwa kuchaguliwa na kuapishwa kuwa Mbunge wa Singida Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niingie katika sheria yetu hii ambayo iko mezani na kwanza nimpongeze sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri waliyofanya katika kuleta marekebisho ambayo yako mbele yetu lakini pia niongeze sauti yangu kwa kazi nzuri ambayo imefanywa na Mawakili wetu wa Serikali katika kesi ambayo wameshinda tena wameshinda kwa akili kubwa sana. Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki nasi wajue tuko nao katika kutetea mali zetu popote zilipo duniani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya vitu ambavyo vimenikuna sana katika hoja hii iliyoko mezani ni Mabadiliko ya Sheria ya Vizazi na Vifo, Sura 108 kwamba sasa Serikali itagatua mamlaka yale ya kutoa vyeti vile vya uzazi na vifo katika vijiji, kwamba Mtendaji wa Kijiji pale kijijini kwangu atafanya kazi hiyo na itapunguza adha ambayo wananchi wanapata. Mfano, nilikuwa nazungumza na Mgosi Mheshimiwa Shangazi kwamba watu wake wanatoka kwenye kijiji cha Mnazi wanakwenda mpaka Korogwe halafu wapande mlima waende mpaka Lushoto, kilometra 170 ndiyo warekodi kizazi au unatoka kwenye Tarafa yangu ya Jipendea kule kwa Kihindi unakwenda mpaka Lembeni mpaka unafika

Mwanga kilometa 70, halafu urudi zingine 70 kwa ajili ya kusajili uzazi tu au kusajili kifo. Kwa hiyo, ndiyo unakuta Watanzania wengi wanakuwepo lakini hawakusajiliwa wanapotakiwa sasa wawe na nyaraka zile za uzazi hawana. Kwa hivi hili ni jambo la kimapinduzi na sote tunaliunga mkono kwa nguvu zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ni muhimu sana katika suala hili ni kuweza kujua wananchi wa Tanzania ni akina nani? Kwa sababu katika kijiji Mtendaji wa Kijiji anawafahamu watu wote pale. Sasa watu wakijitokeza tu kutoka eneo lolote kwenda kwenye Mji Mkuu wa Wilaya kujianzikisha wanaweza kuandikishwa wale waliomo na wale ambao hawamo. Kwa hivi, jambo hili ni jambo zuri na tunaliunga mkono kwa nguvu zote zile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sura hii pia imerekebisha uasili wa watoto au *adoption of children* katika maeneo yetu. Kwa hivi hii sheria sasa inakuwa sheria ya kisasa na mambo tunakwenda nayo ni yale ya kilimwengu yaliyoendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nimeliona limefanywa kwa uzuri kabisa ni Sheria inayorahisisha Uendeshaji wa Masuala ya Jinai na Mashtaka katika maeneo mbalimbali kufuatana na marekebisho ambayo yametokea katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa kweli mimi sikuwa na mambo mengi ya kufanya katika kazi hii nilipenda niseme hayo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na Mungu akulinde. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru wachangiaji wote tumebakwa na mchangiaji mmoja na ataanza Saa Kumi na Moja Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa kwa hiyo ajiandae saa kumi na moja, baada ya hapo Serikali mjiandae kutoa majibu na hatimaye Muswada kuitishwa na Bunge Zima.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno haya, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilsitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, Mheshimiwa Mchengerwa, dakika 10.

MHE. MOHAMED O. MCHENERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sikudhamiria kuchangia lakini...

MWENYEKITI: Basi kaa chini.

MHE. MOHAMED O. MCHENERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na baadhi ya hoja nimeona nizungumze kwa uchache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme msingi wa marekebisho Na. 4 mwaka 2019 ni utekelezaji wa hati idhini iliyotolewa na Mheshimiwa Rais, hati namba 48, 49 pamoja na 50 ya mwaka 2019. Marekebisho namba 2 ya mwaka 2018 ndio msingi wa marekebisho haya namba 4 mwaka 2019 ambayo yamekwenda kubadilisha mfumo wa kisheria, hususan wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa zimekuwepo hoja nydingi ambazo hata ambaye pengine ningelikuwa sina ufahamu wa sheria ningelihoji hoja kama hizo ambazo baadhi ya Wabunge wamekuwa wakizihoji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo pengine linahitaji ufanuzi, kwanza pengine Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakuwana kazi kubwa sana ya kuwaelimisha Wabunge kuhusiana na marekebisho ya sheria hizi zote 11 ambazo kimadhumini na kimantiki ilikuwa na maana kubwa sana ili kuweza kutekeleza Sheria Na. 2 ya

mwaka 2018 lakini pia kuweza kuweka mfumo mzuri wa utoaji haki hususan katika hii Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwepo hoja ya ni kwanini Mkurugenzi wa Mashitaka anapewa mamlaka ya ye ye kuidhinisha kesi kwenda mahakamani. Hii ni misingi ambayo imewekwa katika Sheria ya *National Prosecution Service Act* lakini pia ukisoma Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (*Prevention of Corruption*) imewataka TAKUKURU kabla ya kuendelea na mashitaka basi kuwasilisha taarifa zao au uchunguzi wao kwa Mwendesha Mashitaka ili aweze kutoa kibali cha kushitaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wamehoji ni kwa nini Mwanasheria Mkoo wa Serikali ameleta kifungu hiki cha kumtaka Mkurugenzi wa Mashitaka kutoa kibali cha kushitaki. Pia kitu kikubwa ambacho pengine Wabunge wangejielekeza ni kwamba si Bunge tu hili kwa wakati huu au mtu ye yeyote mwengine mwenye mamlaka ya kufanya marekebisho yoyote hata Mwanasheria Mkoo wa Serikali kwa leo hataweza kufanya marekebisho tofauti na haya ambayo yamekuja kwa sababu msingi wa hoja hii ni Ibara ya 59(b) ambayo imempa Mamlaka wa Mashitaka wa kushitaki makosa yote ya kijinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi kama Kamati au mimi kama Mchengerwa pengine nimeona ni vyema kabisa iwapo tutakwenda katika misingi ile ambayo Mheshimiwa Rais aliisema ya kupunguza mashauri, tutawezaje kupunguza mashauri? Tunatambua kwamba kuna kesi nydingi ambazo zipo kwa Mkurugenzi wa Mashitaka lakini ili kuweza ku-*qualify* kifungu hiki, tuliona ni vyema sasa tukaongeza kifungu kingine ambacho kitampa mamlaka Waziri wa Katiba na Sheria ili kuongeza vitu viwili; kitu cha kwanza ni kuongeza wale wasaidizi wa Mkurugenzi wa Mashitaka wawe na mamlaka ya kutoa idhini ya kushitaki na ili tuweze kusaidia kwa sababu Taifa lolote ambalo linapambana na rushwa, msingi wake ni kuruhusu Mkurugenzi

wa Kupambana na Rushwa kuruhusiwa kuingia mahakamani moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hii ni *practice* ya nchi nydingi sana duniani, ukienda kule UK, Finland, Scotland na nchi nydingine Mkurugenzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa amepewa mamlaka sawa na Mkurugenzi wa Mashitaka lakini huku kwetu Katiba imezuia kwa mujibu wa Ibara ya 59 lakini ili tuweze ku-*qualify* eneo hilo ni vyema sasa kama ambavyo Serikali imekubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na pengine wajumbe wanaweza wakasoma jedwali la marekebisho ambalo Mwanasheria Mkuu wa Serikali amelileta ambalo tayari limeweka kifungu cha kusaidia katika kupambana na rushwa lakini pia katika kupunguza mashauri ambacho kitamtaka Waziri wa Katiba na Sheria kuongeza baadhi ya vifungu katika kanuni ambazo zitawataka Mawakili wote wa Serikali Wafawidhi wa Mikoa na Wilaya kuweza kusikiliza au kutoa idhini ya usikilizwaji wa kesi za jinai katika maeneo yao ambazo zitaangukia kwenye kiwango fulani cha fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili kuweza kupunguza tatizo hili la mrundikano wa mahabusu nimeona hili ni eneo zuri ambalo tumpongeze Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuridhia eneo hili kuingizwa kwenye sheria na tuwatoe hofu wale ambao wadau wa kupambana na rushwa kwamba Bunge hili kwa wakati huu halina mamlaka ya kurekebisha Katiba Ibara ya 59(b) na pengine marekebisho haya ambayo tayari yameletwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndio tiba ya eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo pengine limekuwa natafsiri ambayo kwa kweli si nzuri au baadhi ya watu wametoa tafsiri ambayo pengine haikueleweka vizuri na kutokana na hotuba yangu ya Kamati ni eneo lile la waendesha mashitaka yaani Mawakili wa Serikali kuzuiliwa kufanya kazi ambazo zinagongana na kazi za msingi za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale mapendekezo ambayo Kamati ya Katiba imeyatoa ni mapendekezo mazuri nitumie fursa hii kumpongeza sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuridhia marekebisho ambayo kamati ilikuwa imeyatoa na msingi wa marekebisho ambayo yametolewa kwenye jedwali la Serikali na ambalo limetolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni hoja ambazo Kamati ya Katiba na Sheria imezitoa. Na ukisoma katika taarifa ya Kamati ya Katiba na Sheria imekwenda kutoa tafsiri ni namna gani Serikali itaweza kutibu tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa pengine Serikali ianzishe utaratibu wa kutoa posho ambazo zinakwenda kutibu lile tatizo la Mawakili wa Serikali kutoruhusiwa *ku-practice*. Pili, ikumbukwe pia kwamba kuwa wakili wa kujitegemea viro vyeti viwili ambavyo Mwanasheria anapaswa kupata; cheti cha kwanza ni kile cha *ku-practice* kama Wakili lakini cheti cha pili ni kuruhusiwa kuwa kamishna wa viapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili Serikali iweze kutibu tatizo hili na kama kamati ilivyoshauri na tuipongeze Serikali kwa kukubali sasa kwamba wale Mawakili wa Serikali wataruhusiwa moja kwa moja kuwa Makamishna wa Viapo na kwa kulitibu hilo pengine linaondoa kelele nyingi ambazo Wabunge wamekuwa nazo hususan ni kwanini Mawakili wa Serikali hawataruhusiwa *ku-practice*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; tuipongeze Serikali kwa kuongeza baadhi ya ibara katika marekebisho ya jedwali la Serikali liliowasilishwa hapa Bungeni ambalo sasa linamtaka Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwenda kuweka utaratibu mzuri ambao utawaruhusu Wanasheria wa Serikali kuruhusiwa *ku-practice* kwenye kesi ambazo hazina mgongano na Serikali. Kwa hiyo, yule Mwanasheria wa Serikali ambaye pengine angetamani *ku-practice* kama Wakili wa kujitegemea atawekewa utaratibu na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambao utamruhusu yeye kuruhusiwa *ku-practice* kwa kuangalia tu kwamba jambo analokwenda kulifanya haligongani na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni maeneo mawili ambayo pengine ningetamani kuyazungumza ili kuweza kuweka mambo vizuri. Baada ya kusema hayo, nakushukuru. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa *Attorney General*, dakika kumi zinatosha?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika 20.

MWENYEKITI: Mengi umeyamaliza lakini, haya.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Basi nitajitahidi na dakika kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kufanya majumuisho ya mjadala huu kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2019. Jumla ya Waheshimiwa Wabunge saba wamechangia muswada huu kwa kuzungumza nao ni Mheshimiwa Najma, Mheshimiwa Ally Saleh, Mheshimiwa Lathifah, Mheshimiwa Daniel Mtuka, Mheshimiwa Asha Abdallah, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe na Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja mbalimbali zilizotolewa za Waheshimiwa Wabunge kuna masuala ya jumla lakini pia kuna masuala yanayogusa sheria mojamoja. Kwa ajili tu ya rekodi nitapenda kujibu kidogo hoja aliyoibua Mheshimiwa Lathifah kwamba Muswada huu umeletwa kwa hati ya dharura kwa ajili tu ya kuweka rekodi vizuri, si sahihi kwamba Muswada huu uliletwa kwa hati ya dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na maoni juu ya *DPP* kushirikiana na ngazi nytingine na wadau wengine wa Serikali anapotekeleza majukumu yake. Hili tumelipokea lakini Waheshimiwa Wabunge wakijielekeza kwenye aya h hasa kipengele (b) na (c) cha jedwali la kwanza la marekebisho la Serikali hili limefanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye sheria mojamoja, tuanze na Sheria ya Mawakili; hapa nisingependa kuharibu tena maneno na maelezo mazuri sana ambayo ameyatoa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria. Kwa hiyo, kwa kweli nisiharibu maelezo hayo mazuri lakini niseme tu pendekezo la posho Serikali imelichukua na kwa sababu ni suala la kiutawala litafanyiwa kazi kiutawala. Pendekezo la mafunzo limepokelewa nalo ni la kiutawala linafanyiwa kazi kiutawala. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia palikuwa na hoja ya Mheshimiwa Lathifah na yenyewe kwa lengo la kuweka pia rekodi vizuri iliyokuwa inaonesha wasiwasi kwamba mabadiliko haya ya sheria yanavunja Ibara ya 13(2) ya Katiba. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa na wengine wote wenye wasiwasi huo kwamba hakuna uvunjaji wowote wa Katiba kwa sababu hapa linazungumziwa suala la ubaguzi lakini mara nyingi tunapokuwa tunarejea Ibara ya 13(2) kuhusu mambo ya ubaguzi huwa tunasahau kurejea pia Ibara ya 13(5) inayoeleza ubaguzi ni nini. Ujisoma Ibara hiyo utaona kwamba katika jambo hili hakuna ubaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sheria ya Vizazi na Vifo, tumepokea maoni kuhusu kutoa mafunzo kwa wale watakao kaimu majukumu ya Msajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na hasa hapa inagusa makosa yaliyoachwa kwenye orodha ya makosa ambapo *plea bargaining* inaweza kutumika. Majibu yetu ni kwamba nadhani hii tayari ni hatua tumepeiga na tuone sheria itaendaje na sheria inaishi, pakionekana tena kuna haja ya kurekebisha maeneo hayo tutaleta marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Sheria ya Kurejesha Wahalifu (*Extradition Act*) hapakuwa na hoja kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Sheria ya Mashauri yanayohusu Serikali (*Government Proceedings Act*) hapakuwa na hoja kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mahakama za Mahakimu (*Magistrates Courts Act*) pia hapakuwa na hoja kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Sheria ya Taifa ya Mashitaka ambayo inaendana na ile Sheria ya Taasisi ya Kupamba na Kuzuia Rushwa palikuwa na changamoto kidogo kuhusiana na mamlaka ya *DPP*. Na hapa tena nisingependa kuharibu maelezo mazuri kabisa ambayo Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mchengerwa ameyatoa kuyaeleza hapa. Kwa hiyo, ningeomba labda niache hivyo hivyo. Lakini tukiangalia katika jedwali la Serikali aya ya heneo hili limeboreshwa vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sheria ya Mapato ya Uhalifu (*Proceeds of Crime*) kumetokea hoja nzito inayogusa suala la mali inayohusishwa na uhalifu na hasa lile suala la kurudi nyuma kwa miaka 5. Ninapenda kutoa taarifa kwamba Serikali imelitafakari hili kwa kina na kwa sababu ya usikivu wake imeamua kufuta kabisa hicho kipengele c kilichokuwa kinafanya rejea ya miaka 5 na hii tumeileta kwenye jedwali la pili la marekebisho ya Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hoja zake na majibu yake ni kama ile Sheria ya Mawakili na kama nilivyosema Mheshimiwa Mchengerwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria amelieleza vizuri sana, isingefaa tena kuharibu maelezo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sheria ya Chama cha Msalaba Mwekundu (*Tanganyika Red Cross Society*) kulikuwa na wasiwasi kwamba imepelekwa kwenye Wizara isiyo ya Muungano. Na hapa nimeona ni vema nieleze kidogo, katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kimsingi tuna masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano na kwa hiyo na Wizara nazo zinafuata mpangilio huo na kwa kweli Kikatiba si sahihi sana kusema kuna Wizara ya Muungano na Wizara isiyo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini basi kama alivyoeleza Mheshimiwa Ally Saleh ambaye ndiye aliibua hoja hii, jambo hili la masuala haya ya *Red Cross Society* na *Red Crescent Society* imetokana na Mikataba ya Kimataifa. Na Mikataba ya Kimataifa ni masuala yanayohusu mambo ya nje na haya mambo ya nje ni masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuhitimisha, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri, tumepokea maoni mazuri ambayo yamelenga kuboresha si Muswada tu bali hata masharti mengine ya sheria mama na kwa ujumla maoni na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni ushahidi kwamba suala la marekebisho ya sheria kwa lengo la kuboresha utekelezaji madhubuti wa sheria zilizopo linamuhusu kila mmoja wetu na ni jambo endelevu ndiyo maana kila mwaka Serikali inakuja na Muswada wa aina hii illi kuboresha masharti ya sheria zetu na kuzifanya ziendane na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa shukrani hizo, naomba tena kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono, Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA BUNGE ZIMA

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria
Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2019
(The Written Laws Miscellaneous Amendments
(No. 4) Bill, 2019)**

MWENYEKITI: Tukae, Katibu.

Ibara ya 1
Ibara ya 2

Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5

*(Ibara ya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 6
Ibara ya 7

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 8

*(Ibara ya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 9

*(Ibara ilizotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12

*(Ibara ya ziliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

*(Ibara zillzotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 16

*(Ibara ya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebishi ya Serikali)*

Ibara ya 17

Ibara ya 18

Ibara ya 19

Ibara ya 20

Ibara ya 21

*(Ibara zillzotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 22

*(Ibara ya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebishi ya Serikali)*

Ibara ya 23

Ibara ya 24

Ibara ya 25

*(Ibara zillzotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 26

*(Ibara ya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebishi ya Serikali)*

Ibara ya 27

Ibara ya 28

Ibara ya 29

Ibara ya 30

Ibara ya 31

Ibara ya 32

Ibara ya 33
Ibara ya 34

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 35

*(Ibara ya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 36

*(Ibara ilizotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 37

*(Ibara ya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 38
Ibara ya 39
Ibara ya 40
Ibara ya 41
Ibara ya 42
Ibara ya 43

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 44

*(Ibara ya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47
Ibara ya 48

*(Ibara zillzotajwa hapo juu zillpitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 49

*(Ibara ya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 50

*(Ibara illzotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 51

*(Ibara ya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 52

*(Ibara zilizotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa Kamati ya
Bunge Zima imemaliza kazi yake.

(Bunge Lilitrudia)

MWENYEKITI: Tukae, mtoa hoja.

T A A R I F A

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa
Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 89(1) ya Kanuni za
Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 napenda kutoa
taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada
wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 wa

Mwaka 2019 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 4 Bill, 2019*) ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 4 wa Mwaka 2019 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 4 Bill, 2019*) kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(*Makofi*)

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja illiamuliwa na Kuafikiwa*)

MWENYEKITI: Wameafiki wote, Katibu. (*Makofi*)

NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali zipatazo Kumi na Moja (11) kwa Lengo la Kuondoa Mapungufu ambayo yamejitokeza katika Sheria hizo wakati wa Utekelezaji wa Baadhi ya Masharti katika Sheria hizo (*A Bill for an Act to amend Certain Written Laws*)

(*Kusomwa Mara ya Tatu*)

(*Muswada wa Sheria wa Serikali Ulipitishwa na Bunge*)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge kwa hatua hii kazi ya Bunge imekwisha, tukupe hongera Mheshimiwa AGna Serikali kwa ujumla lakini nikupe hongera

Mwenyekiti wa Kamati na Kamati yako mmefanya kazi nzuri lakini niwapongeze vilevile Kambi ya Upinzani maombi yao ya kurekebisha yamekubaliwa imeonekana namna tunavyo *caucus* na tunavyofanya kazi pamoja kati ya vyama ndani ya Bunge. Mheshimiwa AG hongera sana kwa kazi nzuri, Mungu akujaalie; sasa imebaki hatua ya kwenda mamlaka ya juu ambao wao ndio watakaomalizia na kuifanya sasa kuwa ni sheria.

Baada ya maneno haya, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. (*Kicheko*)

*(Saa 11. 24 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,
Tarehe 5 Septemba, 2019, Saa Tatu Asubuhi)*